# HEKIMA YA

# MAFUNDISHO YA KIISLAMU

Na

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as]

Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyyah

Mfasiri

Jamil R. Rafiq

Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyyah Tanzania

*Hekima Ya Mafundisho Ya Kiislamu*
Tafsiri ya Kiswahili ya *Islami Usul Ki Filasfi*

© Islam International Publications Ltd.

Chapa ya Kwanza ya Kiurdu: Qadian 1893
Chapa ya Kwanza ya Kiswahili: Kenya 1987
Chapa ya Pili ya Kiswahili iliyodurusiwa: 2010
Nakala: 2000

Kimeenezwa na:
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyyah, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed
S.L.P. 376, Dar es Salam.
Simu: +255222110473
Fax: +255222121744

Kimechapwa na:
Ahmadiyyah Printing Press
Dar es Salam, Tanzania
Simu: +255222111031

Msanifu na Mchoraji: Sharifu Tanwir Mujtaba

ISBN: 978-1-84880-531-6

# YALIYOMO


**DIBAJI ........................................................................ VII**

**NENO LA MBELE ........................................................................IX**

**ISLAM........................................................................ 1**

KILA DAI NA KILA HOJA NI LAZIMA VITOKANE NA KITABU KILICHOFUNULIWA........................................................................ 1

**SWALI LA KWANZA ........................................................................ 3**

**HALI ZA BINADAMU ZA MAUMBILE, KHULKA NA ROHO..................... 3**

NAMNA TATU ZA HALI ZA KIBINADAMU ........................................................ 3

ROHO IMEUMBWA ........................................................................ 17

KIPAMBANUZI BAINA YA HALI ZA KITABIA NA ZA KIKHULKA NA KUBATILISHA IMANI YA KUAFUA UZIMA ........................................ 21

NJIA TATU ZA KUREKEBISHA: ........................................................ 24

SHABAHA HASA YA KURANI TUKUFU NI MAREKEBISHO MATATU............ 27

KHULKA HASA........................................................................ 30

KHALQ NA KHULQ ........................................................................ 31

KUHARIMISHA NGURUWE ........................................................ 40

HALI ZA KHULKA ZA MTU ........................................................ 42

KHULKA KUHUSU KUEPUKANA NA UBAYA ........................................ 43

TIBA TANO ZA KUHIFADHI UTAWA ................................................ 48

NJIA ZA KUTENDA MEMA........................................................ 59

USHUJAA WA KWELI ........................................................ 69

UKWELI ..... 72
SUBIRA ..... 74
KUWAHURUMIA VIUMBE ..... 76
KUTAFUTA DHATI TUKUFU ..... 77
HEKIMA YA KUDHIHIRIKA KWA MTUME[saw] UARABUNI ..... 81
HISANI YA KURANI TUKUFU KWA DUNIA NZIMA ..... 82
HOJA ZA KUWEPO KWA MUNGU MWENYE ENZI ..... 84
SIFA ZA MWENYEZI MUNGU ..... 88
DUA MOJA YA KUPENDEZA ..... 101
UHAKIKA WA SHARUBATI YA KAFURI NA YA TANGAWIZI ..... 109
ATHARI YA TANGAWIZI ..... 111
NJIA YA KUUNGANA KIROHO NA MWENYEZI MUNGU KIKAMILIFU ..... 120

**SWALI LA PILI ..... 125**

**HALI YA MTU INAKUWAJE BAADA YA KUFA? ..... 125**
MAARIFA YA NAMNA TATU ..... 130
KUHUSU AKHERA ..... 130
ULIMWENGU WA AINA TATU ..... 134

**SWALI LA TATU ..... 149**

**NINI SHABAHA YA MAISHA YA BINADAMU KATIKA DUNIA NA NI NJIA GANI YA KUIPATA? ..... 149**
NJIA ZA KUPATA SHABAHA YA MAISHA YA MTU ..... 152

**SWALI LA NNE ..... 161**

**NINI ATHARI YA VITENDO KATIKA DUNIA NA AKHERA? ..... 161**

HEKIMA YA MWENYEZI MUNGU KUAPA KWA VITU MBALIMBALI.......... 164

**SWALI LA TANO ........................................................ 173**

**NI ZIPI NJIA ZA KUPATA ELIMU YA ROHO? ....................................173**

UHAKIKA WA UMBİLE LA MTU................................................................ 178

SIFA MAALUM YA ISLAM......................................................................... 186

MSEMAJI AMEJAALIWA KUPATA UFUNUO ............................................ 187

NJIA YA KUPATA ELIMU KAMILI NI UFUNUO WA MUNGU...................... 188

ZAMA MBILI ZA MAISHA YA MTUME[saw].................................................... 193

SHABAHA YA VITA VYA MTUME[saw] ......................................................... 198

بِسۡمِ اللّٰهِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِيۡمِ

# DIBAJI

Kwa Toleo La Pili

Nafurahi kuweka mbele ya wasomaji toleo la pili la kitabu hiki *Hekima ya Mafundisho ya Kiislamu* kilichotolewa kwa Kiswahili mara ya kwanza mnamo mwaka 1987.

Ningependa kuwaeleza wasomaji ya kwamba kitabu hiki kilipochapishwa kwa Kiurdu mara ya kwanza, kwa bahati sehemu fulani ya muswada wake haikupata kuchapishwa. Jambo hili limegunduliwa baada ya kulinganisha kitabu hiki na muswada wake wenyewe uliopo hadi sasa salama katika Maktaba ya Ukhalifa, mjini Rabwah, Makao Makuu ya Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyyah.

Sehemu hiyo imekwisha ingizwa katika toleo la Kiurdu la mwaka 2008 la kitabu hiki, nayo imefasiriwa kwa Kiswahili na mfasiri mwenyewe wa kitabu hiki, Maulana Sheikh Jamil R. Rafiq, na imeingizwa katika toleo hili lililo mkononi mwenu. Sehemu hiyo yaanzia kutokea uk 12 hadi uk 17.

Toleo hili la pili limeshughulikiwa na

Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani, Sheikh Mubarak Mahmud, Sheikh Ansar Hussain, Dkt. Muhammad Shafiq Sehgal, na Sharifu Tanwir Mujtaba

katika *Deski ya Kiswahili*, Makao Makuu Rabwah, Pakistan.

Hao wote walioshughulikia kazi hii wanastahili kushukuriwa na kuombewa. Mwenyezi Mugu Awajaalie malipo bora na Akubali huduma yao. Amin.

Chaudhry Muhammad Ali M.A.
Wakilut Tasnif
Tahrik e Jadid
Rabwah. Pakistan
07.06.2010

## Neno la Mbele

Bwana mmoja, jina lake Swami Shugan Chandar, aliyeendelea kwa miaka mitatu minne hivi kushughulikia kazi ya kuirekebisha na kuihudumia jamii Kaisth ya Mabaniani, alipata wazo mnamo mwaka 1892 kwamba kutakuwa hakuna faida yoyote mpaka watu wote wajumuike pamoja. Hatimaye akafikiria kuitisha mkutano mmoja wa kidini. Basi mkutano wa kwanza wa aina hiyo ukafanyika mjini Ajmer. Kisha mnamo mwaka 1896 kwa kuona mji wa Lahore unafaa kwa mkutano wa pili akaanza kufanya matayarisho yake.

Bwana Swami akaunda kamati moja kwa kusimamia matayarisho ya mkutano huo wa kidini, ambao mwenyekiti wake alikuwa Master Durga Parshad, na katibu Mkuu akawa mwana sheria Baniani wa Mahakama Kuu ya Lahore, jina lake Lala Dhanpat Rae, B.A., LL.B.

Mkutano ulipangwa kufanyike tarehe 26, 27 na 28 Desemba 1896, na kwa kuendesha mkutano wasimamizi sita wafuatao wakateuliwa:

1. Rae Bahadur Babu Partol Chand, Jaji wa Mahakama Kuu ya Panjab.

2. Khan Bahadur Sheikh Khuda Bakh-sh, Jaji katika Mahakama ya Lahore kuhusu madai madogo.

3. Rae Bahadur Pandat Radha Kishan, mwana sheria wa Mahakama Kuu, Gavana wa zamani wa Jammu.

4. Hadhrat Maulawii Hakim Nuruddin[ra] , Tabibu wa mfalme.

5. Rae Bhwani Das, M.A., Extra Settlement Ofisa, Jhelum.

6. Sardar Jawahir Singh, katibu wa Kamati ya Masingasinga, Lahore.

(Taarifa ya Mkutano Mkuu wa Dini, uk.b, Chapa ya Matba‘ Siddiki, Lahore, 1897)

Swami Shugan Chandar akitoa tangazo la Mkutano kwa niaba ya kamati akawasisitizia kwa kiapo Waislamu, Wakristo na Waarya kwamba Maulamaa wao wachukue jukumu la kueleza mkutanoni mazuri ya dini zao. Na akaandika kuwa Mkutano Mkuu wa dini uliopangwa kufanyika mjini Lahore katika Ukumbi wa Mji, makusudio yake ndiyo tu kwamba sifa bora kamilifu na mazuri ya dini ya kweli yakidhihirika katika mkusanyiko wa watu wote waliostaarabika, upendo wake upenye nyoyoni na watu wazingatie vizuri dalil zake na hoja zake. Na kwa njia hii mhubiri mheshimiwa wa kila dini apate nafasi ya kuwahakikishia wengine kweli za dini yake, na wasikilizaji pia wapatiwe nafasi ya kulinganisha hotuba ya mmoja na hotuba ya mwingine katika hafla

hiyo ya waheshimiwa wote, na pale wapatapo mng’aro wa ukweli waukubali.

Na siku hizi, kwa sababu ya ubishi wa kidini mnapatikana hamu pia nyoyoni kwa kutambua dini ya kweli. Kwa hiyo njia bora zaidi inayoonekana ndiyo hii tu kwamba waheshimiwa wote wa dini wenye tabia ya kutoa waadhi na nasaha wawepo mahali pamoja na waeleze mazuri ya dini zao wakitoa majibu ya maswali yaliyokwisha tangazwa tayari. Basi, katika kusanyiko hili la wakuu wa dini mbalimbali, ile dini iliyotoka kwa Mungu wa kweli lazima itaonyesha mng’aro wake wazi wazi. Kwa shabaha hiyo, mkutano huu umependekezwa kufanyika. Na mhubiri mheshimiwa wa kila kaumu anatambua sana kwamba kudhihirisha ukweli wa dini yake ndiyo faradhi yake. Hivyo, kwa kuwa mkutano umepangwa kufanyika kwa shabaha hii kwamba kweli zidhihirike, basi Mwenyezi Mungu Amewajaalia nafasi nzuri ya kutimiza shabaha hiyo ambayo haiwezi siku zote katika hiari ya mtu.

Kisha akiwachochea akaandika:

'Je, naweza kukubali kwamba mtu anayewafikiria wengine kwamba wanaugua maradhi ya kuhilikisha, tena anayakini usalama wao umo katika dawa aliyo nayo, na anadai pia kuwahurumia wanadamu, yeye mtu huyo anaweza kupiga chenga kusudi pindi wagonjwa maskini wanapomwita ili kuwatibu? Moyo

wangu una kiherehere kwamba shauri ikatwe mara moja kwamba dini ipi kwa hakika imejaa mambo ya kweli na yaliyo haki. Sijui yale maneno ambayo kwayo niweze kufafanua shauku hiyo yangu ya kweli.'

Wajumbe wa dini mbalimbali waliitikia mwito wa Bwana Swami kwa kushiriki katika mkutano huo wa dini, ama Mkutano Mkuu wa Dini, mjini Lahore. Na mnamo Desemba 1896, katika likizo za Krismasi mkutano mmoja mkuu wa dini ulifanyika mjini Lahore ambamo wajumbe wa dini mbalimbali wakatoa hotuba wakijibu maswali matano yaliyokwisha tangazwa na kamati ya mkutano, ambayo yalikuwa yamechapishwa kwa kujibiwa. Na kwa kuyajibu, sharti iliwekwa na kamati ya kwamba mtoaji hotuba kadri awezavyo atoe jawabu kutokana na kitabu alichokwisha amini kuwa kitakatifu kidini.

Maswali yenyewe yalikuwa haya:

1. Hali za binadamu za maumbile, khulka na roho.

2. Nini hali ya mtu baada ya kufa?

3. Nini shabaha ya maisha ya binadamu katika dunia na ni njia gani ya kuipata?

4. Nini athari ya vitendo katika dunia na akhera?

5. Ni zipi njia za kupata elimu ya kiroho?

(Taarifa ya Mkutano Mkuu wa Dini, uk.b, iliyo-chapishwa katika kiwanda cha uchapishaja cha Siddiki, Lahore, 1897)

Katika mkutano huu uliofanyika kutoka Desemba 26 hadi Desemba 29, wajumbe wa Sanatan Dharma, Ubaniani, Free Thinker, Brahmu Theosophical Society, Religion of Harmony, Ukristo, Islam na Usingasinga walihutubia, lakini katika hotuba hizo zote, hotuba moja tu pekee ilikuwa ni jawabu hasa na kamilifu la maswali hayo. Hotuba hiyo alipokuwa anaisoma Hadhrat Maulawii Abdul Karim wa Sialkot kwa sauti tamu kabisa, hali ya wakati huo haiwezi kuelezeka. Kulikuwa hamna mtu aliye mfuasi wa dini yoyote iwayo asiyelazimika kupiga makelele ya kuisifu na kuitukuza. Hakuna mtu asiyekuwa amevutika mno na kusahau mengine yote. Njia ya kueleza ilikuwa yenye kuvutia sana na kuwapendeza wote. Uhakikisho gani mwingine wa uzuri wa makala hiyo unahitajika kwani hata wapinzani nao walikuwa wanaisifu mno. Gazeti maarufu la Kiingereza, Civil and Military Gazette, Lahore, ingawaje ni la Kikristo likaisifu sana sana hiyo tu na likaonelea hiyo tu kuwa ilistahili kutajwa.

Makala hiyo ilikuwa imeandikwa na Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian. Kwa kuwa makala hiyo haikumalizika katika muda uliokuwa umewekwa, ambao ulikuwa masaa mawili, siku ya 29 Desemba ikaongezwa. Gazeti la 'Punjab Observer' likajaza safu

kwa safu likisifu makala hiyo. Magazeti ya 'Paisa Akhbar', 'Chaudavin Sadii', 'Sadikul Akhbar', 'Mukhbir' Dakkan, 'General wa Gauhar Asafii' la Kalkatta, na mengineyo kwa pamoja yakaisifu ajabu makala hiyo. Mataifa mengine na wafuasi wa dini nyingine wakaikubali kuwa imezishinda makala nyingine zote.

Katibu wa mkutano huu wa kidini, Bwana Dhanpat Rae, B.A. LL.B, wakili wa Mahakama Kuu ya Panjab, aliandika kuhusu hotuba hiyo ndani ya kitabu 'Tarifa ya Mkutano Mkuu wa Dini' kwamba:

'Baada ya hotuba ya Pandat Gurdhan Das, kulikuwa na nafasi ya nusu saa ya kupumzika, lakini kwa kuwa baadaye ilikuwa imepangwa hotuba ya mwakilishi maarufu wa Islam, hivyo washabiki wengi hawakuinuka kabisa. Muda mwingi ulibaki kutimia saa 7:30, lakini uwanja wenye wasaa mkubwa wa Chuo cha Islamia ulijaa kabisa katika dakika chache. Ilikuwa ni hafla ya watu wapatao elfu saba hadi elfu nane. Wataalamu wengi wa dini, madhehebu na vyama mbalimbali walikuwepo. Ijapokuwa viti, meza na matandiko vitiletwa kwa wingi, lakini mamia ya watu hawakuwa na budi kusimama. Miongoni mwa hao waliolazimika kusimama walikuwepo matajiri wakubwa, viongozi wa Panjab, wataalamu, mawakili, maprofesa, madaktari na kadhalika wakuu wa idara mbalimbali. Kukusanyika kwa watu hao hivyo, na

kusikililza kwa masaa manne au matano kwa shauku na jazba kwa kusimama, kunadhihirisha jinsi walivyopenda Mwendeleo huu mtukufu. Mwandishi wa hotuba hakuweza kuhudhuria binafsi mkutanoni, lakini alikwisha mtuma mwanafunzi wake maalum, Maulawii Abdul Karim Sialkoti, ili kusoma makala yake. Ingawaje masaa mawili tu yaliwekwa na kamati kwa makala hiyo kusomwa, lakini wasimamizi wa mkutano walipoona shauku na kiherehere cha wasikilizaji wa makala hiyo, wakaruhusu kwa furaha kwamba mkutano utaendelea hadi makala hiyo ipate kusomwa kikamilifu. Uamuzi huo uliafikiana na maoni ya wasikilizaji, kwani nafasi iliyokuwa imewekwa kwa makala hiyo ilipokwisha, mara Sheikh Abu Yusuf Mubarak alitoa nafasi ya hotuba yake ili makala hiyo ipate kumalizika, na hapo wasikilizaji na wasimamizi wakamtolea shukurani Sheikh huyo kwa kupaaza sauti kwa furaha. Mkutano ungemalizika saa 10:30 sawa na ratiba, lakini kwa kuangalia shauku ya watu wote mkutano uliruhusiwa kuendelea hadi saa 11:00. Kwani makala hiyo ilichukuwa masaa manne takriban, na ilisikilizwa tangu mwanzo hadi mwisho kwa uchangamfu na upendo wa namna moja.'

(Taarifa ya Mkutano Mkuu wa Dini, Ukurasa. 79,80, iliyochapwa katika kiwanda cha uchapishaji wa Siddiki, Lahore).

## 'HABARI KUU NJEMA KWAWATAFUTAO UKWELI'

Katika Mkutano[1] Mkuu wa Dini utakaofanyika katika Ukumbi wa Mji wa Lahore, tarehe 26, 27 na 28 Desemba 1896, makala yangu kuhusu ubora na miujiza ya Kurani Tukufu itasomwa. Makala hii inazidi uwezo wa kibinadamu na ni ishara mojawapo katika ishara za Mungu na imeandikwa kwa msaada Wake maalum. Ndani yake kweli na maarifa ya Kurani Tukufu vimeandikwa vitakavyohakikisha kama jua ling'aavyo kwamba kwa kweli Kurani Tukufu ndiyo Neno la Mungu na Kitabu cha Mola wa walimwengu. Na mtu yeyote atakayesikiliza kwa makini majibu ya maswali yote matano yaliyoelezwa ndani ya makala hii, tangu mwanzo hadi mwisho, nina yakini kwamba ndani ya mtu huyo imani mpya itazalika na nuru moja mpya itang'aa nafsini mwake,

---

[1] Swami Shugan Chandar aliwasisitizia kwa kiapo Waislamu, Wakristo na Waariya kwamba wasikose kabisa wataalamu wao maarufu kueleza mazuri ya dini zao. Basi twampasha bwana Swami habri ya kwamba kwa sababu ya heshima ya kiapo hicho kikubwa tumekuwa tayari kutimiza utashi wako, na Mungu Akipenda, makala yetu itasomwa katika Mkutano wenu. Islam ndiyo dini inayomwagiza Mwislamu wa kweli kutii kikamilifu iwapo jina la Mungu linaingia ndani. Lakini sasa tutaangalia kwamba ndugu zenu Waariya na Mapadre wanaitunza kiasi gani heshima ya Parmeshar (Mungu) wao au Yesu, na wako tayari kuhudhuria kwa jina la Mtukufu Mkuu au hapana? Mwandishi.

na atapata mkononi mwake maelezo makamilifu ya Neno Takatifu la Mwenyezi Mungu.

'Hotuba yangu imeepukana na upuuzi wa kibinadamu wala haina doa la majivuno. Huruma ya binadamu imenilazimisha wakati huu kutoa tangazo hili, ili wakashuhudie uzuri na jamali ya Kurani Tukufu na wazingatie kwamba wapinzani wetu wanadhulumu namna gani kwa kulipenda giza na kuuchukia mwanga. Mungu Aliye Mjuzi wa mambo ya ghaibu Amenijulisha kwa ufunuo kwamba Makala hii itazishinda makala zote zingine. Na ndani yake kuna nuru ya ukweli, hekima na maarifa ambayo watu wa mataifa mengine, wawe Wakristo au Wasanatan Dharm au wowote wengine, wakihudhuria na kusikiliza kwa makini tangu mwanzo hadi mwisho, wataona haya wasiweze kuonyesha ubora huo kutoka katika vitabu vyao vya dini. Kwani Mwenyezi Mungu Amekusudia kudhihirisha shani ya Kitabu chake Kitukufu siku hiyo.'

'Kuihusu hiyo niliona katika kashfi kwamba Mkono mmoja kutoka kwa ghaibu ulipigwa juu ya Jumba langu, na kwa sababu ya mkono huo kuligusa Jumba hilo nuru moja ing’aayo ikatokea kutoka katika Jumba na kuenea pembezoni mwake; mwanga wake ukaangukia hata mkono wangu pia. Hapo mtu mmoja aliyekuwa amesimama karibu nami akapaza sauti akisema: Allahu Akbar, Kharibat Khaibar (Mungu ni Mkuu, Khaibar imeanguka). Uaguzi wake ni kwamba

Jumba linamaanisha moyo wangu panaposhukia nuru ambayo nuru hiyo ni maarifa ya Kurani; na Khaibar ni zile dini mbovu ambamo ushirikina na bidaa vimechanganyikana na mtu amepewa cheo cha Mungu; au sifa za Mungu zimeshushwa hadhi. Basi nimehakikishiwa kwamba kwa njia ya makala hii kuenea sana, uwongo wa dini za batili utadhihirika na ukweli wa Kurani utazidi kutapakaa siku hadi siku mpaka utimize duara lake. Kisha nikahamishwa kutoka katika hali hiyo ya kashfi kwenye hali ya kupokea ufunuo, nami nikafunuliwa: Innallaha Ma'aka. Innallaha Yakuumu Ainamaa Kumta. Yaani, Mungu Yupo pamoja nawe. Mungu Anasimama pale usimamapo. Hiyo ni istiara inayomaanisha Msaada wa Mungu.'

'Sipendi kuendelea kuandika zaidi. Nampasha habari kila mmoja ili kuhudhuria Lahore katika tarehe za Mkutano hata kwa kuacha shughuli zingine za muhimu kwa kusikiliza mambo hayo yenye maarifa, kwani kwa kuyasikiliza hayo akili zao na imani zao zitanufaika wasivyotazamia. Amani iwe kwa kila afuataye mwongozo.

Mimi Mirza Ghulam Ahmad kutoka Qadian, tarehe 21 Desemba 1896. '

(Majmu‘a Ishtihar, J.1 uk. 614)

Yafaa yaandikwe hapa chini maoni ya magazeti mawili matatu, kama mfano:

Gazeti la 'Civil and Military Gazette' (Lahore) likaandika:

'Katika mkutano huo, wasikilizaji walivutika kwa moyo wote kwa hotuba ya Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian, ambaye ni mahiri kabisa kuihami na kuitetea Islam. Kwa kusikiliza hotuba hiyo, khalaiki ya wafuasi wa madhehebu mbalimbali walimiminika kutoka mbali na karibu. Kwa kuwa Mirza Sahib hakuweza kuhudhuria binafsi, hivyo hotuba yake aliisoma mwanafunzi wake hodari, Maulawi Abdul Karim Sialkoti. Tarehe 27, hotuba hiyo ilisomwa kwa masaa matatu. Watu waliisikiliza kwa furaha na makini kabisa, lakini bado jawabu la swali moja pekee lilimalizika. Maulawi Abdul Karim aliahidi kusoma sehemu iliyobakia ikiwa atapewa nafasi zaidi. Kwa hiyo, wasimamizi na mwenyekiti walikubali pendekezo la kuongeza siku ya tarehe 29 Desemba.'

Gazeti la Rawalpindi liitwalo 'Chaudavin Sadii' (Rawalpindi) likaandika:

'Katika hotuba zote, hotuba iliyo nzuri zaidi iliyokuwa roho ya Mkutano ilikuwa ya Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian ambayo ilisomwa na mwenye ufasaha Maulawi Abdul Karim wa Sialkot kwa njia nzuri sana. Hotuba hiyo ilimalizika katika siku mbili: ilisomwa kwa masaa manne tarehe 27 Desemba, na kwa masaa mawili tarehe 29 Desemba. Ikamalizika

kwa masaa sita kwa jumla, ambayo inaelekea kujaza kurasa kubwa 100 hivi.'

'Ilmuradi, Maulawi Abdul Karim alianza kusoma hotuba hiyo; lo, ni vizuri sana alivyoanza kuisoma! Wasikilizaji wakajazwa na upendo ajabu. Sauti za furaha na sifa zikasikika kila fungu la maneno liliposomwa; bali wakati mwingine wasikilizaji wakaomba maneno fulani yarudiwe kusomwa. Maisha mazima, masikio hayajawahi kusikia hotuba nzuri ya kupendeza kiasi hiki.'

'Hotuba zilizotolewa na wataalamu wa dini zingine, kwa kweli hazikuweza kujibu hata maswali yaliyoulizwa. Wasemaji wengi walizungumzia swali la nne tu na waliyagusia kidogo sana maswali mengine. Wasemaji wengi walikuwa na maneno mengi lakini bila kiini, isipokuwa hotuba ya Bwana Mirza Sahib aliyetoa majibu makamilifu ya maswali yote mbalimbali ambayo wahudhuriao waliyasikiliza kwa makini na shauku sana na wakayathamini na kuyatukuza.'

'Sisi sio wafuasi wa Bwana Mirza Sahib, wala hatuhusikani naye hata kidogo; lakini hatuwezi kusema kinyume cha adili, wala hakuna mwenye dhamiri safi awezaye kuihalalisha. Bwana Mirza Sahib alitoa majibu ya maswali yote kutoka katika Kurani Tukufu ilivyopaswa, na akapamba mafunzo ya kimsingi na mafunzo mengine ya Kiislamu kwa hoja

za kiakili na dalili za kifalsafa. Ilionyesha shani ya ajabu kuhakikisha kwanza kiakili masaala za kiungu na kisha kusoma Neno la Mungu kama marejeo.'

'Bwana Mirza Sahib hakueleza tu hekima za masaala za Kurani, bali pia akafafanua hekima za maneno ya Kurani na falsafa yake papo hapo. Gharadhi, hotuba ya Bwana Mirza Sahib kwa jumla ilikuwa kamilifu timilifu ambamo lulu zisizohesabika zilikuwa ziking'aa za maarifa na kweli na hekima na siri; na falsafa ya kiungu ilielezwa namna ambavyo wafuasi wa dini zote wakashikwa na butaa. Watu wengi hivyo hawakuhudhuria katika hotuba ya mtu yeyote mwingine jinsi walivyohudhuria kwa wingi wakati wa hotuba ya Bwana Mirza Sahib. Ili kupambanua baina ya hotuba ya Mirza Sahib na hotuba za wasemaji wengine yatosha kusema kwamba wakati wa hotuba ya Mirza Sahib watu walipakimbilia hapo jinsi nyuki waikimbiliavyo asali. Bali katika hotuba ya wengine wasikilizaji wakaanza kuondoka kwa kuchoka na kutokuvutika. Hotuba ya Sheikh Muhammad Husain wa Batala ilikuwa hivi tu ya kawaida; yale yale mawazo ya kisheikh tunayosikia kila siku yakaelezwa. Haikuwa na jambo lolote jipya. Katika wakati wa hotuba ya sheikh huyo watu kadha wakaondoka; tena sheikh hakuruhusiwa hata dakika chache zaidi ili amalize hotuba yake.' (Gazeti la 'Chaudavin Sadii', la 1 Feb. 1897)

Gazeti la 'General wa Gauhar Asfii' la Kalkatta katika toleo lake la 24 Januari 1897 likaandika chini ya vichwa viwili vya maneno: 'Mkutano Mkuu uliofanyika Lahore' na 'Ushindi wa Islam' hivi:

'Kabla hatujazungumzia taarifa ya mkutano, yatubidi kuwaambia kwamba katika safu za gazeti letu, kama wasomaji wajuavyo, ilikwisha jadiliwa kuwa nani ataifaa kuwa wakili wa Islam katika Mkutano Mkuu wa dini. Kwanza kabisa mwandishi wetu mmoja mheshimiwa kwa mawazo safi na kwa kuzingatia haki alitoa rai ya kumteua Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad, Mtemi wa Qadian, na mhemshiwa wetu mwingine naye katika barua yake kwa bahati akaafikiana na rai hiyo. Maulawii Seyyid Muhammad Fakhruddin Fakhri kuhusu uteuzi huo akawachagua kwa rai yake huru yenye thamani iliyokuwa na nguvu ya hoja majina ya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad, mtemi wa Qadian, na Mheshimiwa Sir Seyyid Ahmad wa Ali Garh, na pia akawapigia kura Maulawii Abu Said Muhammad Husain wa Batala, Maulawii Haji Seyyid Muhammad Ali wa Kanpur na Maulawii Ahmad Husain wa Adhimabad kuwa mawakili wa Kiislamu. Yafaa hapa kueleza pia kwamba mwandishi mmoja wa gazeti moja la hapa akamchagua Maulawii Abdul Haq wa Delhi, mwandishi wa Tafsiri Haqqani kwa kazi hii.'

Kisha akinukuu sehemu ile ya tangazo la Swami Shugan Chandar ambamo yeye akawachochea

wataalamu wa dini mbalimbai na kuwaalika waje kuonyesha uzuri wa dini zao, gazeti hili laandika:

'Kwa kuangalia matangazo ya mkutano huu na kwa kualikwa huko, wataalamu gani wa India wakawa na ari ya kuonyesha hamu ya kuwakilisha dini tukufu ya Kiislamu na kuchukua jukumu la kuihami dini ya Kiislamu wakajibidiisha kiasi gani ili kutilia nyoyoni mwa wafuasi wa dini nyingine heba ya Kurani kwa njia ya hoja na dalili?

Tumepata kujua kutokana na njia ya kutegemewa kwamba wahusika wa mkutano waliwaandikia hususan Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad na Sir Seyyid Ahmad ili washiriki mkutanoni. Hadhrat Mirza Sahib ingawaje hakuweza kuhudhuria binafsi mkutanoni kwa sababu ya kuwa na afya yake isiokuwa nzuri, lakini akatuma makala yake na akamteua mwanafunzi wake maalumu Maulawii Abdul Karim Sialkoti ili kuisoma mkutanoni. Lakini Bwana Sir Seyyid Ahmad akajiweka kando asishiriki katika mkutano wala hakutuma makala. Hiyo haikuwa kwa sababu yu mzee basi hawezi kushirika katika mikutano ya aina hii, wala haikuwa kwa sababu katika siku hizo hizo ulikwisha wekwa Mkutano wa Elimu huko Merati, bali sababu yake ilikuwa kwamba haijali mikutano ya dini, kwani akaandika kwa uwazi katika barua yake ambayo tutaitoa gazetini mwetu wakati mwingine Insha Allah, kwamba yeye si mtoa mawaidha au nasaha wala si sheikh; kazi hii ndiyo ya watoa waadhi

na nasaha. Kwa kuangalia ratiba ya mkutano na pia kwa kufanya uchunguzi tumejuta kujua kwamba Maulawii Seyyid Muhammad Ali Kanpuri, Maulawii Abdul Haq wa Delhi na Maulawii Ahmad Husain Adhimabadi nao hawakuonyesha shauku kwa mkutano huu, wala miongoni mwa kundi la maulamaa mtaalamu yeyote hakueleza nia yake ya kusoma makala ama kutuma makala kwa kusomwa. Naam, mtaalamu mmoja ama wawili wakapiga moyo konde na kukanyaga humo lakini kinyume. Hivyo, ama hawakuzungumzia chochote kuhusu madhumuni iliyowekwa kujadiliwa ama wakapayuka tu ovyo kama itakavyobainika kutokana na taarifa yetu ya baadaye. Ilmuradi, inayothibitika kutoka katika taarifa ya mkutano ni kwamba Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad, mtemi wa Qadian, peke yake ndiye aliyetimiza wajibu wa kuishindania Islam katika uwanja huu wa mashindano, na akauhakikisha uchaguzi huo kuwa sawa kwa kuteuliwa kwake kuwa mwakilishi wa Kiislamu na kutiliwa sahihi na wawakilishi wa madhehebu mbalimbali ya Kiislamu kutoka Peshawar, Rawalpindi, Jhelum, Shahpur, Bhera, Khushab, Sialkot, Jammu, Wazirabad, Lahore, Amritsar, Gurdaspur, Ludhiana, Shimla, Delhi, Ambala, Riasat Patiala, Kapur Thala, Dera Dun, Ilahabad, Madras, Bombay, Haidarabad Dakkan, Binglor, na sehemu nyinginezo za India. Ukweli wenyewe unaothibitika ni kwamba kama si makala ya Hadhrat Mirza Sahib, Waislamu wangedhalilika na

kujuta mbele ya wafuasi wa dini zingine. Lakini Mkono wenye nguvu wa Mungu Uliihami dini tukufu ya Kiislamu isianguke; bali kwa njia ya makala hiyo Islam ikapata ushindi hata kwamba achilia mbali marafiki, maadui nao wakatamka kwa jazba ya kitabia kwamba makala hii imezishinda makala zote, imezishinda makala zote. Bali makala ilipomalizika kusomwa maadui wakakiri wakisema, “Sasa uhakika wa Islam umebainika na Islam imepata ushindi. Uteuzi huu ulihakikika kuwa sawa kabisa kama mshale unaolenga sawasawa katika mwanga wa mchana. Sasa hamna nafasi ya kuupinga uchaguzi huu hata kidogo, bali huo ni sababu ya fahari kwetu na humo mna shani ya Kiislamu, humo mna adhama ya Kiislamu, na hiyo ni kweli kabisa.'

' Ingawaje, hicho kilikuwa ni kikao cha pili cha Mkutano Mkuu wa Dini katika India, lakini hicho kiliishinda mikutano yote na mabaraza yote ya Bara Hindi katika shani, utukufu, jaha na heshima. Humo mlihudhuria machifu wa sehemu mbalimbali za India, na twatoboa kwa furaha kwamba Madras yetu pia imeshiriki katika mkutano huu. Mkutano ukavutia kiasi hiki hata siku moja ililazimika kuongezwa katika siku tatu zilizokuwa zimetangazwa kwa mkutano.'

'Wasimamizi wa Mkutano walichagua jengo la Islamia College lenye wasaa mkubwa sana mjini Lahore, lakini jinsi khalaiki ya watu

walivyosongamana wasaa huo wote haukutosha. Adhama ya mkutano inathibitika vya kutosha kutokana na jambo hili kwamba zaidi ya waheshimiwa wa Panjab nzima, majaji wa Chief Court na mahakama kubwa ya Ilahabad, Mheshimiwa Babu Partol Chandar na Bwana Bennerji wakahudhuria mkutanoni kwa furaha sana.'

Makala hii kwanza ilichapishwa neno kwa neno katika 'Taarifa ya Mkutano Mkuu wa Dini', na matoleo yake kadha kwa Kiurdu na Kiingereza yalichapishwa na Jumuiya ya Ahmadiyyah kwa sura ya kitabu kiitwacho: 'Hekima ya mafundisho ya Kiislamu'. Isitoshe, tafsiri yake kwa Kifaransa, Kidachi, Kihispania, Kiarabu, Kijerumani na lugha nyinginezo imekwisha tolewa tayari. Wanafalsafa maarufu na wahariri wa magazeti na majarida ya nchi za kigeni wakaandika maoni kem kem juu ya makala hii, na wataalamu wenye hekima wa kimagharibi wakaisifu sana. Kwa mfano:

1. 'Bristal Times and Mirror' likaandika: Kwa yakini, mtu azihutubiaye Ulaya na Amerika hivyo hawezi kuwa mtu wa kawaida.'

2. Spirtual Journal, Bostan, likaandika: 'Kitabu hiki ni habari njema halisi kwa wanadamu.'

3. Theosophical Book Notes likaeleza: 'Kitabu hiki ni picha nzuri sana ivutiayo mno ya dini ya Muhammad[saw] .'

4. 'Indian Review' likaandika: Mawazo ya kitabu hiki ni yenye kung'aa, yaelezayo yote yaliyotakikana na yaliyojaa hekima, na msomaji hulazimika kukisifu.'

5. Muslim Review likaandika: 'Msomaji wa kitabu hiki atakuta humo fikira nyingi za kweli, zenye maana ya ndani, za asili na za kusisimua.' (Silsila Ahmadiyyah, utungo wa Hadhrat Sahibzada Mirza Bashir Ahmad r.a. uk. 69)

Uzuri wa makala hii ni kwamba ndani yake dini nyingine yoyote haikushambuliwa, bali mazuri tu ya Islam yameelezwa, na maswali yote yamejibiwa kutoka katika Kurani Tukufu tu namna ambavyo yathibitika Islam kuwa kamilifu, bora na timilifu kuliko dini zote.

Jalal-ud-Din Shams

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ [1]

نَحْمَدُهٗ وَنُصَلِّیْ عَلٰی رَسُوْلِهِ الْكَرِيْمِ [2]

# ISLAM

## KILA DAI NA KILA HOJA NI LAZIMA VITOKANE NA KITABU KILICHOFUNULIWA

Leo nitaeleza uzuri wa dini ya Kiislamu katika mkutano huu ambao shabaha yake ni kwamba kila mmoja aliyekaribishwa aeleze uzuri wa dini yake akijibu yale maswali yaliyokwisha tangazwa mapema. Kabla sijaanza kutoa maelezo yangu, ningependa kuwaambia kwamba nimejilazimisha kuwa lolote nitakaloeleza litokane na Neno Takatifu la Mwenyezi Mungu, Kurani Tukufu. Kwani, sawa na maoni yangu ni lazima kabisa kwamba kila mtu atoapo majibu ya swali lolote, anatakiwa atoe majibu hayo kulingana na mafundisho ya kile kitabu anachoshikilia na anakiamini kuwa ni kitabu cha Mungu; wala asijipanulie eneo la madaraka yake ya kuwakilisha kitabu hicho hadi aonekana kana kwamba yuatunga kitabu kipya. Hivyo, kwa kuwa leo nitahakikisha

---

[1] Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu.

[2] Twamsifu Mungu na kumsalia Mtume Wake Mtukufu.

ubora wa Kurani Tukufu na kudhihrisha ukamilifu wake, yanipasa nisitoe maelezo ya jambo lolote yasiyokuwemo ndani yake, bali nieleze makusudio yote yale yaliyodokezwa au kufafanuliwa mle ndani yake au nitoe maelezo yatokanayo na aya zake moja kwa moja, ili wale ambao wamehudhuria waweze kulinganisha mafundisho ya dini mbalimbali kwa urahisi. Na kwa kuwa kila mmoja anayekiamini kitabu fulani atalazimika kushikamana na maelezo ya kitabu kile, na kunena kulingana na kitabu kile, mimi sitaeleza walau Hadithi za Mtume[saw] katika maelezo yangu, kwani Hadithi zote zilizo sahihi zimetokana na Kurani Tukufu tu ambacho ndicho kitabu kamili kilichojikusanyia vitabu vyote. Ilmuradi, leo ni siku ya kudhihirika shani ya Kurani Tukufu, nami namwomba Mungu Anisaidie katika hii kazi.

# SWALI LA KWANZA

## HALI ZA BINADAMU ZA MAUMBILE, KHULKA NA ROHO

Wasikilizaji waheshimiwa wanapaswa kuzingatia kwamba katika kurasa za mwanzo za makala hii nimetaja baadhi ya mambo yanayoonekana kwamba hayahusikani na madhumuni yenyewe, lakini ni ya muhimu sana ili kuelewa sawasawa majibu yaliyo sahihi. Kwa hiyo nimeyaeleza mwanzoni ili mtu asipate shida kuelewa makusudio.

### NAMNA TATU ZA HALI ZA KIBINADAMU

Ieleweke kwamba swali la kwanza lahusikana na hali za maumbile. khulka na roho za binadamu. Fahamuni basi, kwamba Neno Takatifu la Mungu Mwenye Enzi, yaani Kurani Tukufu, limezitenganisha hali hizi tatu kwa kueleza chanzo tofauti cha kila moja. Au tuseme, ziko chemchemi tatu tofauti zinamobubujika hali hizi tatu.

#### HALI YA KWANZA: NAFSI AMMARAH

Chemchemi ya kwanza iliyo chanzo cha hali zote za ki-maumbile imeitwa Nafsi Ammarah (Nafsi inayoamrisha kutenda maovu) katika Kurani Tukufu kama isemavyo:

إِنَّ النَّفْسَ لَأَمَّارَةٌ بِالسُّوٓءِ [1]

Yaani sifa ya Nafsi Ammarah ni kwamba inamwelekeza mtu kwenye maovu yaliyo kinyume cha ukamilifu wake na dhidi ya hali za khulka bora na inataka kumwongoza kwenye njia mbaya zichukizazo. Ilmuradi, kuelekea kwenye maovu ni hali ya mtu inayomtawala kabla hajaingia katika hali ya ki-khulka. Hali hii huitwa ya ki-maumbile maadamu mtu hatendi tendo fulani kwa kuongozwa na akili na maarifa, bali hufuata tu hali yake ya maumbile kama wanyama, katika mambo ya kula na kunywa, kulala na kuamka, kukasirika na kughadhibika na kadhalika. Lakini mtu anapozitawala hali zake za ki-maumbile kwa kutumia akili, busara na maarifa yake na kuzisawazisha ipasavyo, hapo hali zake hizo haziitwi tena za ki-maumbile bali huitwa hali za kikhulka kama itakavyoelezwa zaidi mbele.

HALI YA PILI: NAFSI LAWWAAMAH

Chanzo cha hali za kikhulka kimeitwa Nafsi Lawwaamah (Nafsi inayojilaumu ikitenda maovu) ndani ya Kurani Tukufu. Kurani Tukufu yasema:

وَلَآ أُقْسِمُ بِالنَّفْسِ اللَّوَّامَةِ ۝٣ [2]

[1] Yuusuf, 12:54
[2] Al-Qiyaamah, 75:3

Yaani, naapa kwa nafsi inayojilaumu kila ikitenda ubaya au ikipita kiasi. Nafsi hii ijilaumuyo ndiyo chanzo cha hali za kibinadamu zinamozalika hali za kikhulka na katika hatua hii mtu anaokoka katika kufanana na wanyama. Hapa kuapa kwa Nafsi Lawwaamah kuna shabaha ya kuitukuza kana kwamba imestahili kupata heshima mbele ya Mungu kwa sababu ya kupata maendeleo kutoka katika hali ya Nafsi Ammarah na kuwa Nafsi Lawwaamah. Imeitwa Lawwaamah kwa sababu inamlaumu mtu juu ya maovu yake wala hairidhiki kwamba mtu aishi kama wanyama na kutimiza mahitaji yake ya ki-maumbile bila kuzingatia baadhi ya masharti na vizuizi. Bali Nafsi Lawwaamah inamtaka mtu aonyeshe hali nzuri na khulka njema, na katika kutimiza mahitaji yote ya maisha ya kibinadamu asipite kiasi asilani, na maono ya kiasili na tamaa za ki-maumbile vidhihirike kwa kutumia akili. Hivyo basi, kwa kuwa nafsi hiyo inamlaumu mtu juu ya mienendo miovu, imeitwa jina la Nafsi Lawwaamah, nafsi ijilaumuyo sana mno. Lakini ingawaje Nafsi Lawwaamah haipendi jazba za ki-maumbile bila kutumia akili, hata hivyo haina uwezo kamili wa kutenda mema barabara na wakati mwingine hali za maumbile zinapata kuishinda. Hapo inateleza na inaanguka. Kana kwamba ni mtoto mnyonge asiyependa kuanguka, lakini huanguka kwa sababu ya udhaifu kisha hujuta kwa unyonge wake. Ilmuradi

hii ndiyo ile hali ya kiadili ya nafsi ambapo nafsi hiyo inajitahidi kujikusanyia khulka njema na kuchukia uasi lakini haiwezi kupata ushindi kamili.

HALI YA TATU: NAFSI MUTMAINNAH

Kisha kuna chemchemi ya tatu inayopaswa kuitwa chanzo cha hali za kiroho. Kurani Tukufu imeiita kwa jina la Nafsi Mutmainnah (Nafsi iliyotulia) kama isemavyo:

يَٰٓأَيَّتُهَا ٱلنَّفۡسُ ٱلۡمُطۡمَئِنَّةُ ٢٨ ٱرۡجِعِيٓ إِلَىٰ رَبِّكِ
رَاضِيَةٗ مَّرۡضِيَّةٗ ٢٩ فَٱدۡخُلِي فِي عِبَٰدِي ٣٠ وَٱدۡخُلِي جَنَّتِي ٣١ [1]

Yaani, Ewe nafsi uliyepata faraja na utulivu kutoka kwa Mungu, rudi kwa Mola wako hali umemridhia Naye Amekuridhia. Basi ingia katika watumishi wangu na ingia katika Pepo Yangu. Hili ndilo daraja ambamo nafsi inaokoka katika unyonge wote na kujaa nguvu za kiroho na inaungana na Mwenyezi Mungu hata kwamba haiwezi kuishi bila kuwa na Yeye. Na jinsi maji kutoka juu yanavyopita kwenye mteremko, na kwa sababu ya kuwa mengi na kukosekana kwa vizuizi yanapita kwa kishindo, hivyo ndivyo nafsi hiyo inavyomwendea Mungu kwa kasi. Hilo ndilo limeashiriwa katika kauli hii ya Mwenyezi Mungu: Ewe nafsi uliyepata faraja, rudi kwa Mola wako. Basi mtu mwenye Nafsi

[1] Al-Fajr, 89:28-31

Mutmainnah anajigeuza kabisa si baada ya kifo bali katika maisha haya haya, na anapata Pepo siyo tu huko akhera bali pia katika dunia hii hii. Na jinsi aya inavyosema, 'Rudi kwa Rabb wako', yaani kwa mlezi wako, basi wakati huo yeye analelewa na Mungu — mapenzi ya Mungu huwa chakula chake na anakunywa maji kutoka katika chemchem hiyo ya uzima na kwa hiyo anaokolewa katika mauti kama Asemavyo Mwenyezi Mungu mahali pengine katika Kurani Tukufu:

قَدْ أَفْلَحَ مَنْ زَكَّىٰهَا ﴿١٠﴾ وَقَدْ خَابَ مَنْ دَسَّىٰهَا ﴿١١﴾ [1]

Yaani, aliyeitakasa nafsi yake kutokana na tamaa za dunia, ameokoka wala hataangamia; lakini yule aliyejificha ndani ya tamaa za dunia ambazo ni jazba za ki-maumbile, yeye mtu huyo amekata tamaa ya kupata uzima.

Basi, hizo ndizo hali za namna tatu zinazoweza kuitwa za maumbile, za khulka na za roho. Na kwa kuwa mahitaji ya ki-maumbile yanapokuwa mengi, huwa yenye hatari sana na mara nyingi huharibu khulka na roho, kwa hiyo miongoni mwa hayo, mengine yameitwa Nafsi Ammarah katika Kitabu Kitakatifu cha Mwenyezi Mungu. Na kama iulizwe kwamba Kurani Tukufu inaagiza vipi kuhusu hali hizo za ki-maumbile za binadamu na inaziruhusu hadi

[1] Ash-Shams, 91:10-11

kiasi gani, basi ibainike kwamba sawa na Kurani Tukufu hali za ki-maumbile zinahusikana sana na hali za kikhulka na za kiroho, kwa kiasi hiki kwamba hata mitindo ya kula na kunywa pia huziathiri hali za khulka na roho. Kama hali hizi za tabia ya kiasili (maumbile) zitumike sawa na maagizo ya sheria, hapo, jinsi kila kitu kinavyokuwa kama chumvi kikiingia katika mgodi wa chumvi, ndivyo hivyo hali hizo zinavyogeuka kuwa hali za kikhulka na zinaathiri sana mno hali za kiroho. Ndiyo sababu Kurani Tukufu imetia sana maanani utakaso wa mwili, adabu za kidhahiri na usawa wa nje kwa kutimiza miradi ya ibada na utakaso wa roho na shabaha ya unyenyekevu. Na ukitafakari, utaona kwamba falsafa hii ndiyo sawa kabisa kwamba hali za kimwili zinaiathiri roho kwa nguvu sana kama tunavyoshuhudia kwamba ingawaje matendo yetu hutendwa na mwili lakini hayana budi kuziathiri hali za roho.

Kwa mfano, ikiwa tunaanza kulia hata kama kwa kujikalifisha, mara tutaona machozi halisi yataanza kutiririka machoni na kuathiri moyo ambao utasikia huzuni kwa kuyafuata macho. Kadhalika tukianza kucheka kwa kujikalifisha, mara moyo nao utachangamka. Pia imeshuhudiwa kwamba sujuda ya mwili nayo huleta unyenkekevu katika roho pia. Na kinyume chake twashuhudia pia kwamba tukitembea kwa kukaza shingo na kutokeza kifua, hali hii ya

kutembea itazalisha maringo na majivuno. Mifano hiyo inahakikisha kikamilifu kwamba bila shaka yoyote hali za kimwili zinaathiri hali za kiroho.

Kadhalika ni jambo la hakika kwamba vyakula vya aina mbalimbali vinaathiri nguvu za akili na moyo. Kwa mfano, angalieni, wale watu wasiokula nyama kabisa hupungukiwa pole pole ushujaa mpaka wanakuwa waoga na wanapoteza kipawa kizuri walichojaaliwa na Mungu. Ushuhuda huu wapatikana pia katika sheria ya ulimwengu iliyowekwa na Mungu kwamba kati ya wanyama walao majani hata mmoja hana ule ushujaa alio nao mnyama mla nyama. Jambo hilo limeshuhudiwa katika ndege pia. Hivyo basi, hapana shaka kwamba vyakula vinaathiri khulka. Naam, wale watu wanaosisitiza kula nyama tu usiku na mchana na hula mboga kidogo sana, hao wanapungukiwa khulka za upole na unyenyekevu. Lakini wanaoshika njia ya wastani ndio wanarithi khulka za aina zote mbili. Kwa sababu ya hekima hiyo Kurani Tukufu inasema:

كُلُوْا وَاشْرَبُوْا وَلَا تُسْرِفُوْا ۚ [1]

Yaani, kuleni nyama pamoja na vitu vingine pia, lakini msipite kiasi katika kutumia chochote kimojawapo ili hali ya khulka isipate kuathirika vibaya na ili wingi huo usiwahi kuharibu afya pia. Na

---

[1] Al-A‘raaf, 7:32

kama matendo ya kimwili yanavyoiathiri roho, ndivyo hivyo wakati mwingine roho nayo inavyouathiri mwili. Kwa mfano, aliyepatwa na huzuni hujaa machozi machoni na mwenye kufurahika moyoni hutabasamu. Vitendo vyetu vyote vya ki-maumbile kama vile kula na kunywa, kulala na kuamka, kutikisika na kutulia, kuoga na kadhalika, vyote hivyo huziathiri hali zetu za roho. Umbo la mwili wetu linalingana sana na ubinadamu wetu. Ukipigwa mahali fulani maalum katika ubongo, mara moja uwezo wako wa kukumbuka mambo hutoweka, na pigo juu ya mahali pengine fulani hupoteza fahamu. Hewa yenye sumu wakati maradhi fulani ya kuambukiza yanapozuka inaathiri haraka kabisa katika mwili na kuingia moyoni, na mara moja mfumo mzima wa khulka huharibika kiasi hiki kwamba mtu anakuwa kama mwenye wazimu na anaaga dunia katika dakika chache. Kwa kifupi, mapigo ya kimwili huonyesha maajabu yanayohakikisha kwamba mwili na roho vina uhusiano fulani ambao kutoboa siri yake si kazi ya binadamu.

Isitoshe, kuna dalili nyingine pia yenye kuhakikisha uhusiano huo. Ukitafakari utajua kwamba mwili ndio mama wa roho. Katika tumbo la uzazi la waja wazito, roho haiingii kotoka nje, bali hiyo ni nuru inayofichikana katika tone la shahawa nayo inang’aa pamoja na ukuaji wa mwili. Maneno Matukufu ya Mwenyezi Mungu yanatufahamisha kwamba katika tumbo la uzazi roho inajidhihirisha kutoka katika

mwili unaoumbika kutokana na shahawa. Mwenyezi Mungu Anasema ndani ya Kurani Tukufu:

ثُمَّ أَنشَأْنَاهُ خَلْقًا آخَرَ ۚ فَتَبَارَكَ اللَّهُ أَحْسَنُ الْخَالِقِينَ ﴿١٥﴾ [1]

Yaani, kisha katika ule mwili ulioumbika katika tumbo, twadhihirisha umbo lingine liitwalo roho. Na ni Mwenye Mibaraka Mungu Aliye Mbora wa waumbao.

Na kauli hii kwamba twalidhihirisha umbo lingine katika mwili huo huo, ni siri ya ndani sana inayotoboa uhakika wa roho na kuashiria kwenye uhusiano ule imara uliopo baina ya mwili na roho. Dokezo hilo pia linatufundisha kwamba matendo ya binadamu na maneno yake na vitendo vyake vya maumbile vianzapo kudhihirika katika njia ya Mwenyezi Mungu vyahusikana pia na hekima hiyo. Yaani mle ndani ya amali njema mnafichikana roho moja tangu mwanzo jinsi inavyofichikana katika tone la shahawa. Na kadiri kiwiliwili cha matendo kinavyotengenezeka ndivyo roho hiyo inavyozidi kung'arika. Na kiwiliwili kinapokamilika, mara roho hiyo hung'aa kwa mwanga wake kamili na inajidhihirisha kuwepo kwake kiroho, na harakati zilizo wazi za uhai zinaanza. Ndiyo kusema kwamba kiwiliwili cha amali kinapokamilika, mara moja kitu fulani kutoka ndani yake kinaanza kuonyesha mwako wake kama umeme. Hizo ndizo

---

[1] Al-Mu'minuun, 23:15

zama ambazo kuhusu hizo Mwenyezi Mungu Anasema kimethali ndani ya Kurani Tukufu:

فَإِذَا سَوَّيْتُهُ وَنَفَخْتُ فِيهِ مِن رُّوحِي فَقَعُوا لَهُ سَاجِدِينَ ۝٣٠ [1]

Yaani, nikamilishapo kiwiliwili chake na kusawazisha maonyesho ya utukufu na kumpulizia Roho Yangu, basi nyote mwangukie katika sujuda kwa sababu yake. Hivyo, aya hiyo pia inadokeza kwamba baada ya kukamilika tengenezo la amali, roho ile inapata kung'aa ndani yake ambayo Mwenyezi Mungu Ameinasibisha Kwake. Kwani, kiwiliwili hicho kinaumbika baada ya maisha ya anasa za kidunia kuangamia; ndiyo maana mwanga huo wa Mungu uliokuwa hafifu hapo mwanazoni, unawaka ghafula kwa nguvu na kumlazimisha kila mmoja kuusujudia ili kushuhudia adhama hii kubwa ya Mungu na kuvutika Kwake. Basi, kila mmoja husujudu kwa kuona Nuru hii na kuiendea isipokuwa Ibilisi alipendaye giza.

[2]**Hapa hapatakuwa pasipo faida kueleza jambo moja jingine jepesi. Nalo ni hili kwamba mtoto aumbikaye katika tumbo la uzazi huwa anaanza kutikisika baada ya miezi minne na siku kumi, na

---

[1] Al-Hijr, 15:30

[2] Maneno toka alama hii (**)hadi alama hiyo tena kwenye ukurasa 17 yamo katika muswada wa asili, lakini hayakupata kuchapishwa katika taarifa ya mkutano wala katika toleo la kwanza (la Kiurdu). Katika toleo hili haya yameingizwa kwa idhini ya Hadhrat Khalifatul Masih V[atba]. [Mwenezi]

muda huo ndio karibu nusu ya muda anaokaa mtoto katika chumba cha faragha cha uterasi. Basi, jinsi ambavyo kijusi, yaani mtoto wa ndani ya uterasi, anadhihirisha dalili ya uhai wake katika mwezi wa nne na anaingia katika hali ya kuwa kiumbe chenye uhai kutoka kwenye hali ya kimimea, ndivyo ilivyo kanuni hiyo katika kuzaliwa kiroho. Yaani, jinsi kijusi kidhihirishavyo alama za uhai na onyesho kamilifu la kuhuika baada ya kukaa nusu ya muda akaao ndani ya chumba cha faragha cha uterasi, ndivyo ikadiriwavyo kwa maisha ya kiroho. Maisha mazuri yasiyoingiliwa na uharibifu wa hisia zake, kwa watu wengi ndiyo mpaka miaka themanini, na nusu ya themanini ni arobaini inayolingana na neno 'nne', yaani, miezi minne ambayo ikiisha timia mtoto wa tumboni mwa uzazi hupata roho ya uhai. Basi, tajiriba sahihi yaongoza kwenye jambo hili kwamba mtu atimizapo, au akurubiapo kutimiza, nusu ya maisha yake mazuri, yaani miaka arobaini ilinganayo na miezi minne ya kukaa katika uterasi, hapo kama anayo roho ya ukweli katika asili yake, basi hiyo roho hudhihirisha katika wakati huo maalum athari zake zilizo wazi na huanza kutikisika.

Jambo hili halifichikani kwa mtu yeyote kwamba kabla ya miaka arobaini, mara nyingi, mtu anatawaliwa na zama za giza; maana, miaka saba, minane hupita utotoni, kisha mtu anashughulikia kupata elimu mpaka miaka ishirini na mitano au ishirini na sita, ama anaipoteza katika mambo ya

kipuuzi. Kisha baada ya hapo kwa sababu ya kuoa na kupata mke na watoto au kwa sababu ya maumbile anatawaliwa na matamanio ya kidunia na huzalika tamaa na shauku ya kupata mali na heshima za kidunia, na ili kujitimizia ladha, huanza kufikiria kupita kiasi; hata akielekea kwa Mungu, huwa na shabaha ya kidunia kiasi kadha; na hata akiomba dua, mara nyingi huomba zaidi kwa ajili ya dunia; na akilia aombapo, pengine shabaha kadha za kidunia huwa zinachanganyika humo. Imani yake juu ya maisha ya akhera huwa dhaifu sana, na hata kama anayo imani hiyo, kipindi cha kuishi kabla ya kufa huonekana kirefu. Na jinsi boma la kuzuia maji ya mto ubomokavyo na kuangamiza ardhi iliyo pembezoni mwake, ndivyo mafuriko ya jazba za kianasa yanavyohatarisha kabisa maisha ya mtu. Katika hali hiyo, yeye anawezaje kuamini mambo mapesi sana ya maisha ya akhera; bali huwa anayacheka na kuyadhihaki mafunzo ya dini na kueleza mantiki yake kavu na falsafa yake ya kipuuzi. Naam, kama yu mwenye tabia njema ya asili, hapo yeye anamwamini pia Mungu, lakini si kwa moyo wala kwa uaminifu hasa, bali kwa sharti tu ya kupata ufanisi katika mambo yake; akipata shabaha za kidunia anakuwa wa Mungu, la sivyo, yu wa shetani.

Ilmuradi, katika umri huo wa ujana hali huwa ya hatari; huruma ya Mungu isiposaidia, mtu huangukia shimo la jahanamu. Ni kweli kabisa ya kwamba umri

huo ndio chanzo cha mabaya yote. Katika umri huo mtu hujipatia magonjwa mengi ya kimwili na maradhi za kutahayarisha. Wakati mwingine kwa sababu ya makosa ya umri huo mbichi anampa kisogo Mungu Asiyebadilika. Ilmuradi, hizo ndizo zama ambamo hofu ya Mungu huwa kidogo, mtu anapenda nyege, na tamaa ya nafsi inamtawala, naye hamsikilizi mshauri. Anapatilizwa hatia za zama hizo maisha mazima. Kisha afikiapo miaka arobaini, joto la ujana laanza kupoa kidogo, hapo hujuta hatia nyingi zile ambazo wenye kunasihi walikuwa wameshindwa vibaya kumwachisha hizo. Na harara za nafsi zaendelea kufifia zenyewe, kwani kimwili pia huanza zama za umri kuchakaa. Yazalika wapi sasa damu ya kuchochea shari iliyokuwa ikizalika hapo kabla! Nguvu zile za viungo na furaha ya kulevya ya ujana iliyokuwa hapo awali yabakia wapi!! Sasa zawadia zama za kurudi nyuma na kuhasiri. Na juu ya hayo, mtu hulazimika kushuhudia vifo vya wazee waliokuwa wenye umri mkubwa sana kuliko yeye, bali pengine kwa kadiri ya Mungu vifo vya wadogo navyo vyavunja moyo. Na mara nyingi katika zama hizo, wazazi nao wanaingia kaburini, na mifano mingi ya kuonyesha kuwa dunia hii siyo ya kudumu yadhihirika. Na Mwenyezi Mungu Anaweka mbele yake kioo kwamba tazama, hiki ndicho kisa cha dunia; na uliyokuwa na uchu wake, mwisho wake ndio huu. Ndipo yeye anazingatia makosa yake ya zamani kwa majuto mkubwa, na humjia mapinduzi

makubwa, na dunia mpya yaanza, sharti tabia yake ya asili ina wema ndani yake, naye yu miongoni mwa wale waliokaribishwa. Kuhusu hiyo Anasema Mungu Mwenye shani tukufu:

وَوَصَّيْنَا الْإِنسَانَ بِوَالِدَيْهِ إِحْسَانًا ۖ حَمَلَتْهُ أُمُّهُ كُرْهًا وَوَضَعَتْهُ كُرْهًا ۖ
وَحَمْلُهُ وَفِصَالُهُ ثَلَاثُونَ شَهْرًا ۚ حَتَّىٰ إِذَا بَلَغَ أَشُدَّهُ وَبَلَغَ أَرْبَعِينَ سَنَةً قَالَ
رَبِّ أَوْزِعْنِي أَنْ أَشْكُرَ نِعْمَتَكَ الَّتِي أَنْعَمْتَ عَلَيَّ وَعَلَىٰ وَالِدَيَّ وَأَنْ أَعْمَلَ
صَالِحًا تَرْضَاهُ وَأَصْلِحْ لِي فِي ذُرِّيَّتِي ۖ إِنِّي تُبْتُ إِلَيْكَ وَإِنِّي مِنَ الْمُسْلِمِينَ ﴿١٦﴾ [1]

Yaani, tumemwusia mwanadamu: Uwafanyie wema wazazi wako. Tazama, mamako alivumilia taabu zipi kwa ajili yako. Akasumbuka kwa muda mrefu kwa himila yako na akakuzaa kwa taabu na uchungu. Kwa himila yako na kwa kukunyonyesha akataabika kwa miezi thelathini. Kisha Anasema: Mtu mwema awapo mwenye umri wa miaka arobaini na kufikia umri wa kupevuka akili, ndipo hukumbuka maagizo ya Mungu na kusema: Ee Mola wangu, nijaalie sasa nishukuru neema zako zilizo juu yangu mimi na wazazi wangu. Ee Mola wangu, nifanyize sasa amali Uiridhiayo. Na kwa ajili yangu Uwarekebishe watoto wangu; yaani, kama nilipata kuwakosea wazazi wangu, isije hao nao wakafanya hivyo; na kama nilipatwa na zama za kuwa mhuni, isije nao wakafikiwa na zama kama hizo. Ee Mungu Wangu, natubu sasa, nami nimekuwa

[1] Al-Ahqaaf, 46:16

miongoni mwa watii wako. Basi, Mwenyezi Mungu Amekwisha fafanua kwamba mwaka wa arobaini huwadia ukiwa na baraka kwa watu wema. Na yule aliye na roho ya ukweli ndani yake, roho hiyo hulazimika kutikisika. Manabii wengi watukufu walipata unabii mnamo mwaka huo wa arobaini. Bwana wetu na Mwongozi wetu Hadhrat Muhammad Mteule[saw] naye alidhihirika katika mwaka wa arobaini wa umri wake kwa kuwarekebisha viumbe wa Mungu.**

## ROHO IMEUMBWA

Ni kweli kabisa nilivyosema hapo nyuma kwamba roho ni nuru nyepesi inayozalika mumo humu ndani ya mwili, nayo inakulia katika tumbo la uzazi. Kuzalika muradi wake hapa ni kwamba kwanza inafichikana humo bila kuhisika na kisha hudhihirika, lakini tangu mwanzo asili yake inakuwemo katika tone la shahawa. Hakuna shaka kwamba sawa na matakwa ya Mungu wa mbinguni na kwa idhini Yake, roho ina uhusiano usioeleweka na shahawa, nayo ni kiini king'aacho cha manii. Hatuwezi kusema hicho ni sehemu ya shahawa jinsi kiungo kimojawapo cha mwili kilivyo sehemu ya mwili; lakini pia hatuwezi kusema kwamba hicho chaingia kutoka nje au kikianguka juu ya ardhi kinachanganyikana na shahawa; bali hufichikana katika shahawa jinsi moto ufichikanavyo katika jiwe gumu la aina ya chakmaki (flint). Kitabu cha Mungu hakimaanishi kwamba roho

hushuka kutoka mbinguni au huanguka ardhini kutoka angani na kisha kwa bahati huchanganyika na shahawa na kuingia katika tumbo la uzazi. Wazo kama hilo haliko sawa kwa vyovyote, kwani sheria ya asili ya ulimwengu inalibatilisha. Kila siku tunashuhudia kwamba katika chakula kilichooza na katika majeraha machafu vidudu huzalika; katika mavazi machafu chawa huzalika, tumboni mwa mtu pia minyoo hupatikana. Je, twaweza kusema kwamba vidudu hivyo huingia kutoka nje au huonekana vikishuka kutoka mbinguni? Ukweli ni kwamba roho hutokana na mwili wenyewe — jambo linalohakikisha kwamba roho ni kitu kilichoumbwa.

## ROHO KUZALIWA MARA YA PILI

Nakusudia sasa kueleza kwamba Mwenyezi Mungu Mwenye uwezo wote Aliyeitoa roho kutoka katika mwili kwa uwezo Wake kamili, yaonekana, Amekusudia kuiumba mara ya pili pia kutokana na mwili. Harakati za roho hutegemea harakati za mwili. Upande wowote tunakopeleka mwili, upande huo huo na roho pia huufuata. Kwa hivyo, kuzitia maanani hali za maumbile ndiyo kazi ya kitabu sahihi cha Mwenyezi Mungu. Na ndiyo maana Kurani Tukufu imetoa mafunzo kwa kuzirekebisha hali za tabia ya asili ya binadamu, na imetoa maagizo yote kuhusu vitendo vya binadamu kama vile kucheka na kulia, kula na kunywa, kuvaa, kulala, kusema na kunyamaza, kuoa na kukaa kapera, kutembea na

kutulia, kutimiza masharti ya usafi wa kidhahiri yaani kuoga na kadhalika, na kuzingatia mambo fulani katika hali ya maradhi na afya; na imeeleza kuwa hali za kiwiliwili za binadamu zinaziathiri hali zake za kiroho. Kama maagizo yote hayo yakiandikwa kwa kirefu, sidhani nafasi ya kutosha itaweza kupatikana kuisoma makala hii nzima katika kikao hiki.

## MAENDELEO YA BINADAMU KWA TARATIBU

Ninapotafakari juu ya Neno Tukufu la Mwenyezi Mungu na jinsi Mungu Alivyompatia mtu sheria za kusawazisha na kurekebisha hali zake za ki-maumbile na kumnyanyua pole pole kwa shabaha ya kumfikisha kwenye daraja la juu la kiroho, hapo naona kanuni moja iliyojaa hekima. Nayo ni kwamba kwanza Mungu Alitaka kumfundisha binadamu njia za kuketi na kuinuka, kula na kunywa, kuongea na mambo mengine ya maisha, na kwa njia hii kumwokoa katika hali ya Unyama na kumtenga mbali na wanyama kwa shabaha ya kumfunza adabu. Hilo ni daraja la chini sana la khulka. Kisha Akataka kuzisawazisha tabia za asili za mtu zinazoweza kuitwa khulka duni hadi baada ya kurekebika zingine na kuwa khulka njema. Lakini hatua hizo mbili kwa hakika ni kitu kimoja tu kwani chahusikana na kurekebisha hali za maumbile; ipo tofauti ya daraja tu la chini na la juu. Mungu Mwenye hekima tupu Ameeleza mfumo wa khulka kwa njia hiyo ili mtu aweze kupata maendeleo kutoka khulka za chini hadi kwenye khulka za juu.

Kisha kuna hatua ya tatu; nayo ni kwamba mtu azame katika upendo na radhi ya Mwumba wake wa kweli, na dhati yake mtu huyo iwe kwa ajili ya Mungu peke Yake. Hilo ndilo daraja ambalo kwa kulikumbusha hilo Mungu Ameiita dini ya Waislamu kwa jina Islam. Kwani Islam maana yake ni kuwa wa Mungu kikamilifu bila kubakiza sehemu yoyote, kama Mungu Subhanahu wa Ta'ala Anenavyo:

بَلَىٰ مَنْ أَسْلَمَ وَجْهَهُ لِلَّهِ وَهُوَ مُحْسِنٌ فَلَهُ أَجْرُهُ
عِنْدَ رَبِّهِ وَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿١١٢﴾ [1]

قُلْ إِنَّ صَلَاتِي وَنُسُكِي وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٦٣﴾
لَا شَرِيكَ لَهُ ۖ وَبِذَٰلِكَ أُمِرْتُ وَأَنَا أَوَّلُ الْمُسْلِمِينَ ﴿١٦٤﴾ [2]

وَأَنَّ هَٰذَا صِرَاطِي مُسْتَقِيمًا فَاتَّبِعُوهُ ۖ وَلَا
تَتَّبِعُوا السُّبُلَ فَتَفَرَّقَ بِكُمْ عَنْ سَبِيلِهِ ۚ [3]

قُلْ إِنْ كُنْتُمْ تُحِبُّونَ اللَّهَ فَاتَّبِعُونِي يُحْبِبْكُمُ
اللَّهُ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ ۗ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٣١﴾ [4]

Yaani aliyeokoka ni yule anayetoa dhati yake kwa Mungu ili kuwa dhabihu katika njia Yake. Aonyeshe ukweli wake si kwa nia tu bali pia kwa matendo mema. Afanyaye hivyo amekwisha wekewa malipo

[1] Al-Baqarah, 2:113
[2] Al-An'aam, 6:163-164
[3] Al-An'aam, 6:154
[4] Aali'Imraan, 3:32

yake kwa Mungu; watu wa aina hii hawatakuwa na hofu wala hawatahuzunika. Sema, sala yangu na dhabihu yangu, kuishi kwangu na kufa kwangu ni kwa ajili ya Yule Mungu Ambaye ulezi Wake umevienea vitu vyote. Hakuna kitu chochote wala mtu yeyote aliye mshirika wake; kiumbe hakina ushirika naye kwa namna yoyote. Nimeagizwa kufanya hivyo. Mimi ndimi wa kwanza kuimarika katika mradi huo wa Kiislamu, yaani mwenye kutoa dhati kuwa dhabihu katika njia ya Mungu. Basi, njooni mkafuate njia yangu wala msijichagulie njia iliyo kinyume chake, kwani mtatengana na Mungu. Waambie, nifuateni mimi na kanyageni njia yangu ili Mungu Naye Awapendeni na kuwasamehe dhambi zenu, kwani Yu Msamehevu sana, Mrehemevu.

## KIPAMBANUZI BAINA YA HALI ZA KITABIA NA ZA KIKHULKA NA KUBATILISHA IMANI YA KUAFUA UZIMA

Sasa nitaeleza hatua hizo tatu za mtu. Lakini kwanza ningependa kukumbusha kwamba hali za tabia ya asili ya mtu ambazo chanzo chake ndiyo Nafsi Ammarah (Nafsi iamrishayo sana kutenda maovu) si mbali na hali za kikhulka sawa na madokezo ya maneno matukufu ya Mwenyezi Mungu. Kwani maneno matukufu ya Mungu yameeleza vipawa vya mtu, taama zake na mahitaji yake chini ya hali za tabia yake ya asili, na hizo hali za tabia ya asili ndizo

zinazokuwa Khulka zikitumika baada ya kusawazishwa sawa na akili na busara katika mahali pafaapo. Kadhalika hali za khulka haziko mbali na hali za kiroho; bali hali hizo hizo za kikhulka zinageuka kuwa hali za kiroho zikitumika kwa kujipoteza ndani ya Mungu na kutakasa nafsi na kuungana na Mungu kwa kujitenga mbali na vitu vyote na kuafikiana na Allah kwa upendo wote na kwa kuzama kikamilifu katika dhati Yake kwa makini na utulivu wote. Hali za tabia ya asili hazimtukuzi mtu mpaka zigeuke na kuwa hali za kikhulka, kwani hizo zapatikana hata katika wanyama bali na vitu vingine pia. Kadhalika khulka njema peke yake hazimpatii mtu uzima wa kiroho, bali mtu aweza kudhihirisha khulka njema hata akiwa anamkana Mungu kuwepo Kwake. Kuwa mpole wa moyo au mpenda suluhu au kuachana na shari na kutokushindana na mwenye shari ndizo hali za tabia ya asili ambazo aweza kujipatia hata yule asiyestahili ambaye hana habari ya chemchemi ya wokovu kabisa. Maana, kuna wanyama wengi ambao huwa wapole na wakizoeshwa huonyesha suluhu wala hawamshambulii mtu hata wakipigwa vikali kwa bakora, lakini hata hivyo hawawezi kuitwa binadamu, achilia mbali binadamu wa daraja la juu, kwa sababu ya kuonyesha tabia hizo. Halikadhalika mwenye imani mbovu kabisa, bali mtu mwovu pia anaweza kuwa na sifa hizo. Yawezekana mtu kuwa na huruma nyingi mno kiasi hiki kwamba hahalalishi kuwaua

wale vidudu wanaozalika katika jeraha na anawahami wenye uhai kiasi hiki kwamba hataki kabisa kuwaudhi wale chawa wanaopatikana katika nywele za kichwani au wadudu wanaozalika katika tumbo lake, katika matumbo yake na katika ubongo. Bali nakubali kwamba huruma ya mtu yaweza kufikia kiasi hiki hata kwamba mtu huyo anaacha kula asali kwani yapatikana kwa kuangamiza viumbe wengi na kuwafukuzilia mbali nyuki wengi kutoka kwenye masega yao. Naamini mtu anaweza kukataa kutumia hata miski kwani hiyo ni damu ya kulungu maskini ambayo hupatikana kwa kumwua na kumtenganisha na watoto wake. Halikadhalika sikatai mtu kujiepusha na kutumia lulu na kuvaa hariri kwani hizo hupatikana kwa kuwaua wadudu fulani wanyonge. Naam, nakubali kwamba mtu aweza kukataa kufyonzwa damu na maruba na kuvumilia udhia kuliko kumwua ruba. Na mwishowe nakiri kwamba mtu aweza kujiua kwa kukataa kunywa maji kabisa kwa kuwalinda wale vijidudu wanaokuwemo katika maji daima. Naweza kukubali hayo yote, lakini siwezi kukubali katu kwamba hizo hali za tabia ya asili zinaweza kuhesabiwa kuwa ni khulka au kwamba hizo peke yake zaweza kutakasa ule uchafu umzuiao mtu asipate nafasi ya kuungana na Mungu mwenye Enzi. Sitakubali kabisa kwamba kutokuwa na udhia kwa njia hiyo ambako hata baadhi ya wanyama na ndege pia humzidi mtu kwaweza kumpatia mtu ubinadamu (utu) wa hali ya juu. Bali katika fikara

yangu, huko ndiko kushindana na sheria iliyowekwa ulimwenguni na kupingana na khulka njema sana ya kuridhika na kukataa neema Aliyotupatia Mungu. Bali hali ya kiroho huipata mtu kwa kutumia kila khulka katika mahali pafaapo na kisha kukanyaga katika njia za Mungu kwa uaminifu na kuwa wake Yeye peke Yake. Na alama ya mtu kuwa wa Mungu ni kwamba yeye hawezi kuishi bila kuwa na Yeye. Aliyeungana na Mungu ni kama samaki aliyechinjwa kwa mkono wa Mungu na mapenzi ya Mungu ndiyo maji yake.

## NJIA TATU ZA KUREKEBISHA:

### MTUME[saw] KUTUMWA KWA SABABU YA KUWAKO KWA HAJA KALI YA KUREKEBISHA

Kama nilivyokwisha taja hapo nyuma, ziko chemchemi tatu za hali za binadamu, yaani Nafsi iamuruyo sana maovu, Nafsi inayojilaumu sana juu ya maovu na Nafsi iliyotulia. Basi na njia za kurekebisha nazo ni tatu.

Kwanza, washenzi wasio na adabu waimarishwe katika khulka njema za hali ya chini. Yaani, wafuate njia za kibinadamu katika mambo kama ya kula, kunywa, na mengine ya kistaarabu kama vile kuoa na kadhalika: wasitembee uchi wala wasile nyamafu kama mbwa na pia wasionyeshe adabu yoyote mbovu. Hilo ni daraja la kwanza katika kurekebisha hali za tabia ya kiasili. Mathalan, majangili wa Port Blair

wakitakiwa kufundishwa adabu, kwanza watapaswa kufundishwa khulka ndogo ndogo za mwanzo.

Njia ya pili ya kurekebisha ni kwamba mtu akiisha imarika katika adabu za dhahiri hizo ndogo ndogo za mwanzo ndipo afundishwe khulka kubwa za kibinadamu na afunzwe kutumia vipawa vyake vyote vile katika mahali panapofaa.

Njia ya tatu ya kurekebisha ni kuwaonjesha ladha ya kuungana na Mungu wale waliokwisha imarika sana katika khulka njema. Basi ziko njia hizo tatu za kurekebisha zilizotajwa ndani ya Kurani Tukufu.

Na Seyidna wa Maulana Nabii wetu[saw] alitumwa wakati ambapo dunia ilikuwa imeharibika kwa kila jiha na kuangamia jinsi asemavyo Mwenyezi Mungu:

ظَهَرَ الْفَسَادُ فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ [1]

Yaani, bara na bahari zilichafuka. Ndani yake imedokezwa kwamba waliopata Kitabu cha Mungu zamani na wale ambao hawakukipata, wote waliharibika. Hivyo basi, shabaha ya Kurani Tukufu kwa kweli ilikuwa ni kuhuisha wafu kama Asemavyo:

اِعْلَمُوْٓا اَنَّ اللّٰهَ يُحْيِ الْاَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا ط [2]

---

[1] Ar-Ruum, 30:42

[2] Al-Hadiid, 57:18

Yaani, jueni kwamba Mwenyezi Mungu sasa atahuisha ardhi upya baada ya kufa kwake. Katika zama hizo Waarabu walikuwa washenzi wa hali ya juu sana. Haikubaki kati yao nidhamu yoyote ya kibinadamu. Waliona fahari juu ya maovu yao. Mtu mmoja aliweza kuoa wake mia kadha. Kula haramu waliona ni sawa hasa. Walihalalisha kuoa mama zao, ndiyo sababu Mungu akalazimika kuagiza:

حُرِّمَتْ عَلَيْكُمْ أُمَّهَٰتُكُمْ [1]

Yaani, leo mmeharimishiwa kuoa mama zenu. Kadhalika walikuwa wanakula nyamafu; pia wengine walikuwa walaji wa nyama ya binadamu. Hapakuwa dhambi yoyote duniani ambayo hawakuitenda. Wengi walikana maisha ya akhera, bali wengi kati yao hawakuamini kuwepo kwa Mungu. Walikuwa wakiwaua binti zao kwa mikono yao. Walikula mali ya mayatima kwa kuwaua. Walikuwa na sura za kibinadamu lakini pasipo akili katika bongo zao. Hawakuwa na haya wala ghera kabisa. Walitumia ulevi kama maji. Mzinzi mkubwa zaidi alihesabiwa kuwa kiongozi wao. Elimu ilikosekana kati yao kiasi hiki kwamba mataifa yaliyo jirani yao yaliwapa jina Ummi, yaani wasio na elimu. Katika wakati kama huo Mtume wetu[saw] alitumwa kwa kuwarekebisha watu wa aina hiyo. Zama za aina za marekebisho

[1] An-Nisaa, 4:24

tulizotaja hapo nyuma zilikuwa hizo kikwelikweli. Ndiyo maana Kurani Tukufu imedai kuwa kamili kuliko sheria zote zingine, kwani vitabu vingine vya dini havikuwahi kupata nafasi ya kufanya marekebisho yote ya aina hizo tatu lakini Kurani ilipata nafasi hiyo. Na shabaha ya Kurani Tukufu ilikuwa kuwafanya washenzi wakatili kuwa binadamu sawasawa na kisha kuwafanya watu hao waungane na Mungu. Ndiyo sababu mambo hayo matatu yamo katika Kurani Tukufu.

## SHABAHA HASA YA KURANI TUKUFU NI MAREKEBISHO MATATU

### HALI ZA TABIA YA KIASILI ZIKISAWAZISHWA ZINAKUWA KHULKA

Kabla sijaanza kueleza namna tatu za marekebisho kwa kirefu sina budi kusema kwamba hakuna mafunzo yoyote ya Kurani Tukufu unayolazimishwa kwa nguvu kuyakubali, bali shabaha ya Kurani nzima ndiyo kuleta hayo marekebisho ya aina tatu, na kiini cha mafundisho yake ni hayo hayo marekebisho matatu. Maamrisho mengineyo ni njia tu za kuleta hayo marekebisho. Jinsi Daktari pia wakati fulani anavyopasua na pengine hutia marahamu kwa kuponya, ndivyo Kurani Tukufu inavyotumia maamrisho mbalimbali katika mahali pafaapo kwa ajili ya kumhurumia binadamu. Lakini maarifa yote hayo na mawaidha na wasia ni njia tu za kusawazisha

hali za tabia ya asili ya mtu zilizo za kinyama na kuzifanya kuwa hali za khulka na kisha kuzifikisha hali hizo za kikhulka hadi kwenye mto mkubwa wa kiroho usio na ufuko.

Nimekwisha eleza mapema kwamba hali za tabia ya asili ya mtu na hali za khulka si vitu viwili tofauti, bali hali za tabia ya asili zikisawazishwa na kutumiwa sawa na akili na busara katika mahali panapofaa zinakuwa hali za kikhulka; na kabla ya kusawazishwa chini ya utawala wa akili haziitwi khulka hata zifanane namna gani na khulka, bali ni mkondo tu wa tabia ya asili usiojiweza. Kwa mfano kama mbwa au mbuzi akionyesha upendo na unyenyekevu kwa bwana wake, huwezi kumwita mbwa huyo kuwa mwenye khulka njema au mbuzi huyo kuwa na adabu nzuri. Kadhalika hatuwezi kumwita mbwa mwitu au simba kuwa na khulka mbovu kwa sababu tu ya umbuai wao. Bali kama ilivyotajwa hapo juu, hali ya kikhulka huanzia pale tu itumikapo akili na busara katika wakati na mahali pa kufaa. Vile vile yule mtu asiyetumia akili na maarifa hufanana na watoto wachanga ambao bado hawajaanza kutumia akili zao, au hufanana na wenye wazimu waliopotewa na akili na fahamu. Ni dhahiri kwamba wakati mwingine mtoto mchanga au mtu mwenye wazimu anabahatika kutenda mambo fulani yafananayo na khulka, lakini mtu yeyote mwenye busara hatayahesabu kuwa khulka kwani hayakutendwa kwa kukusudia kwa

kutumia akili na busara bali yametendeka tu kikawaida kwa sababu ya ki-maumbile. Kwa mfano, mtoto anaelekea kwenye matiti ya mama mara baada ya kuzaliwa, na kifaranga baada ya kuzalika hukimbilia kudona punje; mwana ruba atakuwa na tabia za ruba na mwana nyoka ataonyesha tabia za nyoka na mwana simba atadhihirisha tabia za simba. Hususan mtoto wa binadamu apaswa kuchunguzwa kwa makini jinsi anavyoanza kuonyesha tabia za kibinadamu tangu kuzaliwa. Kisha anapokuwa na umri wa mwaka mmoja na nusu tabia zake zinaonekana kwa uwazi zaidi. Mathalan, sasa analia kwa sauti kubwa zaidi kuliko hapo mwanzoni na pia tabasamu zake zaelekea kuwa kicheko na vile vile macho yake yanaonekana yanaangalia huko na huko kwa kusudi. Katika umri huo jambo lingine la kitabia huzalika ya kwamba anadhihirisha kwa vitendo radhi yake au kutokuridhia kwake. Anapenda kumpiga fulani au kumpa mwingine kitu fulani. Lakini vitendo hivyo vyote huwa vya ki-maumbile. Basi mtu asiyestaarabika ni kama mtoto huyo mchanga aliyepata kipambanuzi haba sana cha utu, huyo naye huonyesha harakati za umbile tu katika kauli na amali zake na kutikisika na kutulia kwake. Yeye huwa chini ya utawala wa maono ya umbile lake. Hatendi lolote kwa kutafakari na kutumia akili na busara yake bali lolote lililomo ndani yake ki-maumbile hutoka nje kwa kuchochewa na harakati fulani za ki-nje. Yawezekana maono yake ya tabia yake ya asili

yanayodhihirika kwa sababu kadha yasiwe yote mabaya bali mengine yanaweza kufanana na khulka njema, lakini hayakudhihirishwa baada ya kutafakari na kutumia maarifa, akili na busara. Hata kama akili kidogo imetumika pia, hata hivyo maono hayo hayatahesabiwa kuwa khulka kwa sababu ya maneno ya ki-maumbile kuwa mengi na kushinda.

## KHULKA HASA

Ilmuradi, hatuwezi kunasibisha khulka hasa kwa yule mtu aliyetawaliwa na hali yake ya ki-maumbile kama watoto na wendawazimu, ambaye anaishi kama majangili. Bali zama za khulka njema au mbovu huanzia wakati akili aliyojaaliwa binadamu na Mungu hupevuka na kuweza kupambanua khulka njema na khulka' mbovu, na mtu anajuta kwa kuachana na njia nzuri na kusikitika na kuhuzunika kwa kutenda maovu. Na hizi ndizo zama za pili za mtu zilizoitwa Nafsi Inayojilaumu katika Kurani Tukufu iliyo Neno Takatifu la Mungu. Lakini itambulikane kwamba mawaidha ya juu juu tu hayatoshi kumfikisha mtu katili kwenye hali ya Nafsi Lawwaamah (Nafsi ijilaumuyo); bali hakuna budi ajipatie kumtambua Mungu kiasi fulani hata kwamba asione kuumbwa kwake kuwa upuuzi, ili khulka za kweli zizalike ndani yake kwa kumwelewa Mungu. Ndiyo sababu Mwenyezi Mungu kila mara amesisitiza kumtambua Mungu wa kweli na ameyakinisha kwamba kila kitendo na khulka huleta matokeo fulani

yanayosababisha raha ya kiroho au adhabu ya kiroho katika uhai wake na yataonyesha athari yake wazi wazi katika maisha ya akhera. Kwa kifupi, katika daraja la Nafsi Ijilaumuyo, mtu hupata sehemu ya akili, maarifa na dhamiri hata kwamba anajilaumu akitenda mabaya na anapenda kufanya mema. Hilo ndilo daraja ambamo mtu hujipatia khulka bora.

## KHALQ NA KHULQ

Hapa ningependa kufafanua neno Khulq (khulka). Jueni kwamba neno Khalq (kwa fat'ha yaani 'a') maana yake ni uumbaji wa kiwiliwili, na Khulq (kwa dhamma yaani 'u') lamaanisha uumbaji wa kiroho. Na kwa kuwa uumbaji wa kiroho hukamilika kwa sababu ya khulka, wala si maono ya umbile peke yake, hivyo neno Khulq latumika kwa khulka tu, si kwa maono ya ki-maumbile. Pia inapaswa kueleza kwamba watu wa kawaida hudhani kwamba upole na unyenyekevu peke yake ndiyo khulka; hilo ni kosa. Bali kulingana na viungo vya kiwiliwili kuna hali mbalimbali za sifa za kibinadamu katika undani wake. Hali hizo ndizo zaitwa khulka. Mathalan, mtu hulia kwa macho, lakini kulingana na kitendo hicho kuna hali ya huzuni na unyenyekevu katika moyo. Hali hii ikitumika sawa na akili katika mahali pafaapo ndiyo huitwa khulka. Kadhalika mtu hukabiliana na adui yake kwa mkono na kwa kulingana na kitendo hicho kuna nguvu katika moyo wa mtu ambayo nguvu hiyo huitwa ushujaa. Basi mtu atumiapo nguvu hii katika mahali

panapofaa, nguvu hiyo itaitwa khulka. Vile vile mtu wakati mwingine anawaokoa wadhulumiwao katika dhuluma ya wadhalimu, au anapenda kuwasaidia wenye hali ndogo au wenye njaa, au kuwahudumia wanadamu kwa njia nyingine yoyote iwayo, basi kulingana na hali hiyo ipo nguvu fulani moyoni mwa mtu ambayo huitwa huruma. Na pengine humwadhibu mdhalimu kwa mikono yake, basi kuna nguvu fulani katika moyo iitwayo kujilipiza kisasi. Na wakati mwingine mtu akishambuliwa anaamua kutokumshambulia adui yake na anamsamehe mdhalimu, basi kulingana na harakati hii ipo nguvu pia katika moyo ambayo huitwa msamaha na subira. Na tena wakati mwingine mtu hupenda kuwanufaisha wengine kwa mikono au miguu yake au kwa moyo au fahamu yake na hutoa mali yake kwa kuinua hali ya watu, basi kulingana na tendo hili kuna nguvu katika moyo iitwayo ukarimu. Hivyo basi, mtu atumiapo nguvu hizo zote sawa na akili katika mahali panapofaa, nguvu hizo zaitwa khulka. Mwenyezi Mungu akimwambia Mtume[saw] Amesema:

إِنَّكَ لَعَلَىٰ خُلُقٍ عَظِيمٍ ۝ [1]

Yaani, wewe unayo khulka njema, tukufu. Na sawa na maelezo hapo juu kauli hii ya Mungu inamaanisha kwamba namna zote za khulka kama vile ukarimu,

---

[1] Al-Qalam, 68:5

ushujaa, uadilifu, huruma, hisani, ukweli, kuwa na moyo mkunjufu, zote hizo zinapatikana ndani yako. Ilmuradi, nguvu zote zilizomo katika moyo wa mtu kama vile adabu, kuona haya, uaminifu, umurua, ghera, uimara, unyofu, utawa, usawa, huruma na kadhalika ushujaa, ukarimu, usamehevu, subira, hisani, ukweli, uaminifu na nyinginezo zilizo hali za tabia ya asili ya mtu zikitumiwa sawa na akili na busara katika mahali mbalimbali panapofaa huitwa khulka. Na khulka hizo kwa hakika ndizo hali za ki-maumbile tu, nazo zaitwa khulka pale tu zitumiwapo kwa kuafikiana na wakati na mahali sawa na akili ya mtu. Na kwa kuwa sifa mojawapo ya binadamu ni kwamba yu kiumbe awezaye kupata maendeleo, hivyo basi, kwa kufuata dini ya kweli na kukaa na watu wema na kwa njia ya mafunzo mema, yeye anayageuza maono ya ki-maumbile kuwa khulka — jambo ambalo haliko katika uwezo wa viumbe wengine.

REKEBISHO LA KWANZA

YAANI HALI ZA TABIA YA ASILI

Sasa kati ya namna tatu za marekebisho za Kurani Tukufu naeleza namna ya kwanza ihusikanayo na daraja la chini sana la hali za ki-maumbile. Hii ndiyo sehemu mojawapo ya khulka inayoitwa adabu. Na hizo ndizo adabu zinazowaleta washenzi na katili kwenye hali ya wastani katika mambo ya maisha yaliyo hali za tabia ya asili kama vile kula,kunywa,

kuoa na kadhalika, na zinaokoa katika maisha ya kishenzi, ya kinyama na ya kikatili. Mwenyezi Mungu anasema ndani ya Kurani Tukufu kuhusu adabu hizo zote katika aya zifuatazo:

حُرِّمَتْ عَلَيْكُمْ أُمَّهَاتُكُمْ وَبَنَاتُكُمْ وَأَخَوَاتُكُمْ وَعَمَّاتُكُمْ وَخَالَاتُكُمْ وَبَنَاتُ
الْأَخِ وَبَنَاتُ الْأُخْتِ وَأُمَّهَاتُكُمُ اللَّاتِي أَرْضَعْنَكُمْ وَأَخَوَاتُكُمْ مِنَ الرَّضَاعَةِ
وَأُمَّهَاتُ نِسَائِكُمْ وَرَبَائِبُكُمُ اللَّاتِي فِي حُجُورِكُمْ مِنْ نِسَائِكُمُ اللَّاتِي دَخَلْتُمْ
بِهِنَّ فَإِنْ لَمْ تَكُونُوا دَخَلْتُمْ بِهِنَّ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ وَحَلَائِلُ أَبْنَائِكُمُ
الَّذِينَ مِنْ أَصْلَابِكُمْ وَأَنْ تَجْمَعُوا بَيْنَ الْأُخْتَيْنِ إِلَّا مَا قَدْ سَلَفَ [1]

لَا يَحِلُّ لَكُمْ أَنْ تَرِثُوا النِّسَاءَ كَرْهًا [2]

وَلَا تَنْكِحُوا مَا نَكَحَ آبَاؤُكُمْ مِنَ النِّسَاءِ إِلَّا مَا قَدْ سَلَفَ [3]

أُحِلَّ لَكُمُ الطَّيِّبَاتُ ... وَالْمُحْصَنَاتُ مِنَ الْمُؤْمِنَاتِ وَالْمُحْصَنَاتُ مِنَ الَّذِينَ أُوتُوا
الْكِتَابَ مِنْ قَبْلِكُمْ إِذَا آتَيْتُمُوهُنَّ أُجُورَهُنَّ مُحْصِنِينَ غَيْرَ مُسَافِحِينَ
وَلَا مُتَّخِذِي أَخْدَانٍ [4]

وَلَا تَقْتُلُوا أَنْفُسَكُمْ [5]

[1] An-Nisaa, 4:24
[2] An-Nisaa, 4:20
[3] An-Nisaa, 4:23
[4] Al-Maaidah, 5:6
[5] An-Nisaa, 4:30

وَلَا تَقْتُلُوٓا اَوْلَادَكُمْ [1]

لَا تَدْخُلُوْا بُيُوْتًا غَيْرَ بُيُوْتِكُمْ حَتّٰى تَسْتَاْنِسُوْا وَتُسَلِّمُوْا عَلٰٓى اَهْلِهَا ۗ.. [2]

فَاِنْ لَّمْ تَجِدُوْا فِيْهَآ اَحَدًا فَلَا تَدْخُلُوْهَا حَتّٰى يُؤْذَنَ لَكُمْ ۚ وَاِنْ قِيْلَ لَكُمُ
ارْجِعُوْا فَارْجِعُوْا هُوَ اَزْكٰى لَكُمْ ۗ [3]

وَاْتُوا الْبُيُوْتَ مِنْ اَبْوَابِهَا ۖ [4]

وَاِذَا حُيِّيْتُمْ بِتَحِيَّةٍ فَحَيُّوْا بِاَحْسَنَ مِنْهَآ اَوْ رُدُّوْهَا ۗ [5]

اِنَّمَا الْخَمْرُ وَالْمَيْسِرُ وَالْاَنْصَابُ وَالْاَزْلَامُ رِجْسٌ مِّنْ عَمَلِ الشَّيْطٰنِ
فَاجْتَنِبُوْهُ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُوْنَ ﴿٩١﴾ [6]

حُرِّمَتْ عَلَيْكُمُ الْمَيْتَةُ وَالدَّمُ وَلَحْمُ الْخِنْزِيْرِ وَمَآ اُهِلَّ لِغَيْرِ اللّٰهِ بِهٖ
وَالْمُنْخَنِقَةُ وَالْمَوْقُوْذَةُ وَالْمُتَرَدِّيَةُ وَالنَّطِيْحَةُ وَمَآ اَكَلَ السَّبُعُ اِلَّا مَا ذَكَّيْتُمْ ۗ
وَمَا ذُبِحَ عَلَى النُّصُبِ [7]

يَسْـَٔلُوْنَكَ مَاذَآ اُحِلَّ لَهُمْ ۗ قُلْ اُحِلَّ لَكُمُ الطَّيِّبٰتُ ۙ [8]

اِذَا قِيْلَ لَكُمْ تَفَسَّحُوْا فِى الْمَجٰلِسِ فَافْسَحُوْا يَفْسَحِ اللّٰهُ لَكُمْ ۚ

---

1 Al-An‘aam, 6:152
2 An-Nuur, 24:28
3 An-Nuur, 24:29
4 Al-Baqarah, 2:190
5 An-Nisaa, 4:87
6 Al-Maaidah, 5:91
7 Al-Maaidah, 5:4
8 Al-Maaidah, 5:5

وَإِذَا قِيلَ انْشُزُوا فَانْشُزُوا [1]

كُلُوا وَاشْرَبُوا وَلَا تُسْرِفُوا [2]

وَقُولُوا قَوْلًا سَدِيدًا ۝٧١ [3]

وَثِيَابَكَ فَطَهِّرْ ۝٥ وَالرُّجْزَ فَاهْجُرْ ۝٦ [4]

وَاقْصِدْ فِي مَشْيِكَ وَاغْضُضْ مِنْ صَوْتِكَ [5]

تَزَوَّدُوا فَإِنَّ خَيْرَ الزَّادِ التَّقْوَىٰ [6]

وَإِنْ كُنْتُمْ جُنُبًا فَاطَّهَّرُوا [7]

وَفِي أَمْوَالِهِمْ حَقٌّ لِلسَّائِلِ وَالْمَحْرُومِ ۝٢٠ [8]

وَإِنْ خِفْتُمْ أَلَّا تُقْسِطُوا فِي الْيَتَامَىٰ فَانْكِحُوا مَا طَابَ لَكُمْ مِنَ النِّسَاءِ مَثْنَىٰ
وَثُلَاثَ وَرُبَاعَ ۖ فَإِنْ خِفْتُمْ أَلَّا تَعْدِلُوا فَوَاحِدَةً [9]

وَآتُوا النِّسَاءَ صَدُقَاتِهِنَّ نِحْلَةً [10]

Tafsiri:Mmeharimishiwa (kuoa) mama zenu, binti zenu, na dada zenu, na shangazi zenu, na dada za

---

[1] Al-Mujaadalah, 58:12
[2] Al-A‘raaf, 7:32
[3] Al-Ahzaab, 33:71
[4] Al-Muddaththir, 74:5-6
[5] Luqmaan, 31:20
[6] Al-Baqarah, 2:198
[7] Al-Maaidah, 5:7
[8] Adh-Dhaariyaat, 51:20
[9] An-Nisaa, 4:4
[10] An-Nisaa, 4:5

mama zenu, na binti za ndugu, na binti za dada, na mama zenu waliowanyonyesheni, na dada zenu wa kunyonya, na mama wa wake zenu, na binti zenu wa kambo walio katika ulinzi wenu, waliozaliwa na wake zenu mliowaingilia — lakini kama ninyi hamjawaingilia, basi si vibaya kwenu (kuwaoa) — na wake wa wana wenu waliotoka katika migongo yenu; na (imeharimishwa) ya kwamba muwaoe madada wawili wakati mmoja, isipokuwa yale yaliyokwisha pita.

Si halali kwenu kuwarithi wanawake kwa nguvu.

Wala msiwaoe wake waliowaoa baba zenu, isipokuwa yale yaliyokwisha pita.

Na wanawake wema katika wale waliopewa Kitabu kabla yenu (ni halali kwenu), mtakapowapa mahari zao, mkifunga nao ndoa, bila kufanya uzinzi wala msiwaweke mahawara wa siri.

Kulikuwa na desturi ya baadhi ya Waarabu wajinga kwamba mtu asipopata kizazi, mkewe alikuwa akienda kulala na mwanamume mwingine ili kupata mimba. Kurani Tukufu imeharimisha jambo hili. Desturi hiyo imetajwa ndani ya Kurani kwa kusema "mahawara wa siri."

Kisha Kurani imesema: wala msijiue. Msiwaue watoto wenu. Msiingie nyumba ambazo si nyumba zenu (kama washenzi) mpaka mwombe ruhusa, na muwatolee salamu waliomo humo.

Na kama hamtakuta humo yeyote, basi msiingie mpaka mmeruhusiwa. Na mkiambiwa, Rudini, basi rudini; hili ni takaso kwenu (24:29). Msiingie majumbani kwa kuruka kuta, bali fikeni majumbani kwa kupitia milangoni mwao. Na mnaposalimiwa kwa maamkio, basi itikeni kwa yaliyo bora kuliko hayo, au mrejeshe hayo hayo.

Bila shaka pombe na kamari na masanamu (ya kuabudu) na mishale (ya ramli) ni uchafu ulio kazi ya shetani. Basi jiepusheni nayo, ili mpate kufaulu.

Mmeharimishiwa nyamafu na damu na nyama ya nguruwe, na kilichosomewa jina lisilo la Mwenyezi Mungu, na kilichonyongwa, na kilichokufa kwa kupigwa, na kilichokufa kwa kuanguka na kilichokufa kwa kupigwa pembe, na alichokula mnyama mkali isipokuwa mlichochinja (kwa sheria) na pia mmeharimishiwa kilichochinjwa juu ya mawe ya sanamu.

Wanakuuliza wamehalalishiwa nini. Sema: mmehalalishiwa vitu vizuri (5:5). Msile nyamafu au kinachofanana na nyamafu na vitu vibaya.

Mnapoambiwa kuwafanyia wengine nafasi katika mikutano yenu, basi fanyeni nafasi. Na mkiambiwa kusimama, basi simameni bila kusita (58:12). Kuleni nyama pia na dengu vile vile na vyote vilivyo vizuri, lakini msisisitize kimojawapo peke yake, wala msipite

kiasi katika ulaji, bali kuleni kiasi tu. (7:32) Msizungumze ovyo, bali ongeeni sawa na hali. (33:71)

Vaeni nguo safi. Hifadhini mwili, nyumba, mtaa na kila mahali mnapoketi visichafuke. Shikeni tabia ya kuoga kila mara na zoeeni kuweka nyumba zenu katika hali ya usafi. (74:5-6)

Msitembee kwa kasi sana wala pole pole sana (isipokuwa kama ipo haja). Shikeni hali ya wastani, msizungumze kwa sauti ya juu sana wala ya chini kabisa. (31:20)

Ukienda safari, ufanye matayarisho yote mapema na chukua masurufu ya kutosha kujiepusha na kuomba-omba. (2:198) Mnapokuwa na janaba, ogeni. (5:7)

Mnapokula chakula, pia mpeni maskini na pia watupieni mbwa na ndege wengine. (51:20)

Hakuna ubaya kuwaoa mayatima wale mliowalea. Lakini mkihisi kwamba hamtawatendea vizuri kwa sababu hawana jamaa zao wa kulinda haki zao, hapo waoeni wanawake wale walio na wazazi na jamaa wengine watakaowachungeni na mtakaowaheshimu. Mwaweza kuoa mmoja, wawili, watatu hadi wanne sharti mwatendee kwa usawa bila kumpendelea yeyote kati yao. Msipoweza kufanya uadilifu, hapo mtosheke na mmoja tu hata kama mna haja ya zaidi. Kikomo cha wanne kimewekwa ili msizidi sana kwa sababu ya mazoea yenu ya zamani na kufikisha idadi

hadi mamia, au kwamba msielekee kwenye uzinzi. Pia wapeni wake zenu mahari. (4:4-5)

Kwa kifupi, hilo ndilo rekebisho la kwanza ambalo kwalo hali za tabia ya asili ya mtu zimeelekezwa kwenye adabu za kiutu kwa kufutilia mbali desturi za kishenzi. Katika mafunzo hayo bado hazijatajwa khulka bora za hali ya juu, bali hizo ni adabu za mwanzo za kibinadamu. Na nimekwisha sema hapo nyuma kwamba haja ya mafunzo hayo ilisikika kwa sababu watu aliowajia Mtume[saw] kuwarekebisha walikuwa wamewazidi wengine wote katika ushenzi; hawakuwa na ubinadamu kwa jiha yoyote. Kwa hivyo, ilibidi kuwafunza adabu za dhahiri za kibinadamu.

## KUHARIMISHA NGURUWE

Hapa kuna jambo moja la kielimu linalopaswa kuzingatiwa, nalo ni kwamba Mwenyezi Mungu tangu mwanzo Ameweka katika jina lenyewe la nguruwe kidokezo cha uharamu wake. Kwa Kiarabu nguruwe huitwa Khinzir, ambalo ni mchanganyiko wa maneno mawili: Khinz na Ara; na tafsiri yake ni: 'Namwona yu mchafu'. Khinz maana yake ni mchafu sana na Ara tafsiri yake ni 'ninaona'. Basi mnyama huyo amepewa jina tangu mwanzo linaloashiria kwenye ubaya wake. Ni la ajabu kuwa nguruwe huitwa Suu’ar kwa Kihindi ambalo neno hilo tena limeundwa kutokana na maneno mawili: Suu (mbaya) na Ara (naona), yaani 'namwona yu mbaya'.

Msishangae kuona neno la Kiarabu, Suu, limeingiaje katika Kihindi, kwani nimekwisha hakikisha katika kitabu changu Minan-ur-Rahman kwamba Kiarabu ni mama wa lugha zote; na maneno ya Kiarabu yameisha ingia katika lugha zote; si mawili au matatu bali maelfu kwa maelfu. Hivyo, Suu'ar ni neno la Kiarabu na ndiyo sababu tafsiri yake kwa Kihindi ni 'Mbaya', na kwa hivyo, nguruwe huitwa 'Mbaya'. Hamna shaka katika jambo hili kwamba wakati ambapo Kiarabu kilikuwa ni lugha ya dunia nzima, jina la mnyama huyu lilijulikana katika nchi hii kwa Kiarabu lililokuwa na tafsiri ya Khinzir, kisha likabaki kama kumbukumbu. Naam, pia yawezekana, neno hili kwa kubadilika-badilika likawa lingine; lakini neno sahihi ndilo hili tu kwani linajieleza lenyewe. Tena neno Khinzir lahakikisha zaidi habari hii. Na haina haja ya kufahamu ukweli wa maana hii ya 'uchafu' ndani ya mnyama mwenyewe huyo. Kwani kila mmoja anafahamu kwamba mnyama huyo ni mlaji sana wa uchafu na ni mpujufu wa hali ya juu sana. Kwa hiyo, sababu ya kuharimisha nyama yake ni dhahiri shahiri, kwani sheria ya ulimwengu yatuongoza kwamba athari ya nyama ya mnyama huyo mwovu haina budi kuwa mbaya kwa mwili na roho. Na tumeisha hakikisha hapo nyuma kwamba vyakula havina budi kuleta athari katika roho pia, kwa hiyo haina shaka kwamba athari ya 'mbaya' huyo itakuwa mbaya vile vile, jinsi Matabibu wa Kiyunani walivyowahi kueleza kabla haijaja Islam kwamba

nyama ya nguruwe kitabia hupunguza sifa ya kuona haya na huzidisha upujufu. Hali kadhalika nyamafu pia imekatazwa na sheria kwani hiyo hutia athari yake katika roho ya mlaji wake na pia huharibu afya ya mwili. Na wanyama wote waliokufa kwa kunyongwa au kwa kupigwa na bakora na kadhalika ambao damu zao zinabakia ndani ya miili yao nao huhesabiwa kuwa ni nyamafu. Je, damu ikibakia ndani ya mzoga yaweza kubaki katika hali yake ya kawaida? Hata! Bali kwa sababu ya kuwa na majimaji itaharibika haraka sana na kwa hiyo nyama yote itaoza. Isitoshe, vijidudu vya damu vilivyogunduliwa siku hizi kwa uchunguzi wa kisasa vikijifia humo katika damu vitaeneza harufu mbaya yenye sumu katika mwili mzima wa mzoga.

## HALI ZA KHULKA ZA MTU

Sehemu ya pili ya Kurani Tukufu ni kuzisawazisha hali za tabia ya asili kwa kuleta masharti yafaayo na kuzifanya ziwe khulka bora. Basi ifahamike kwamba sehemu hii ni kubwa sana. Nikitaka kuieleza kwa marefu na mapana, yaani nikikusudia kuzieleza khulka zote zilizoelezwa na Kurani Tukufu, makala hii itakuwa ndefu sana hata kwamba nafasi iliyowekwa kwa kuisoma hadharani haitatosha walau kusoma sehemu yake ya kumi tu. Kwa hivyo natoa mifano ya khulka chache tu.

Itambulikane sasa kwamba khulka ni za aina mbili: kwanza ni zile khulka zinazomwezesha mtu asitende ubaya. Pili, zile khulka zimwezeshazo kutenda wema. Katika kundi la kwanza zinaingia zile khulka ambazo kwazo mtu anajaribu asidhuru mali ya mwenzake, hesima yake au maisha yake, si kwa ulimi wake wala kwa mkono au jicho au kwa viungo vyake vingine na wala asikusudie kufanya hivyo. Na katika kundi la pili, zaingia khulka zote zile zimwezeshazo mtu kujaribu kwa ulimi wake au mkono wake au mali yake au ujuzi wake au kwa njia yoyote nyingine ili kunufaisha mwenzake katika mali yake au heshima yake au kukusudia kudhihirisha shani yake au heshima yake; au kama alidhulumiwa na mtu fulani, basi amsamehe mdhalimu huyo na kumwokoa katika udhia na adhabu ya kimwili au kutozwa faini ili muradi kumnufaisha kwa njia hii; au kumwadhibu kwa namna ambayo itakuwa ni rehema kwa ajili yake moja kwa moja.

## KHULKA KUHUSU KUEPUKANA NA UBAYA

Ibainike sasa kwamba zile khulka zilizowekwa na Mwumbaji wa kweli kwa kumwezesha mtu asitende maovu zinaitwa kwa majina manne katika lugha ya Kiarabu ambayo katika lugha hiyo kuna neno maalum kwa kila wazo la kibinadamu na kila hali yake na kila khulka yake.

Basi, khulka ya kwanza huitwa Ihswaan. Neno hili linamaanisha ule utwa unaohusikana na nyege. Muhswan au Muhswanah ni yule mwanaume au mwanamke ambaye kwa kujiepusha na chanzo cha uzinzi huepukana na zinaa ambayo matokeo yake kwa wote wawili ni dhila na laana katika dunia hii na adhabu huko akhera. Isitoshe, jamaa zao wa karibu nao hupata hasara kubwa ya kuaibika. Mathalan, kama kuna mtu ambaye amemzini mke wa mtu, au kama bado hajamzini lakini ametenda mambo ya kuelekea kwenye zinaa nao wakafumaniwa, hapo huyo mume mwenye ghera aliyedhulumiwa, ambaye mkewe alikuwa tayari kutenda uchafu huo au kama zinaa yenyewe imekwisha tendeka, atalazimika kumpa talaka; na kama yu mja mzito, basi na mtoto wa tumboni naye ataathirika vibaya; na hiyo yote ni hasara atakayolazimika huyo mume kuivumilia kwa sababu ya mwanamke huyo mwovu.

Kumbukeni hapa kwamba khulka hii iitwayo Ihswaan (utawa) itahusikana na yule ambaye anao uwezo wa kumtazama mwingine kwa tamaa au kwa kufanya uzinzi, yaani mtu amejaaliwa nguvu hiyo ya nyege na akiamua anaweza kuzini, lakini anajiepusha kabisa na ovu hili. Lakini yule asiye na nguvu ya nyege kwa sababu yungali mtoto au towashi au huntha au mzee mkongwe, hataitwa Muhswan (mtawa) kwa sababu hatendi uzinzi. Naam, sifa hii ipo ndani yake kama tabia yake ya asili, lakini

nimekwisha kariri mara nyingi kwamba hali za tabia ya asili haziitwi khulka mpaka ziletwe katika mahali pafaapo kwa kutumia akili na busara. Kwa hiyo, basi, watoto wadogo na wasiofaa kwa wanawake na wanaojihasi kwa njia fulani hawawezi kuitwa watawa ijapokuwa kidhahiri wataishi kwa utawa, kwani utawa wao kwa kweli ni hali ya ki-maumbile na wala si chochote kingine kiwacho. Na kwa kuwa ovu hili laweza kutendwa na mwanamke pia jinsi liwezavyo kufanywa na mwanamume, hivyo Kitabu Kitakatifu cha Mungu kinawaagiza wote hao wawili kwamba:

قُلْ لِّلْمُؤْمِنِيْنَ يَغُضُّوْا مِنْ اَبْصَارِهِمْ وَيَحْفَظُوْا فُرُوْجَهُمْ ۭ ذٰلِكَ اَزْكٰى لَهُمْ ۭ [1]
وَقُلْ لِّلْمُؤْمِنٰتِ يَغْضُضْنَ مِنْ اَبْصَارِهِنَّ وَيَحْفَظْنَ فُرُوْجَهُنَّ وَلَا يُبْدِيْنَ
زِيْنَتَهُنَّ اِلَّا مَا ظَهَرَ مِنْهَا وَلْيَضْرِبْنَ بِخُمُرِهِنَّ عَلٰي جُيُوْبِهِنَّ ... وَلَا
يَضْرِبْنَ بِاَرْجُلِهِنَّ لِيُعْلَمَ مَا يُخْفِيْنَ مِنْ زِيْنَتِهِنَّ ۭ وَتُوْبُوْٓا اِلَى اللّٰهِ جَمِيْعًا
اَيُّهَ الْمُؤْمِنُوْنَ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُوْنَ ۝٣١ [2]

وَلَا تَقْرَبُوا الزِّنٰٓى اِنَّهٗ كَانَ فَاحِشَةً ۭ وَسَاۗءَ سَبِيْلًا ۝٣٢ [3]

وَلْيَسْتَعْفِفِ الَّذِيْنَ لَا يَجِدُوْنَ نِكَاحًا [4]

وَرَهْبَانِيَّةَۨ ابْتَدَعُوْهَا مَا كَتَبْنٰهَا عَلَيْهِمْ اِلَّا ابْتِغَاۗءَ رِضْوَانِ اللّٰهِ

---

[1] An-Nuur, 24:31
[2] An-Nuur, 24:32
[3] Banii Israaiil, 17:33
[4] An-Nuur, 24:34

فَمَا رَعَوْهَا حَقَّ رِعَايَتِهَا ۖ [1]

Yaani, Waambie wanaume waaminio wayaepushe macho yao yasiwatazame wanawake wanaoweza kutamanisha (yaani walio halali kuolewa nao). Katika wakati kama huo shikeni tabia ya kuinamisha macho. Na zilindeni tupu zenu. Kadhalika yalindeni masikio yenu yasipate kusikia nyimbo za wanawake wageni na sauti zao nzuri wala msisikilize maelezo ya uzuri wa sura zao. Njia hii ndiyo nzuri sana kwa utakaso wa macho na moyo. Kadhalika waagize wanawake waaminio pia kwamba wajiepushe na kuwatazama wanaume wasio haramu na pia wayalinde masikio yao yasisikilize sauti zao zichocheazo nyege; na wateremshe shungi zao mpaka vifuani mwao; yaani kifua, masikio mawili, kichwa na mapaja vifunikwe (24:32). Wala wasipige miguu yao kama wacheza ngoma. Hii ndiyo njia inayoweza kumlinda mtu asiteleze (24:32).

Na njia ya pili ya kusalimika ni kuelekea kwa Mwenyezi Mungu na kumwomba dua Yeye alinde isipatikane hali ya kuteleza. Wala msikurubie zinaa; yaani mjiweke mbali na mambo yanayoweza kuleta wazo hilo wala msishike njia zinazowezesha uovu huo kutendeka. Aziniye hutenda uovu wa mwisho kabisa. Njia ya uzinifu ni mbaya mno; huzuia msipate

---

[1] Al-Hadiid, 57:28

shabaha; ni kitu cha hatari sana kwa lengo lenu la mwisho. Na yule asiye na nafasi ya kuoa, ahifadhi utawa wake kwa njia nyingine kama vile kufunga saumu au kula kidogo au kujishughulisha katika kazi ngumu za mikono. Watu wengine wamezusha njia nyingine ya kupata utawa kwa kujizuia wasioe kusudi maisha mazima au kwa kujihasi na kuishi makapera; lakini sisi hatukuwaamrisha hivyo, ndiyo maana hawakuweza kutekeleza bidaa zao hizo. Mungu Anaposema kwamba Yeye hakuamrisha kujihasi, anaashiria kwamba kama hiyo ingalikuwa amri Yake, watu wote wangelazimika kuitekeleza na hapo kizazi cha binadamu kingemalizika na dunia ingekwisha kabisa. Kama mtu akitaka kupata utawa kwa kukatilia mbali dhakari yake, hapo yeye anampinga Mungu Aliyeumba sehemu hii. Isitoshe, kwa kuwa thawabu hupatikana iwapo nguvu fulani ipo lakini kwa kumwogopa Mungu, mtu ashindane na nafsi yake wala asitumie vibaya nguvu hiyo, bali afaidike nayo kwa kuitumia kwa njia ifaayo. Hivyo, ni dhahiri kwamba mtu anayepoteza sehemu hiyo ya mwili hujinyima kupata thawabu mbili. Thawabu hupatikana kama mtu anayo jazba fulani isiyofaa na kisha anashindana nayo. Lakini yule ambaye hanayo ile jazba kama alivyo mtoto mdogo, atapata thawabu gani? Je, mtoto aweza kustahili kupewa thawabu kwa sababu eti yu mtawa?

## TIBA TANO ZA KUHIFADHI UTAWA

Katika aya hizo Mwenyezi Mungu Hakutoa mafunzo tu ya kupata khulka ya Ihswaan yaani utawa, bali Ameeleza tiba tano za kuwa na khulka hii; nazo ni hizi: (1) Kuyalinda macho yasimtazame asiye-harimishwa kuolewa. (2) Kuyahifadhi masikio yasiwahi kusikiliza sauti ya wasioharimishwa. (3) Kutokusikiliza visa vya wanawake hao wageni. (4) Kukiepusha na nafasi zinazoweza kumshawishi mtu kutenda uovu huo. (5) Kama hujafunga ndoa bado, ufunge saumu na kadhalika.

Hapa naweza kudai kwamba mafundisho hayo mema pamoja na tiba hizo zote zilizoelezwa na Kurani Tukufu yamefundishwa na Islam peke yake. Lipo hapa jambo moja la maarifa la kuzingatiwa. Nalo ni kwamba ile hali ya tabia ya asili iliyo chanzo cha tamaa ambayo mtu hawezi kuepukana nayo bila kuigeuza kikamilifu, haina budi kutaharuki wakati wowote inapopata nafasi, au kuingia katika hatari kubwa mno. Kwa hiyo, Mungu Mwenye Enzi Hakuagiza tuwatazame wanawake wageni bila wasiwasi na kuangalia mapambo yao na kuangalia dansi zao na mengineyo kwa sharti kwamba tuwe na nia nzuri. Wala Hakutuagiza kusikiliza nyimbo zao wasichana au maelezo ya uzuri wa miili yao hata kwa nia safi. Bali Amesisitiza tusiwatazame wanawake wageni kabisa wala kuangalia sehemu za mapambo yao, si kwa nia safi au nia mbaya; kadhalika

tusisikilize sauti zao nyororo na maelezo ya uzuri wa miili yao kwa nia safi au mbaya. Bali twapaswa kuchukia kuwasikiliza au kuwaona kama tuchukiavyo mzoga ili tusiteleze. Kwani kutazama ovyo bila kuangalia sheria hakuna budi kutatelezesha. Hivyo basi, Mwenyezi Mungu Anataka kwamba macho yetu na mioyo yetu iepukane na hatari zote; ndiyo maana Ameleta mafunzo bora ya aina hii. Hapana shaka kwamba vitendo bila masharti huleta hatari ya kuteleza. Kama tukiweka chapati nyororo mbele ya mbwa mwenye njaa, kisha tukitumai kwamba mbwa huyo hataweza kuzila chapati hizo, tutakuwa tumekosea kufikiri hivyo. Kwa hiyo, Mwenyezi Mungu Akapenda nguvu za binadamu zisipate nafasi ya siri pia kutumika vibaya wala isipatikane hali yoyote iwezayo kuhatarisha khulka.

Hiyo ndiyo hekima ya sheria ya Kiislamu ya wanawake kuvaa baibui. Katika Kitabu cha Mungu kuvaa baibui hakumaanishi kuwaweka wanawake kama wafungwa. Hiyo ni fikara ya wale wasio na elimu ya kanuni za Kiislamu. Bali shabaha yake ni kuwazuia wanawake na wanaume wasitazamane ovyo na kuonyesha mapambo yao, kwani ndani yake kuna heri kwa wote. Mwishowe ieleweke pia kwamba kujiepusha na kupaona pasipofaa kwa kuinamisha macho na kutazama vile tu vilivyoruhusiwa kunaitwa Ghadh-dhi Baswar. Kila mtawa apendaye kudumisha utakaso wa moyo wake hapaswi kuinua macho yake

ovyo upande wowote apendavyo kama wanyama; bali hupaswa kuzoea kuinamisha macho katika maisha ya ustaarabu. Hayo ndiyo mazoea yenye baraka yatakayoigeuza hali ya tabia ya asili kuwa khulka bora sana bila kuleta tofauti katika mahitaji yake ya maisha. Hiyo ndiyo khulka inayoitwa Ihswaan au Utawa.

Namna ya pili ya kuepukana na shari ndiyo khulka iitwayo Uamini au uaminifu, yaani kutopenda kumwudhi mwingine kwa kumnyang'anya mali yake kwa shari na nia mbaya. Basi ibainike kwamba Uamini au Uaminifu ni hali moja ya tabia ya asili ya mtu. Ndiyo sababu mtoto mchanga ambaye kwa sababu ya uchanga wake huwa na tabia ya asili wala hajapata mazoea mabaya, yeye naye huchukia kujimilikisha kitu cha mwingine kiasi hiki kwamba anamnyonya mama asiyekuwa mzazi wake kwa taklifu. Kama hawekewi mama wa kunyonya katika zama asipojijua itakuwa shida kubwa kumfanya amnyonye mama mwingine asiyekuwa mzazi wake katika zama ajijuapo. Bali pengine husumbuka mno, na yawezekana akurubie kufa, lakini huchukia tu kumnyonya mwanamke mwingine. Kuna siri gani ya kuchukia kiasi hicho? Ni hii kwamba hubeua kitabia kumwelekea mwingine minghairi ya mama yake. Sasa tukichunguza kwa makini sana tutatambua kwamba tabia hii ya mtoto kutoridhika kabisa na kujipatia kitu cha watu kiasi hiki kwamba anasumbuka, ndio mzizi wa Uamini na Uaminifu.

Mtu hawezi kuwa mwaminifu kikwelikweli mpaka achukie na kukirihika, kama afanyavyo mtoto, kunyakua mali ya watu. Lakini mtoto hatumii hali hii ya tabia ya asili katika mahali pake; ndiyo maana husumbuka sana kwa ujinga wake; kwa hiyo tabia yake hii ndiyo hali ya maumbile anayodhihirisha bila kujiweza: kwa hiyo kitendo chake hicho hakiwi khulka, ingawaje huo ndio mzizi wa khulka ya uaminifu katika tabia ya asili ya mtu. Na jinsi ambavyo mtoto hawezi kuitwa mwamana na mwaminifu kwa sababu ya hali yake hiyo, kadhalika yule mtu asiyetumia tabia yake hii ya asili katika mahali panapofaa hawezi kupata khulka hii. Kuwa mwamana na mwaminifu ni jambo gumu. Mtu hawi mwamana na mwaminifu mpaka mtu huyo atekeleze wajibu wake kwa kila jiha. Mathalan, Mwenyezi Mungu Amefahamisha njia ya uaminifu katika aya zifuatazo kwa kusema hivi:

وَلَا تُؤْتُوا السُّفَهَاءَ أَمْوَالَكُمُ الَّتِي جَعَلَ اللَّهُ لَكُمْ قِيَامًا وَارْزُقُوهُمْ فِيهَا
وَاكْسُوهُمْ وَقُولُوا لَهُمْ قَوْلًا مَّعْرُوفًا ﴿٦﴾ وَابْتَلُوا الْيَتَامَىٰ حَتَّىٰ إِذَا بَلَغُوا النِّكَاحَ
فَإِنْ آنَسْتُم مِّنْهُمْ رُشْدًا فَادْفَعُوا إِلَيْهِمْ أَمْوَالَهُمْ ۖ وَلَا تَأْكُلُوهَا إِسْرَافًا
وَبِدَارًا أَن يَكْبَرُوا ۚ وَمَن كَانَ غَنِيًّا فَلْيَسْتَعْفِفْ ۖ وَمَن كَانَ فَقِيرًا فَلْيَأْكُلْ
بِالْمَعْرُوفِ ۚ فَإِذَا دَفَعْتُمْ إِلَيْهِمْ أَمْوَالَهُمْ فَأَشْهِدُوا عَلَيْهِمْ ۚ وَكَفَىٰ بِاللَّهِ حَسِيبًا ﴿٧﴾[1]
وَلْيَخْشَ الَّذِينَ لَوْ تَرَكُوا مِنْ خَلْفِهِمْ ذُرِّيَّةً ضِعَافًا خَافُوا عَلَيْهِمْ فَلْيَتَّقُوا

[1] An-Nisaa, 4:6-7

اللّٰهَ وَلْيَقُوْلُوْا قَوْلًا سَدِيْدًا ۝١٠ اِنَّ الَّذِيْنَ يَاْكُلُوْنَ اَمْوَالَ الْيَتٰمٰى ظُلْمًا
اِنَّمَا يَاْكُلُوْنَ فِيْ بُطُوْنِهِمْ نَارًا ۭ وَسَيَصْلَوْنَ سَعِيْرًا ۝١١ [1]

Tafsiri: Kama yupo kati yenu mwenye mali ambaye hana fahamu nzuri na ipo hofu kwamba atapoteza mali yake, kama vile mtoto yatima asiyebalehe, hapo mkiwa wasimamizi msimpe mali yake, kwani mfumo wa uchumi na maisha huitegemea hiyo mali. Bali kutoka katika mali hii yake yeye apatiwe chakula na mavazi kulingana na haja, na mwambieni maneno mazuri, yaani yale yatakayokuza akili na busara yake na kwa njia hii apate ulezi ipasavyo ili asibaki bila kuelimika. Kama yu mtoto wa mfanya biashara, afundishwe njia ya kufanya biashara na kama ni ufundi mwingine basi na afundishwe huo ufundi barabara. Ilmuradi mwendelee kumlea na kumfunza na pia mara kwa mara kumkagua ili kujua iwapo ameisha zingatia mafunzo yenu au bado. Na anapobalehe, yaani akiwa mwenye umri wa miaka 18 hivi, mpatieni mali yake sharti mwone kwamba amepevuka kiakili na ataweza kuhifadhi mali yake. Wala msitumie mali yake kwa fujo wala msiharibu mali yake kwa kutumia haraka haraka kwa hofu kwamba akibalehe atachukua mali yake. Msimamizi aliyetajirika asichukue katika mali hiyo kiasi fulani

[1] An-Nisaa, 4:10-11

kama ujira wa huduma aliyotoa, lakini mtu mwenye hali ndogo anaweza kuchukua kiasi kipasacho.

Waarabu walikuwa na desturi maarufu kwamba wasimamizi wa mali ya mayatima wakihitaji kuchukua chochote katika mali ya mayatima, walikuwa wakipata sehemu ya faida ipatikanayo kwa kutumia mali hiyo katika biashara; lakini hawakuharibu rasilmali. Basi Kurani yaashiria kwenye desturi hii kwamba nanyi mfanye hivyo. Kisha imeagizwa kuwapa mali zao mayatima mbele ya mashahidi. Na kama mtu akikurubia kufa naye anaowatoto dhaifu na wadogo, yeye mtu huyo hapaswi kufanya wasia utakaowanyima watoto haki zao. Wale wanaokula mali ya mayatima kwa njia ya kuwadhulumu, hao hula moto siyo mali, nao watatupwa katika moto uunguzao.

Sasa angalieni Mwenyezi Mungu Alivyoeleza jiha nyingi za uaminifu. Kwa hiyo, uaminifu wa kweli ndio ule unaozingatia jiha zote hizo. Na kama mtu haangalii jiha zote hizo za uaminifu kwa kutumia akili yake yote, hapo uaminifu wake utakuwa na hiyana za aina nyingi zilizofichama ndani yake. Kisha mahali pengine imeagizwa:

وَلَا تَأْكُلُوْٓا اَمْوَالَكُمْ بَيْنَكُمْ بِالْبَاطِلِ وَتُدْلُوْا بِهَآ اِلَى الْحُكَّامِ لِتَأْكُلُوْا فَرِيْقًا

مِّنْ أَمْوَالِ النَّاسِ بِالْإِثْمِ وَأَنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿١٨٩﴾ [1]

إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُكُمْ أَنْ تُؤَدُّوا الْأَمَانَاتِ إِلَىٰ أَهْلِهَا [2]

إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْخَائِنِينَ ﴿٥٩﴾ [3]

وَأَوْفُوا الْكَيْلَ إِذَا كِلْتُمْ وَزِنُوا بِالْقِسْطَاسِ الْمُسْتَقِيمِ [4]

وَلَا تَبْخَسُوا النَّاسَ أَشْيَاءَهُمْ [5]

وَلَا تَعْثَوْا فِي الْأَرْضِ مُفْسِدِينَ ﴿٦١﴾ [6]

وَلَا تَتَبَدَّلُوا الْخَبِيثَ بِالطَّيِّبِ [7]

Yaani: Msiliane mali zenu kwa njia isiyo halali wala msitoe mali zenu kama rushwa kwa mahakimu ili kwa kusaidiwa nao mzinyakue mali za watu. Zirudisheni amana kwa wenyewe; Mungu Hawapendi wenye kuhini. Na timizeni kipimo mpimapo, na pimeni kwa mizani iliyo sawa, wala msiwapunje watu mali zao. Wala msitembee ardhini kwa nia ya kuleta ufisadi, yaani kwa nia ya wizi, ujambazi, kusingizia au kujipatia mali ya watu kwa njia isiyo halali. Kisha Amesema, wala msibadilishe mazuri kwa mabaya. Ndiyo kusema kwamba jinsi

---

1 Al-Baqarah, 2:189

2 An-Nisaa, 4:59

3 Al-Anfaal, 8:59

4 Banii Israaiil, 17:36

5 Al-A‘raaf, 7:86

6 Al-Baqarah, 2:61

7 An-Nisaa, 4:3

ambavyo ni haramu kula mali ya watu, ndivyo ilivyo haramu kuuza kilicho kibovu, na pia kuchukua kizuri na kutoa kilicho kibaya.

Katika aya hizo Mwenyezi Mungu Amekwisha eleza njia zote za hiyana kikamilifu bila kuacha hata njia moja. Hakuagiza tu usiibe ili isije mjinga akaelewa kwamba wizi tu ndio haramu kwake lakini njia zingine mbaya zimehalalishwa. Ilmuradi, kama mtu hanayo khulka hii ya uaminifu kwa marefu na mapana jinsi ilivyoelezwa na Kurani, bali anaonyesha uaminifu katika baadhi ya mambo tu, hapo kitendo chake kicho hakitahesabiwa kuwa ni khulka ya uaminifu, bali hii ndiyo hali ya tabia ya asili iliyojidhihirisha bila kutumia akili na busara.

Namna ya tatu ya khulka inayohusiana na kuepukana na ubaya ni ile iitwayo Hudnah au Haun kwa Kiarbu — yaani kutokumdhuru mtu kimwili kwa njia ya kumdhulumu na kuishi kwa amani pasipo shari. Hapana shaka kwamba kukaa kwa amani na suluhu ndiyo khulka bora sana na ni kitu cha lazima kwa binadamu. Na ile nguvu ya tabia ya asili inayopatikana katika mtoto ambayo ikirekebishwa huitwa suluhu ndio upendo au tuseme uhusiano. Ni wazi kwamba mtu katika hali ya tabia ya asili ambapo hajapata akili, hawezi kufahamu maana ya suluhu wala vita. Wakati huo mtu huwa na tabia ya upendano ulio chanzo cha suluhu ambayo haiingii katika khulka kwa sababu ya kukosekana matumizi ya akili na

busara. Bali hiyo itahesabiwa kuwa ni khulka pindi mtu atakapoitumia katika mahali pake pa kufaa baada ya kuepukana na kila shari. Kuhusu hiyo Mwenyezi Mungu Anasema:

وَأَصْلِحُوا ذَاتَ بَيْنِكُمْ ۖ [1]

وَالصُّلْحُ خَيْرٌ ۗ [2]

وَإِن جَنَحُوا لِلسَّلْمِ فَاجْنَحْ لَهَا [3]

عِبَادُ الرَّحْمَٰنِ الَّذِينَ يَمْشُونَ عَلَى الْأَرْضِ هَوْنًا [4]

وَإِذَا مَرُّوا بِاللَّغْوِ مَرُّوا كِرَامًا ﴿٧٣﴾ [5]

ادْفَعْ بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ فَإِذَا الَّذِي بَيْنَكَ وَبَيْنَهُ عَدَاوَةٌ كَأَنَّهُ وَلِيٌّ حَمِيمٌ ﴿٣٥﴾ [6]

Yaani: Suluhisheni mambo baina yenu (8:2). Suluhu ni bora (4:129). Wakielekea kwenye suluhu, nawe uelekee kwayo (8:62). Waja wa Mungu wanatembea katika ardhi kwa suluhu (25:64) na wakisikia lolote la kipuuzi kwa mtu yeyote lililo chanzo cha ugomvi, hulikwepa na kupita njia yao. Ndiyo kusema kwamba watu wema hawapendi kushindana mpaka wasumbuke sana. Na njia ya kutambua wakati wa suluhu ni kwamba mtu asijali mambo madogo

---

[1] Al-Anfaal, 8:2

[2] An-Nisaa, 4:129

[3] Al-Anfaal, 8:62

[4] Al-Furqaan, 25:64

[5] Al-Furqaan, 25:73

[6] Haa Miim As-Sajdah, 41:35

madogo ya uchochezi au uchokozi, bali asamehe tu. Itambulikane kwamba neno 'Laghwu' (upuuzi) lililotumika katika aya hiyo hapo juu mfano wake ni kama mtu kwa nia ya kuudhi anatamka la ovyo au anatenda tendo fulani ambalo halina madhara hasa, basi alama ya kupenda suluhu ni kutokujali tamko au tendo hilo na kuonyesha uungwana. Lakini kama udhia wenyewe haupo katika eneo la 'upuuzi', bali mtu amedhurika kimaisha au kimali au kiheshima, hapo khulka ya suluhu haihusikani, bali kusamehe dhambi kama hiyo ndiyo khulka ambayo huitwa 'afwu' (Msamaha), ambayo itaelezwa mbele inshallah. Kisha Amesema, kama mtu kwa nia mbaya akitamka la ovyo au la kipuuzi an kisha mkimjibu kwa suluhu, basi kwa kuonyesha khulka hii, adui atageuka kuwa rafiki (41:35). Ilmuradi mahali pafaapo pa kuonyesha suluhu ni pale tu ambapo mtu ametendewa ubaya kiasi cha kutokuleta madhara hasa, bali iliyotumika ni midomo michafu tu.

Miongoni mwa khulka zinazohusikana na kuepukana na shari, aina ya nne ni 'Rifq' na 'Kauli Hasan' (Upole na Kauli Njema). Khulka hiyo huzalika kutoka katika ile hali ya umbile iitwayo 'Twalaqat', yaani. uchangamfu. Mtoto asiye na uwezo wa kuongea huonyesha uchangamfu badala ya upole na kauli njema. Hii ndiyo dalili ya kuhakikisha kwamba ule mzizi ambamo tawi hilo huota ndio uchangamfu. Uchangamfu ndiyo nguvu lakini upole na kusema

kauli njema ni khulka ambayo hupatikana wakati uchangamfu utumikapo katika mahali pafaapo. Kuhusu habari hii Mwenyezi Mungu Amefundisha:

وَقُوْلُوْا لِلنَّاسِ حُسْنًا [1]

لَا يَسْخَرْ قَوْمٌ مِّنْ قَوْمٍ عَسٰٓى اَنْ يَّكُوْنُوْا خَيْرًا مِّنْهُمْ وَلَا نِسَآءٌ مِّنْ نِّسَآءٍ
عَسٰٓى اَنْ يَّكُنَّ خَيْرًا مِّنْهُنَّ ۚ وَلَا تَلْمِزُوْٓا اَنْفُسَكُمْ وَلَا تَنَابَزُوْا بِالْاَلْقَابِ ؕ [2]

اجْتَنِبُوْا كَثِيْرًا مِّنَ الظَّنِّ ۫ اِنَّ بَعْضَ الظَّنِّ اِثْمٌ وَّلَا تَجَسَّسُوْا
وَلَا يَغْتَبْ بَّعْضُكُمْ بَعْضًا ؕ... وَاتَّقُوا اللّٰهَ ؕ اِنَّ اللّٰهَ تَوَّابٌ رَّحِيْمٌ ﴿۱۲﴾ [3]

وَلَا تَقْفُ مَا لَيْسَ لَكَ بِهٖ عِلْمٌ ؕ اِنَّ السَّمْعَ
وَالْبَصَرَ وَالْفُؤَادَ كُلُّ اُولٰٓئِكَ كَانَ عَنْهُ مَسْئُوْلًا ﴿۳۶﴾ [4]

Yaani: Waambie watu yaliyo mema hasa. Watu wasiwacheke watu wengine huenda wakawa bora kuliko wao; wala wanawake kwa wanawake huenda wakawa bora kuliko wao. Wala msisingiziane, wala msiitane kwa majina mabaya (49:12). Jiepusheni sana na kufanya shuku, maana shuku pengine inakuwa dhambi; wala msipeleleze aibu za watu wala baadhi yenu wasiwatete wengine (49:13). Usimsingizie mwingine kwa jambo usiloweza kulihakikisha; kumbukeni kwamba kila kiungo kitaadhibiwa kwa

---

[1] Al-Baqarah, 2:84

[2] Al-Hujuraat, 49:12

[3] Al-Hujuraat, 49:13

[4] Banii Israaiil, 17:37

dhambi zake; na masikio, macho, na moyo, hivyo vyote vitaulizwa (17:37).

## NJIA ZA KUTENDA MEMA

Baada ya kueleza namna za khulka zihusuzo kuepukana na shari, sasa natoa maelezo ya aina ya pili ya khulka zinazohusu kutenda mema.

Miongoni mwa khulka za namna hiyo, ya kwanza ni Msamaha, yaani kusamehe makosa ya watu. Huko kufanya wema kunapatikana hivi kwamba yule atendaye dhambi huleta dhara naye anapaswa apewe dhara kwa kuadhibiwa, kufungwa gerezani, kufainishwa au kwa kupigwa na yule aliyekosewa. Kama huyo mkosefu akisamehewa, kwa sharti kwamba msamaha uonekane kuwa ndicho kitu cha kumfaa, basi hapo ndipo umemfanyia wema. Kuhusu jambo hili Kurani Tukufu hufundisha:

وَالۡكٰظِمِيۡنَ الۡغَيۡظَ وَالۡعَافِيۡنَ عَنِ النَّاسِ ؕ [1]

جَزٰٓؤُا سَيِّئَةٍ سَيِّئَةٌ مِّثۡلُهَا ۚ فَمَنۡ عَفَا وَاَصۡلَحَ فَاَجۡرُهٗ عَلَى اللّٰهِ ؕ [2]

Yaani, watu wema ni wale wanaozuia ghadhabu wakati ipasapo kuzuia ghadhabu, na wanasamehe mahali ipasapo kusamehe (3:135). Malipo ya ubaya ni ubaya ulio sawa na huo; lakini anayesamehe sharti msamaha urekebishe hali na wala usilete shari, huo,

[1] Aali‘Imraan, 3:135

[2] Ash-Shu‘araa, 26:41

yaani msamaha ukitumika katika mahali panapofaa na wala siyo mahali pasipofaa, basi mtu huyo atapata ujira (42:41).

Aya hii inahakikisha kwamba Kurani Tukufu haifundishi kutokushindana kwa vyovyote na shari sikuzote na kutokuwaadhibu wakati wote. Bali sheria yenyewe ni kuangalia kwamba wakati huo msamaha unafaa kwa mkosefu na kwa watu kwa jumla au kumwadhibu kutarekebisha hali. Maana, pengine mkosefu anatubu akisamehewa, lakini wakati mwingine anajasiri kutenda dhambi zaidi ukimsamehe. Hivyo, basi, Mwenyezi Mungu Anasema, msizoee kusamehe ovyo, bali fikirini kwa makini kwamba wema utapatikana katika kusamehe wakati huu au katika kuadhibu, kisha fanyeni lile lifaalo. Tukichunguza tabia za binadamu tunakuta kwamba baadhi ya watu wana tabia ya bughudha na inadi hata kwamba wanakumbuka uadui tangu wakati wa mababu zao; kadhalika kuna wengine wenye tabia ya kusamehe kupita kiasi hata kwamba wakati mwingine msamaha wao unaleta fedheha. Wanadhihirisha upole na msamaha pasipo kuona haya, kinyume cha heshima, ghera na utakaso, bali hutia ila katika wema wa mtu. Msamaha huo unawachukiza watu wengine. Ndiyo sababu Kurani Tukufu imeweka sharti kwamba kila khulka itumiwe katika mahali pafaapo; wala haikukubali ile khulka itumikayo mahali pasipofaa.

Kumbukeni kwamba msamaha peke yake sio khulka, bali ni nguvu moja iliyomo katika umbile la watoto. Mtoto anapopigwa na mwingine, hata kama kwa nia mbaya, mtoto huyo husahau habari hii baada ya muda kidogo na humjia tena kwa upendo. Hata kama mtu aliyempiga huyo mtoto alikuwa amenuia kumwua, hata hivyo yule mtoto anachangamka tu kwa maneno yake mazuri. Kwa hiyo, msamaha kama huu hautahesabiwa kuwa khulka isipokuwa tu ukitumika katika mahali panapofaa; la sivyo hiyo ni hali ya umbile tu. Kuna watu wachache kabisa duniani wanaoweza kupambanua baina ya nguvu ya tabia ya asili na khulka. Nimekariri mara nyingi kwamba khulka hudhihirika sawa na hali ifaayo, lakini umbile huonekana wakati mwingine katika mahali pasipofaa. Angalieni, hata ng'ombe ni mnyama asiye na shari, na mbuzi ni mpole; lakini kwa sababu ya tabia hizo tu hatuwezi kuwahesabu kuwa wenye khulka, kwani hawakujaaliwa akili ya kupambanua mahali pafaapo na pasipofaa. Hekima ya Mungu, na kitabu cha kweli kikamilifu kimeiwekea kila khulka sharti ya kuangalia mahali pafaapo.

Khulka ya pili kati ya khulka njema ni adili na ya tatu ni hisani ya nne ni kuwapa watu kama uwapavyo ndugu. Mwenyezi Mungu Anasema:

إِنَّ اللّٰهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالْإِحْسَانِ وَإِيْتَآئِ ذِى الْقُرْبٰى

وَيَنْهَىٰ عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنكَرِ وَالْبَغْيِ ۚ [1]

Yaani: Mwenyezi Mungu Anaamuru usawa (adili) na kutenda wema ukifanyiwa wema. Na kama kuna mahali pafaapo pa kutenda hisani, basi fanyeni hisani. Na kama ipo nafasi ya kufanya zaidi ya hisani na kutenda wanavyotendewa jamaa wa karibu, basi fanyeni hivyo. Na Mwenyezi Mungu Hukataza kupita mipaka au kufanya pasipofaa au kutokuifanya mahali panapofaa kuifanya, au kuipunguza khulka ya kutendea kama kuwatendea ndugu au kuizidisha kuliko kiasi cha kufaa kuonyesha huruma nyingi mno isiyostahili. Katika aya hiyo hapo juu yameelezwa madaraja matatu ya kutenda wema. Kwanza ni daraja la kufanya wema kwa kulipa wema uliofanywa tayari. Hili ni daraja dogo. Hata mtu mwema wa kawaida anaweza kujipatia khulka hii kwa kuwafanyia wema wale wanaomfanyia wema.

Daraja la pili ni gumu kidogo kuliko hilo la kwanza nalo ni kufanya wema bila wewe kufanyiwa wema kwanza, na kuwanufaisha wengine kwa njia ya hisani bila ya wao kwanza kukufanyia wema. Hiyo ni khulka ya daraja la wastani. Lakini ubaya wa hisani ni kwamba mtu huwaza kwamba amefanya hisani na kwa akali hupenda kushukuriwa au kuombewa dua. Na kama aliyefanyiwa hisani akimpinga yeye wakati

---

[1] An-Nahl, 16:91

mwingine katika jambo fulani, hapo humwita mtu asiye na shukurani; na pengine humtwisha mzigo mzito zaidi ya uwezo wake kwa kumkumbusha hisani yake. Mwenyezi Mungu Akiwaonya wafanyao hisani Amesema:

لَا تُبْطِلُوا صَدَقٰتِكُمْ بِالْمَنِّ وَالْاَذٰى ۙ [1]

Yaani, Enyi mfanyao hisani, sadaka zenu ambazo shina lake ni usadiki (ukweli wa moyo) msiziharibu kwa masimbulizi na udhia. Neno sadaka limetokana na neno Swidq (usadiki); kwa hivyo, kama hamna ukweli na ikhlasi katika moyo, sadaka haiwi tena sadaka, bali ni kitendo cha kutaka kuonwa na watu. Ilmuradi, ipo kasoro katika mwenye kufanya hisani kwamba wakati mwingine akikasirika anakumbusha hisani yake; ndiyo sababu Mwenyezi Mungu Amewaonya wafanyao hisani.

Daraja la tatu la kuwatendea wema wengine Alivyosema Mungu Mwenye Enzi ni kwamba mtu asiwe na wazo la hisani wala kutazamia shukrani, bali kwa jazba ya huruma wema utendeke kama watendewavyo jamaa wa karibu, kama mama anavyomtendea wema mwanawe kwa jazba na huruma. Hili ni daraja la mwisho katika kufanya wema ambalo zaidi yake haiwezekani. Lakini Mwenyezi Mungu Ameambatanisha namna hizo zote

---

[1] Al-Baqarah, 2:265

za kufanya wema na wakati au mahali panapofaa; na aya iliyotajwa imekwisha eleza bayana kwamba wema huo usipofanyika katika mahali pafaapo, utageuka kuwa ubaya: adili itakuwa 'fahshaa' yaani kupita kiasi hata ikachafuka; na hisani kuwa 'munkar' yaani kuwa na hali ikanwayo na akili na dhamiri; na kadhalika hiyo khulka ya kuwatendea watu kama kuwatendea ndugu itakuwa 'Baghyi', yaani jazba ya huruma nyingi hiyo bila kuangalia mahali pafaapo itakuwa na sura mbaya sana. "Baghyi" kwa hakika maana yake ni mvua nyingi kuliko kiasi inayoangamiza mashamba. Na neno hilo pia lamaanisha kuzidi kulilo kiasi cha haki kipasacho. Kwa kifupi, katika khulka hizo tatu, yoyote ambayo haitatendeka katika mahali panapofaa, itageuka kuwa ubaya. Ndiyo maana hizo tatu zimewekewa sharti kuwa zitendeke sawa na hali na mahali panapofaa. Ikumbukwe pia kwamba adili peke yake au hisani au huruma afanyiwayo ndugu haiitwi khulka, bali hizo ni hali za umbile ambazo hupatikana hata katika watotob kabla hawajapevuka kiakili. Kwa khulka kupatikana ni sharti kwanza akili ipatikane na kila nguvu ya akili iliyo umbile itumike sawa na mahali panapofaa.

Kisha kuna maagizo mengine pia ya muhimu ndani ya Kurani Tukufu ambayo yote hayo yameelezwa kwa kutumia Alif Lam inayotumika kwa kukifanya kitu kuwa maalum, na kwa njia hii Mungu

Ameashiria kutia maanani wakati na mahali pafaapo, jinsi Asemavyo:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا أَنْفِقُوا مِنْ طَيِّبَاتِ مَا كَسَبْتُمْ ... وَلَا تَيَمَّمُوا الْخَبِيثَ مِنْهُ [1]

لَا تُبْطِلُوا صَدَقَاتِكُمْ بِالْمَنِّ وَالْأَذَىٰ كَالَّذِي يُنْفِقُ مَالَهُ رِئَاءَ النَّاسِ [2]

أَحْسِنُوا إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُحْسِنِينَ ﴿١٩٦﴾ [3]

إِنَّ الْأَبْرَارَ يَشْرَبُونَ مِنْ كَأْسٍ كَانَ مِزَاجُهَا كَافُورًا ﴿٦﴾ عَيْنًا يَشْرَبُ بِهَا عِبَادُ اللَّهِ يُفَجِّرُونَهَا تَفْجِيرًا ﴿٧﴾ [4]

وَيُطْعِمُونَ الطَّعَامَ عَلَىٰ حُبِّهِ مِسْكِينًا وَيَتِيمًا وَأَسِيرًا ﴿٩﴾ إِنَّمَا نُطْعِمُكُمْ لِوَجْهِ اللَّهِ لَا نُرِيدُ مِنْكُمْ جَزَاءً وَلَا شُكُورًا ﴿١٠﴾ [5]

وَآتَى الْمَالَ عَلَىٰ حُبِّهِ ذَوِي الْقُرْبَىٰ وَالْيَتَامَىٰ وَالْمَسَاكِينَ وَابْنَ السَّبِيلِ وَالسَّائِلِينَ وَفِي الرِّقَابِ [6]

إِذَا أَنْفَقُوا لَمْ يُسْرِفُوا وَلَمْ يَقْتُرُوا وَكَانَ بَيْنَ ذَٰلِكَ قَوَامًا ﴿٦٨﴾ [7]

وَالَّذِينَ يَصِلُونَ مَا أَمَرَ اللَّهُ بِهِ أَنْ يُوصَلَ وَيَخْشَوْنَ رَبَّهُمْ وَيَخَافُونَ سُوءَ الْحِسَابِ ﴿٢١﴾ [8]

---

[1] Al-Baqarah, 2:268
[2] Al-Baqarah, 2:265
[3] Al-Baqarah, 2:196
[4] Ad-Dahr, 76:6-7
[5] Ad-Dahr, 76:9-10
[6] Al-Baqarah, 2:178
[7] Al-Furqaan, 25:68
[8] Ar-Ra‘d, 13:22

وَفِيٓ أَمْوَالِهِمْ حَقٌّ لِّلسَّآئِلِ وَالْمَحْرُومِ ﴿٢٠﴾ [1]

الَّذِينَ يُنْفِقُونَ فِي السَّرَّآءِ وَالضَّرَّآءِ [2]

وَأَنْفَقُوا مِمَّا رَزَقْنٰهُمْ سِرًّا وَّعَلَانِيَةً [3]

إِنَّمَا الصَّدَقٰتُ لِلْفُقَرَآءِ وَالْمَسٰكِينِ وَالْعٰمِلِينَ عَلَيْهَا وَالْمُؤَلَّفَةِ قُلُوبُهُمْ وَفِي
الرِّقَابِ وَالْغٰرِمِينَ وَفِي سَبِيلِ اللهِ وَابْنِ السَّبِيلِ ۖ فَرِيضَةً مِّنَ اللهِ ۗ وَاللهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٦٠﴾ [4]

لَنْ تَنَالُوا الْبِرَّ حَتّٰى تُنْفِقُوا مِمَّا تُحِبُّونَ ۚ [5]

وَآتِ ذَا الْقُرْبٰى حَقَّهُ وَالْمِسْكِينَ وَابْنَ السَّبِيلِ وَلَا تُبَذِّرْ تَبْذِيرًا ﴿٢٧﴾ [6]

وَبِالْوٰلِدَيْنِ إِحْسَانًا وَّبِذِي الْقُرْبٰى وَالْيَتٰمٰى وَالْمَسٰكِينِ وَالْجَارِ ذِي الْقُرْبٰى
وَالْجَارِ الْجُنُبِ وَالصَّاحِبِ بِالْجَنْبِ وَابْنِ السَّبِيلِ ۙ وَمَا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ ۗ
إِنَّ اللهَ لَا يُحِبُّ مَنْ كَانَ مُخْتَالًا فَخُورًا ﴿٣٦﴾ الَّذِينَ يَبْخَلُونَ وَيَأْمُرُونَ النَّاسَ بِالْبُخْلِ
وَيَكْتُمُونَ مَآ آتٰهُمُ اللهُ مِنْ فَضْلِهِ ۗ [7]

Tafsiri: Enyi mlioamini, watoleeni watu sehemu ya mali zenu kwa njia ya ukarimu au hisani au sadaka, mali yenu iliyotakasika, yaani isiyochanganyika na mali ya wizi au rushwa au hiyana au ulaghai na dhuluma. Mwepukane na nia ya kuwapa watu mali

---

[1] Adh-Dhaariyaat, 51:20

[2] Aali'Imraan, 3:135

[3] Ar-Ra'd, 13:23

[4] At-Taubah, 9:60

[5] Aali'Imraan, 3:93

[6] Banii Israaiil, 17:27

[7] An-Nisaa, 4:37-38

isiyo safi. Na jambo la pili ni kwamba msibatilishe ukarimu wenu na wema kwa masimbulizi na udhia. Wala msishike njia ya kutoa mali kwa ajili ya kuonwa na watu. Na wafanyieni hisani viumbe wa Mungu, kwani Mwenyezi Mungu Huwapenda wafanyao hisani. Wafanyao wema wa kweli watanyweshwa katika vikombe vilivyochanganyika na kafuri, yaani mioyo yao itatakaswa isipate tena uchungu wa kidunia na majuto na tamaa mbaya. Neno Kafuri linatokana na neno Kafar linalomaanisha kwa Kiarabu kuzuia na kufunika. Basi muradi wake ni kwamba maono yao mabaya yatazuiwa, nao watatakasika na wataburudika kwa kumtambua Mungu.

Kisha Akisema kwamba watu hao watajinywea katika chemchemi ambayo wanaichimba wenyewe hivi leo kwa mikono yao. Hapa Ametoboa siri kubwa ya hekima ya Peponi; mwenye kutambua na atambue. Tena Anasema kuwa ni tabia ya wenye kufanya wema wa kweli kwamba kwa ajili ya Mapenzi ya Mungu peke yake wanawalisha maskini, mayatima na wafungwa vile vyakula wanavyopenda wenyewe kwa ajili yao, na husema hatuwafanyii hisani yoyote bali twatenda hivyo ili tu Mungu Atuwie radhi, na huduma hii ni kwa ajili ya upendo Wake tu; hatutumai malipo kutoka kwenu wala hatuhitaji mtutolee shukurani. Hii inaashiria kwenye jambo hili kwamba hao wanatimiza ile namna ya tatu ya wema unaosababishwa na jazba ya kuhurumia. Watawa wa kweli huwa na tabia ya kuwasaidia jamaa wa karibu

kwa mali zao ili kupata radhi ya Mungu na pia katika mali hiyo wanawatunza mayatima na kuwalea na kuwaelimisha na wanawaepusha maskini na kusikia njaa, na kuwahudumia wasafiri na waombaji. Pia wanatoa mali hizo kwa kuwaachisha huru watumwa na kulipa madeni ya waliolemewa na madeni. Wala hawatumii mali zao kwa fujo wala hawawi na tabia ya ubahili bali wanashika njia ya wastani. Mahali panapofaa kutia kiraka hutia kiraka. Na wanamwogopa Mungu. Na katika mali zao kuna haki za waombao na wasioomba. Katika 'wasioomba' huingia mbwa, paka, mashorewanda, ng'ombe, punda, mbuzi na wengineo. Hata hawawi wachoyo katika hali za shida, mapato madogo, siku za ukame; bali katika hali ya shida pia huonyesha ukarimu sawa na uwezo. Pengine wanatoa sadaka kisirisiri na pengine kidhahiri — kwa siri, ili kuepukana na tabia ya kuonwa na watu; na kidhahiri, kwa kuwahimiza wengine. Kuhusu mali inayotolewa kisadaka iangaliwe kuwapa kwanza wanaohitaji. Naam, wenye kutunza mali hiyo na kusimamia utumiaji wake pia waweza kupewa kidogo mali hiyo. Pia huweza kutolewa katika mfuko huo mali kwa kumwepusha mtu na maovu. Vile vile mali hiyo itatumika kwa kuwaweka huru watumwa na kuwasaidia wenye haja, wenye deni na wenye shida na pia katika njia nyingine ambazo ni njia za Mungu. Hamwezi kupata wema hasa mpaka mtoe kwa kuwahurumia wanadamu ile mali mnyoipenda zaidi. Toeni haki za wenye hali ndogo na maskini; wahudumieni wasafiri. Na mjiepushe na kutumia mali

kwa fujo, yaani katika sherehe za arusi na anasa na katika mila kuhusu kuzaliwa mwana. Wafanyieni wema wazazi wenu na pia jamaa wa karibu na mayatima na maskini na jirani aliye jamaa yenu na jirani asiye jamaa yenu wa karibu na msafiri, mtumishi, mtumwa, farasi, mbuzi, ng'ombe dume na jike na wanyama wote mnaowamiliki, kwani Mungu Aliye Mungu wenu Hupenda tabia hizi. Yeye Hawapendi wasiojali, na wanaojifikiria nafsi zao tu. Wala Hawataki wachoyo na wale wanaowafunza wengine uchoyo na wanaoficha mali zao, yaani huwaambia wenye haja hatuna mali.

## USHUJAA WA KWELI

Miongoni mwa hali za tabia ya asili ya binadamu kuna hali inayolingana na ushujaa. Mtoto mchanga wakati mwingine anatia mkono wake katika moto kwa sababu ya hiyo hali; kwani mtoto mdogo kwa sababu ya ile sifa ya asili ya binadamu ya kupata ushindi hakiogopi kitu chochote kabla hajatambua hatari yake. Katika hali hiyo, mtu anajasiri kuwakabili simba na wanyama wengine mbuai wa msituni, na pengine anajitokeza kupigana peke yake na watu wengi, na anajulikana baina ya watu kwamba yu shujaa mkubwa sana. Lakini hiyo ni hali ya tabia ya asili tu inayokuwepo hata katika wanyama wengine wakali, bali hata katika mbwa pia. Lakini ushujaa wa kweli ambao unalingana na wakati na mahali pafaapo, nao ni khulka njema mojawapo, ndiyo mambo yanayotekelezwa sawa na mahali panapofaa ambayo

yametajwa katika maneno matukufu ya Mwenyezi Mungu kama ifuatavyo:

وَالصّٰبِرِيْنَ فِي الْبَاْسَآءِ وَالضَّرَّآءِ وَحِيْنَ الْبَاْسِ ؕ [1]

وَالَّذِيْنَ صَبَرُوا ابْتِغَآءَ وَجْهِ رَبِّهِمْ [2]

اَلَّذِيْنَ قَالَ لَهُمُ النَّاسُ اِنَّ النَّاسَ قَدْ جَمَعُوْا لَكُمْ فَاخْشَوْهُمْ
فَزَادَهُمْ اِيْمَانًا ۖ وَّقَالُوْا حَسْبُنَا اللّٰهُ وَنِعْمَ الْوَكِيْلُ ﴿١٧٣﴾ [3]

وَلَا تَكُوْنُوْا كَالَّذِيْنَ خَرَجُوْا مِنْ دِيَارِهِمْ بَطَرًا وَّرِئَآءَ النَّاسِ [4]

Yaani, mashujaa ni wale ambao wanapokuwa vitani au wakipata shida hawakimbii. Wanasubiri katika vita na katika shida kwa kupata radhi ya Mungu. Hukusudia kumpendeza Mungu na wala siyo kuonyesha ushujaa wao. Wanatishwa kwa kuambiwa kwamba watu wameungana pamoja kuwaadhibuni, basi waogopeni; lakini wao huzidi katika imani kwa sababu ya kutishwa, na husema: Mungu Anatosha. Yaani ushujaa wao sio kama wa mbwa na wanyama mbuai uaosababishwa na jazba iliyo tabia ya asili inayoelekea upande mmoja tu; bali ushujaa wao huwa na pande mbili: pengine wanashindana na tamaa zao za nafsi kwa ushujaa wao wa kidhati na huzishinda, na pengine wanapoona inafaa

[1] Al-Baqarah, 2:178
[2] Ar-Ra‘d, 13:23
[3] Aali‘Imraan, 3:174
[4] Al-Anfaal, 8:48

kukabiliana na adui, hapo wanashindana naye ili kuusaidia ukweli wale siyo kwa jazba ya kibinafsi. Na huonyesha ushujaa kwa kumtegemea Mungu wala siyo kwa kujitegemea nafsi zao. Msingi wa ushujaa wao siyo kuonwa na watu au maringo wala kufuata tamaa za nafsi, bali kwa kila jiha hutanguliza radhi ya Mungu.

Katika aya hizo imefahamishwa kwamba asili ya ushujaa wa kweli ni subira na uimara. Kusimama imara wakati wa kushambuliwa na tamaa za nafsi au balaa lingine linaloshambulia kama maadui na kutokimbia kama mwoga ndio ushujaa halisi. Hivyo, kuna tofauti baina ya ushujaa wa binadamu na wanyama mbuai. Mnyama mkali hudhihirisha jazba na ghadhabu kwa upande mmoja peke yake; lakini binadamu mwenye ushujaa wa kweli huchagua kati ya kushindana na kutokushindana kwa kuangalia kipi kitafaa wakati huo.

## UKWELI

Na miongoni mwa tabia za asili za mtu kuna ukweli pia. Mwanadamu hapendi kusema uwongo bila kuhimizwa na tamaa ya nafsi, na kuchukia na kusita kuongopa. Ndiyo sababu humkasirikia mtu anayejulikana kuwa mwongo na kumdunisha. Lakini hali hii pekee ya tabia ya asili haiwezi kuingia katika khulka njema, kwani hata watoto wadogo na wendawazimu nao huweza kuonyesha hali hii.

Uhakika wenyewe ni kwamba mtu hawezi kuhesabiwa kuwa mkweli hasa mpaka kwanza ajitenge mbali na tamaa za nafsi zinazomzuia asiseme kweli. Kwani ikiwa mtu anasema kweli katika mambo yasiyompa hasara yoyote, lakini anapoona heshima yake au mali yake au uhai wake uko katika hatari huongopa kwa haraka na kunyamaza asiseme kweli, basi kuna tofauti gani baina yake na wenye wazimu na watoto wadogo. Je watoto na wenye wazimu hawasemi kweli ya aina hii? Hakuna mtu duniani aongopaye hivi hivi tu bila kuhimizwa na jambo fulani. Basi kweli ile inayoachwa wakati wa hasara haiingii katu katika khulka njema za kweli. Mahali hasa pa kusema kweli ndipo pale panapohatarisha uhai au mali au heshima ya mtu. Kuhusu habari hii mafunzo ya Mungu ndiyo haya:

فَاجْتَنِبُوا الرِّجْسَ مِنَ الْأَوْثَانِ وَاجْتَنِبُوا قَوْلَ الزُّورِ ﴿٣١﴾ [1]

وَلَا يَأْبَ الشُّهَدَاءُ إِذَا مَا دُعُوا ۚ [2]

وَلَا تَكْتُمُوا الشَّهَادَةَ ۚ وَمَنْ يَكْتُمْهَا فَإِنَّهُ آثِمٌ قَلْبُهُ ۗ [3]

وَإِذَا قُلْتُمْ فَاعْدِلُوا وَلَوْ كَانَ ذَا قُرْبَىٰ ۖ [4]

---

[1] Al-Hajj, 22:31

[2] Al-Baqarah, 2:283

[3] Al-Baqarah, 2:284

[4] Al-An‘aam, 6:153

كُوْنُوْا قَوّٰمِيْنَ بِالْقِسْطِ شُهَدَآءَ لِلّٰهِ وَلَوْ عَلٰٓى اَنْفُسِكُمْ اَوِ الْوَالِدَيْنِ وَالْاَقْرَبِيْنَ ۚ [1]

وَلَا يَجْرِمَنَّكُمْ شَنَاٰنُ قَوْمٍ عَلٰٓى اَلَّا تَعْدِلُوْا ۗ [2]

وَالصّٰدِقِيْنَ وَالصّٰدِقٰتِ [3]

وَتَوَاصَوْا بِالْحَقِّ ۙ وَتَوَاصَوْا بِالصَّبْرِ ۝٣ [4]

لَا يَشْهَدُوْنَ الزُّوْرَ ۙ [5]

Tafsiri: Jiepusheni na kuabudu masanamu na kusema uwongo, yaani uwongo pia ni sanamu, na anayeutegemea huacha kumtegemea Mungu; kwa hiyo mwongo hupoteza Mungu pia. Tana Amesema, mnapoitwa kutoa ushahidi wa kweli, msikatae wala msifiche ushuhuda wa kweli; na aufichaye, moyo wake hutenda dhambi. Na msemapo, tamkeni iliyo kweli tupu na adili, hata kama mkitoa ushahidi kumhusu jamaa wa karibu. Imarikeni juu ya haki na adili. Inawapasa kila ushuhuda wenu uwe kwa ajili ya Mungu. Msiseme uwongo hata kama uhai wenu unaingia hatarini au wazazi wenu na jamaa zenu wa karibu, kama vile mwana wenu, wanapata madhara. Uadui wa watu fulani usiwazuieni kutoa ushahidi wa kweli. Wanaume na wanawake wasemao kweli

[1] An-Nisaa, 4:136

[2] Al-Maaidah, 5:9

[3] Al-Ahzaab, 33:36

[4] Al-‘Asr, 103:4

[5] Al-Furqaan, 25:73

watapata ujira mkubwa. Wanayo tabia ya kuwasihi wengine pia kusema kweli na hawakai katika vikao vya waongo.

## SUBIRA

Kati ya mambo yaliyo tabia ya asili ya binadamu kuna subira pia

anayotakiwa kuonyesha katika misiba, maradhi na shida ambazo huzipata kila mara. Mtu huonyesha subira baada ya kupiga kelele nyingi na kuomboleza sana. Lakini tambueni kwamba subira hiyo siyo khulka njema bali ni hali ya asili tu ya mtu inayodhihirika yenyewe baada ya mtu kuchoka. Yaani ni tabia ya mtu kulia na kupiga makelele wakati wa msiba na taabu na kisha hutulia baada ya kuchoka na kufikia kikomo cha kuomboleza. Basi hali hizo zote mbili ni tabia za asili wala siyo khulka njema kabisa. Bali kuhusu hali hii khulka yenyewe ni kwamba ikiwa kitu kinapotea, mtu asilalamike kwa kujua kwamba hicho kilikuwa ni amana ya Mungu nasi twaridhika sawa na radhi yake ya kukichukua. Kuhusu khulka hii Mwenyezi Mungu Anatufundisha ndani ya Kurani Tukufu hivi:

وَلَنَبْلُوَنَّكُمْ بِشَيْءٍ مِّنَ الْخَوْفِ وَالْجُوْعِ وَنَقْصٍ مِّنَ الْاَمْوَالِ
وَالْاَنْفُسِ وَالثَّمَرٰتِ ۗ وَبَشِّرِ الصّٰبِرِيْنَ ۝١٥٦ الَّذِيْنَ اِذَآ اَصَابَتْهُمْ مُّصِيْبَةٌ ۙ
قَالُوْٓا اِنَّا لِلّٰهِ وَاِنَّآ اِلَيْهِ رٰجِعُوْنَ ۝١٥٧ اُولٰۤىِٕكَ عَلَيْهِمْ صَلَوٰتٌ مِّنْ رَّبِّهِمْ

وَرَحۡمَةٞۖ وَأُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلۡمُهۡتَدُونَ ١٥٨ [1]

Yaani, Enyi mlioamini, tutaendelea kuwajaribuni kwa njia hii: Pengine mtafikiwa na hali ya kutisha mno; pengine mtapatwa na njaa na umaskini; pengine mtapata hasara katika mali; pengine uhai wenu utaingia hatarini; pengine juhudi zenu zitapotea bure bila kuleta matokeo yaliyotazamiwa; pengine wazao wenu wapenzi watakufa. Basi ni habari njema kwa wale wanaosibiwa na shida hizo ambao husema: Sisi ni wa Mungu na amana Zake na milki Zake, na ni haki kwamba mwenye amana achukue amana zake. Hao ndio watu wapatao rehema za Mungu na hao ndio walioshika njia ya Mola.

Ilmuradi, khulka hiyo huitwa subira na kuridhika na radhi ya Mungu. Na khulka hii pia huitwa adili, kwani Mungu sikuzote Hutenda sawa na matakwa ya mtu na kutekeleza maelfu ya mambo jinsi apendavyo binadamu na kumpa neema zisizohesabika, basi siyo adili mtu kwenda kombo na kutokuridhika juu ya radhi ya Mungu au kulalamika au kuachana na dini na kupotea njia ikiwa Mungu Naye wakati mwingine Alimtaka mtu kuridhika na radhi Yake!

## KUWAHURUMIA VIUMBE

Na miongoni mwa mambo yaliyomo katika tabia ya asili ya mtu ni jazba ya kuwahurumia viumbe.

---

[1] Al-Baqarah, 2:156-158

Wafuasi wa kila dini huwa na jazba ya kuwahurumia washiriki wenzao, na wengi kwa sababu ya jazba hii ya tabia ya asili huwahi kuwadhulumu watu wengi kwa kuwahurumia wafuasi wa dini yao, kana kwamba hao wengine sio wanadamu. Hali kama hiyo haiwezi kuitwa khulka. Bali hiyo ni jazba ya tabia ya asili ambayo ikifikiriwa kwa makini itaonekana ipo katika kunguru na ndege wengine pia. Kunguru mmoja akifa, maelfu ya kunguru wanakusanyika. Kwa hivyo, tabia hii ya asili itaingia katika khulka njema iitwayo Muwasaat kwa Kiarabu na Hamdardi kwa Kiajemi ikiwa huruma hii itaonyeshwa kiadili katika mahali panapofaa. Mwenyezi Mungu Mtukufu Akiashiria kwenye habari hii Anasema ndani ya Kurani Tukufu:

تَعَاوَنُوا عَلَى الْبِرِّ وَالتَّقْوَىٰ ۖ وَلَا تَعَاوَنُوا عَلَى الْإِثْمِ وَالْعُدْوَانِ ۚ [1]

وَلَا تَهِنُوا فِي ابْتِغَاءِ الْقَوْمِ ۖ [2]

وَلَا تَكُن لِّلْخَائِنِينَ خَصِيمًا ﴿١٠٦﴾ [3]

وَلَا تُجَادِلْ عَنِ الَّذِينَ يَخْتَانُونَ أَنفُسَهُمْ ۚ إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ مَن كَانَ خَوَّانًا أَثِيمًا ﴿١٠٨﴾ [4]

Yaani, kuwahurumia na kuwasaidia watu wa taifa lenu kwapaswa kutekelezwe katika mambo mema peke yake na wala siyo katika dhuluma na kupita

---

[1] Al-Maaidah, 5:3

[2] An-Nisaa, 4:105

[3] An-Nisaa, 4:106

[4] An-Nisaa, 4:108

kiasi. Jishughulisheni kwa jazba kuwahurumia washiriki wa dini yenu, msichoke wala msiwe watetezi wa wafanyao hiyana, wasioacha kuhini. Mungu Hawapendi wahaini.

## KUTAFUTA DHATI TUKUFU

Miongoni mwa tabia ya asili ya binadamu mojawapo ni kumtafuta Mtukufu Aliye juu ambaye mtu anayo rohoni mwake mapenzi yanayomvutia kwake. Na athari ya kumtafuta huanza kuhisika tangu mtoto atokapo tumboni mwa mamake. Kwani mara baada ya kuzaliwa, sifa ya kiroho anayoonyesha mtoto ni kumwelekea mama yake mzazi na kumpenda. Kisha kadiri hisia zake zinavyokua, mapenzi hayo yaliyofichikana huanza kufunuka zaidi hata kwamba mtoto haoni raha popote pale isipokuwa mapajani mwa mama yake ambapo hupata raha kamili. Akitengwa na mama yake na kupelekwa mbali naye, maisha yake huwa machungu, na hata kama neema zilundikwe mbele yake, hataona raha ya kweli wala hatapata utulivu ila mapajani mwa mama yake. Sasa mvutano huu wa mapenzi kwa ajili ya mama yake ni kitu gani hasa?

Kwa kweli mvutano huo ndio ule uliowekwa katikatabia ya asili ya mtoto kwa ajili ya Mwabudiwa wa kweli; bali uhusiano wowote wa upendo anaokuwa nao binadamu na jazba ya mapenzi kwa kitu chochote ndiyo kwa hakika mvutano huo huo

kwa Dhati Tukufu. Kana kwamba mtu anamtafuta Yeye lakini kasahau jina lake, kwa hiyo humtafuta katika vitu vingine kwa kuvishika-shika. Ilimuradi, kupenda mali au watoto au mke au kupendezwa na sauti nyororo ya wimbo kwa kweli ni kumtafuta Mpendwa yule aliyepotea. Na kwa kuwa mtu hawezi kumwona kwa macho yake Yule Aliyefichikana kama moto katika kila kitu, wala hawezi kumgundua kwa akili yake isiyokamilika, hivyo mtu amefanya makosa makubwa makubwa kuhusu maarifa yake na kwa sababu ya makosa yake akawapa wengine haki Yake. Mungu Ametoa mfano bora sana ndani ya Kurani Tukufu kwamba dunia hii ni kama jumba la kioo ambalo sakafu yake imetengenezwa na vioo safi mno na kisha chini ya vioo hivyo yamewekwa maji yanayopita kwa kasi. Hapo mtu anapoviona vioo hivyo hudhani ni maji tu matupu na huwa anaogopa kukanyaga vioo jinsi aogopavyo kuingia katika maji, ilhali maji yako chini na juu viko vioo tu. Hivyo basi nyota na sayari hizi kubwa kubwa kama vile jua na mwezi n.k. ndivyo vioo hivyo vinavyoabudiwa kwa kukosea, na ukweli ni kwamba chini ya hizo Nguvu kubwa Tukufu inafanya kazi inayopita kama maji chini ya pazia ya vioo. Waabuduo viumbe wamekosea kuinasibisha kwa vioo hivyo ile kazi inayofanywa na Nguvu iliyo nyuma yake. Na hayo ndiyo maelezo halisi ya aya hii ya Kurani Tukufu:

إِنَّهُۥ صَرۡحٞ مُّمَرَّدٞ مِّن قَوَارِيرَۗ [1]

Ilmuradi, kwa kuwa dhati ya Mungu, ingawaje inang'aa mno lakini tena imefichikana ajabu, hivyo ili kumtafuta, mfumo huu wa kiwiliwili tunaoona hautoshi. Na ndiyo sababu walioutegemea mfumo huu na kuuchunguza utaratibu wake uliokamilika na kuimarika, na wakawa mahiri mno katika elimu ya Nyota na Fizikia na Falsafa kana kwamba walijipenyeza katika ardhi na mbingu, lakini hata hivyo hawakuweza kuepukana na shaka na giza; na wengi wao wakaangukia katika makosa ya aina aina na wakapotea njia. Kama waliwaza kumhusu Mwumbaji, ni kiasi hiki tu kwamba kwa kushuhudia mfumo huu uliokamilika wakatiliwa moyoni kwamba bila shaka anapaswa kuwepo Mwumbaji wa silsila hii iliyojaa hekima. Lakini ni dhahiri kwamba wazo lao hili ni pungufu na elimu hii ina pengo, kwani kauli hii kwamba kuna haja ya Mungu haiwezi kuwa sawa na kusema kwamba Mungu kweli Yupo. Ilmuradi, elimu yao ilikuwa ya kukisia tu isiyotuliza moyo wala haiondolei mbali shaka. Wala hicho sicho kikombe kiwezacho kuondoa kiu ya maarifa kamili iliyotiwa katika tabia ya asili ya mtu; bali maarifa hayo mapungufu ni hatari; kwani ni kelele nyingi lakini matokeo hamna.

[1] An-Naml, 27:45

Ndiyo kusema maadamu Mungu Hajidhihirishi kuwepo Kwake kwa kuzungumza jinsi alivyojidhihirisha kwa Neno Lake, kushuhudia vitendo Vyake peke yake hakutulizi. Kwa mfano, kama tukiona chumba fulani cha ajabu ambacho kimefungwa kutoka ndani, mara tutawaza kuna mtu mle ndani aliyekifunga, kwani haiwezekani kukifunga ndani kutoka nje. Lakini kama baada ya kumwita aliye ndani kwa muda fulani bali kwa miaka, hatusikii sauti ya mtu yeyote aliyemo humo, tutabadilisha rai yetu kwamba kuna mtu ndani aliyekifunga, bali tutafikiri kwamba mtu fulani kutoka nje amekifunga kwa maarifa. Hiyo ndiyo hali ya wataalamu wa falsafa waliomalizia maarifa yao juu ya kushuhudia tu. Hili ni kosa kubwa kumhesabu Mungu kama mfu ambaye kumfukua ndiyo kazi ya mtu. Kama Mungu ndiye yule aliyejulikana kwa maarifa ya mtu, hapo matamanio yetu kumhusu Yeye ni bure. Bali Mungu ndiye Yule aliyewaita watu kwa kudumu na tangu azali kwa kusema MIMI NIPO. Ni kukosa adabu kabisa kufikiri kwamba ni hisani ya mtu juu ya Mungu kwa kumgundua Yeye, na kama si wataalamu wa falsafa, Mungu asingejulikana kamwe. Na kusema kwamba Mungu anawezaje kutamka kwani anao ulimi? Ndiyo kujasiri. Je, Hakuumba nyota na sayari na ardhi bila mikono? Je, Hauoni ulimwengu mzima pasipo macho? Je, Hasikii sauti zetu bila kuwa na masikio ya kiwiliwili? Je, basi haikuwa lazima aseme pia hivyo? Pia si sawa kusema

kwamba Mungu alizungumza zamani tu, sasa hasemi. Hatupigi muhuri juu ya kusema Kwake katika zama zozote. Bila shaka Yeye yuko tayari kuwatajirisha na chemchemi ya ufunuo kwa watafutao hata sasa, kama alivyofanya hapo kabla. Na hata sasa milango ya neema Zake iko wazi kama ilivyokuwa wazi hapo zamani. Naam, kwa sababu ya sheria kukamilika hakuna haja tena ya sheria zozote zingine, na utume na unabii pia uliofikia kikomo chake katika dhati ya Mtume wetu[saw] umekamilika.

## HEKIMA YA KUDHIHIRIKA KWA MTUME[saw] UARABUNI

Mwanga huu wa mwisho kudhihirika Uarabuni pia kuna hekima. Wana wa Ismail ndilo taifa lililotengwa na Wana wa Israeli kupelekwa katika jangwa la Parani. Farani (Parani) kwa Kiarabu maana yake ni wakimbizi wawili. Hivyo, wale ambao Nabii Ibrahimu[as] aliwatenga na Wana wa Israeli, hawakuwa na sehemu katika sheria ya Torati, jinsi ilivyonenwa kwamba hawatapata sehemu pamoja na Isihaka. Basi waliachwa na jamaa zao wa karibu, nao walikuwa hawana jamaa wowote wengine. Katika nchi zingine, zilionekana desturi na amri za ibada kidogo kidogo, jambo linaloonyesha walipata mafunzo ya manabii; lakini Bara Arabu peke yake halikujua mafunzo hayo na lilikuwa nyuma kuliko dunia nzima. Kwa hiyo, zamu yake ikaja mwishowe, na Unabii wake

ukawa kwa watu wote ili nchi zingine zibarikiwe mara ya tena na liondolewe kosa lililokwisha fanyika. Basi tungoje kitabu kipi baada ya hiki kilichokamilika ambacho kimeshika kazi yote ya kumrekebisha binadamu, wala hakihusikani na taifa moja tu kama vitabu vya zamani, bali kilitaka kusuluhisha mataifa yote na kueleza madaraja yote ya ulezi wa binadamu? Kiliwafunza washenzi adabu za kibinadamu na kisha kuwafundisha khulka bora.

## HISANI YA KURANI TUKUFU KWA DUNIA NZIMA

Hii ni hisani ya Kurani peke yake kwamba imepambanua baina ya tabia za asili na khulka bora. Na baada ya kumtoa mtu katika hali ya tabia ya asili na kumfikisha kwenye jumba tukufu la khulka njema, haikutulia bali ile hatua iliyobakia ya kufikia hali ya kiroho ikafungulia milango yake ya maarifa matakatifu. Si tu ikafungua milango hiyo, bali ikawafikisha malaki ya watu kwenye daraja hilo. Hivyo, basi, ikatoa mafunzo ya namna zote tatu kwa njia iliyo bora sana nilivyokwisha eleza hapo nyuma. Na kwa kuwa mafunzo yote yaliyo msingi wa mahitaji yote ya ulezi wa kidini yamekamilika katika Kurani Tukufu kwa hiyo ikatangaza:

اَلْيَوْمَ اَكْمَلْتُ لَكُمْ دِيْنَكُمْ وَاَتْمَمْتُ

عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ الْإِسْلَامَ دِينًا [1]

Yaani: Leo nimekamilisha dini yenu, na nimewakamilishieni neema yangu, nami nimewafurahieni dini ya Kiislamu, yaani upeo wa mwisho wa dini ndilo jambo linalopatikana katika muradi wa Islam, yaani kuwa kwa ajili ya Mungu peke yake na kujiokoa kwa njia ya kujitolea nafsi kuwa dhabihu wala si kwa njia nyingine iwayo yote, na kisha kutekeleza nia hiyo na kusudio hilo kwa vitendo. Hapo ndipo ukamilifu wote huishia. Basi Yule Mungu wasiyemtambua wataalamu wa falsafa, Kurani ikamtambulisha Huyo Mungu wa kweli. Kurani ikashika njia mbili za kumtambulisha Mungu: Kwanza, ile njia inayoimarisha akili ya mtu na kuing'arisha hata kwamba inagundua hoja za kiakili na inaepukana na kufanya makosa. Na pili ni njia ya roho nitakayoeleza hivi karibuni, in-sha-Allahu, nikijibu swali la tatu.

## HOJA ZA KUWEPO KWA MUNGU MWENYE ENZI

Haya, angalieni sasa jinsi Kurani Tukufu ilivyotoa hoja nzuri zisizo kifani kwa kuhakikisha kuwepo kwa Mungu. Inasema mahali fulani:

رَبُّنَا الَّذِي أَعْطَى كُلَّ شَيْءٍ خَلْقَهُ ثُمَّ هَدَى ﴿٥١﴾ [2]

---

[1] Al-Maaidah, 5:4

[2] Taa Haa, 20:51

Yaani, Mungu ndiye Yule aliyekipa kila kitu umbo sawa na hali yake,kisha akakionyesha njia ya kujipatia ukamilifu uliotakikana. Sasa kwa kuzingatia maana ya aya hii, tukiangalia umbo la vitu vyote tangu binadamu hadi wanyama wote wa baharini na nchi kavu bali na ndege pia, tutatambua uwezo wa Mungu kwamba kila kitu kimejaaliwa kiwiliwili sawa na hali yake. Wasomaji wenyewe watafakari juu ya hali hii, maana ni madhumuni iliyo pana sana.

Dalili ya pili ya kuwepo kwa Mungu iliyotolewa na Kurani Tukufu ni kwamba Mungu ndiye sababu ya sababu zote, kama isemavyo:

وَاَنَّ اِلٰى رَبِّكَ الْمُنْتَهٰىۙ﴿٤٣﴾ [1]

Yaani, mwisho wa yote ndio kwa Mola wako. Maelezo yake ni kwamba tukichunguza kwa makini, tutatambua kwamba ulimwengu mzima unafungamana na mfumo maalum wa sababu na matokeo yake. Na kwa sababu hiyo, elimu za aina mbalimbali zimepatikana duniani, kwani sehemu yoyote ya viumbe haiko nje ya mfumo huu. Baadhi ya vitu ni chanzo kwa baadhi ya vingine, na baadhi vingine ndiyo kama matawi. Na ni dhahiri kwamba sababu fulani itajitegemea sababu nyingine, na hiyo ya pili yategemea ile ya tatu n.k. Na haiwezekani kwamba, katika dunia hii yenye eneo maalum,

[1] An-Najm, 53:43

mnyororo wa sababu na matokeo usiishie popote. Hivyo, tutalazimika kukiri kwamba mnyororo huu unaishia kwenye sababu fulani ya mwisho. Basi yule ambaye mnyororo huu unaishia kwake ndiye Mungu. Fumbueni macho na kuangalia kwamba maneno machache ya aya hiyo hapo juu yanaeleza dalili hii inayosema kwamba mwisho wa silsila hii ndio hadi kwa Mola wako.Tena anatoa dalili nyingine juu ya kuwepo kwake Akisema:

لَا الشَّمْسُ يَنۢبَغِي لَهَآ أَن تُدْرِكَ الْقَمَرَ وَلَا الَّيْلُ
سَابِقُ النَّهَارِ ۚ وَكُلٌّ فِي فَلَكٍ يَسْبَحُونَ ۝٤١ [1]

Yaani, jua haliwezi kuufikia mwezi, wala usiku unaodhihirisha mwezi hauwezi kuutangulia mchana unaolidhihirisha jua. Yaani chochote katika hivyo hakiwezi kuvuka mipaka yake. Kama hakuna nyuma yake Yule anayesimamia hivyo vyote, mfumo huu utavunjika moja kwa moja. Dalili hii itawafaa wachunguzi wa nyota na sayari ambazo ni kubwa mno na tofauti kidogo tu ikitokea katika hizo, dunia nzima yaweza kuangamia kabisa. Ni uwezo wa Mungu kwamba hizo hazigongani wala hazibadilishi miendo yao hata kidogo wala hazijachakaa sawa na chembe wala haijaingia tofauti yoyote ndani ya hizo. Kama hakuna msimamizi, vipi mfumo huu mkubwa sana waendelea wenyewe tangu miaka na miaka?

[1] Yaa Siin, 36:41

Akiashiria kwenye hizo hekima, Mungu Mwenye Enzi Amesema mahali pengine:

أَفِي اللَّهِ شَكٌّ فَاطِرِ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ [1]

Yaani, mwafanyia Mwenyezi Mungu shaka Aliyeumba mbingu na ardhi hivyo.

Tena Anaeleza dalili nyingine kuhakikisha kuwepo kwake Akisema:

كُلُّ مَنْ عَلَيْهَا فَانٍ ﴿٢٧﴾ وَيَبْقَىٰ وَجْهُ رَبِّكَ ذُو الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ ﴿٢٨﴾ [2]

Yaani, kila kitu kinaelekea kumalizika, na Mungu peke Yake Ndiye atabaki Ambaye ni Mwenye jalali na heshima. Sasa, kwa mfano hata kama ardhi isagike tikitiki na sayari na nyota nazo zivunjike kabisa na zifutilike mbali, bali hata alama za vitu vyote pia zifutike, hapo pia akili inakubali na dhamiri iliyo safi inakiri kwamba baada ya kuangamia kila kitu, kitu kimoja kitabaki kisichoangamia wala kubadilika ile hali yake ya asili, na hicho ndicho Mungu Aliyeleta sababu za kuviangamiza vitu vyote lakini mwenyewe akabaki pale pale.

Kisha Anaeleza dalili nyingine ndani ya Kurani Tukufu kuhusu kuwepo kwake:

---

[1] Ibraahiim, 14:11

[2] Ar-Rahmaan, 55:27-28

اَلَسْتُ بِرَبِّكُمْ ۖ قَالُوْا بَلٰى ۚ [1]

Yaani, Nikaziuliza roho, Je Miye si Mola wenu? Zikasema, Naam. Katika aya hii Mwenyezi Mungu Ameeleza kimfano sifa za roho zilizowekwa katika tabia yake ya asili nayo ni kwamba Roho kitabia haiwezi kumkana Mungu. Wakanao hukana kwani sawa na mawazo yao hawapati dalili. Lakini hata hivyo wanakubali kwamba kila kiumbe kina mwumbaji wake. Hakuna mjinga duniani ambaye akiugua maradhi fulani anakazania tu kwamba hakuna kilichosababisha maradhi hayo. Kama ulimwengu usingefungamana na mfumo wa sababu na matokeo yake, isingewezekana kutabiri mapema kwamba tarehe fulani tufani itatokea au dhoruba kali itavuma au jua au mwezi utapatwa au mgonjwa atafariki saa fulani au hadi muda fulani maradhi hayo yataongezeka maradhi mengine fulani. Ingawaje mchunguzi huyo hakiri kuwepo kwa Mungu, lakini hata hivyo ameisha mkiri kwa namna fulani, kwani yeye naye anashughulika kutafuta sababu za matokeo, na huko ndiko kukiri kwa namna fulani ingawaje si kikamilifu. Isitoshe, kama mkana Mungu afanywe kuzirai kwa njia fulani hata kwamba kwa kutengeka na mawazo duni na shabaha zote za kidunia aje chini ya usimamizi wa Mungu moja kwa moja, hapo yeye mtu huyo atamkiri Mungu wala

---

[1] Al-A'raaf, 7:173

hatamkana jinsi ilivyohakikishwa na wataalamu waliofanya tajiriba ya jambo hili. Basi aya hiyo inaashiria kwenye hali kama hiyo ya mtu. Ndiyo kusema kumkana Mungu kunaishia kwenye maisha haya duni, waila tabia ya asili ya mtu inamkiri tu.

## SIFA ZA MWENYEZI MUNGU

Baada ya dalili za kuwepo kwa Mungu nilizoeleza kwa mfano mwapaswa kujua pia kwamba Mungu ambaye Kurani Tukufu inatuita kwake, sifa zake zilizoelezwa ndani ya Kurani Tukufu ni hizi:

هُوَ اللّٰهُ الَّذِىۡ لَاۤ اِلٰهَ اِلَّا هُوَ‌ۚ عٰلِمُ الۡغَيۡبِ وَالشَّهَادَةِ‌ۚ هُوَ الرَّحۡمٰنُ الرَّحِيۡمُ ﴿۲۳﴾ [1]

مٰلِكِ يَوۡمِ الدِّيۡنِؕ ﴿۴﴾ [2]

اَلۡمَلِكُ الۡقُدُّوۡسُ السَّلٰمُ الۡمُؤۡمِنُ الۡمُهَيۡمِنُ الۡعَزِيۡزُ الۡجَبَّارُ الۡمُتَكَبِّرُ‌ؕ [3]

هُوَ اللّٰهُ الۡخَالِقُ الۡبَارِئُ الۡمُصَوِّرُ لَهُ الۡاَسۡمَآءُ الۡحُسۡنٰى‌ؕ
يُسَبِّحُ لَهٗ مَا فِى السَّمٰوٰتِ وَالۡاَرۡضِ‌ۚ وَهُوَ الۡعَزِيۡزُ الۡحَكِيۡمُ ﴿۲۵﴾ع [4]

عَلٰى كُلِّ شَىۡءٍ قَدِيۡرٌ ﴿۱۴۹﴾ [5]

رَبِّ الۡعٰلَمِيۡنَۙ ﴿۲﴾ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِيۡمِۙ ﴿۳﴾ مٰلِكِ يَوۡمِ الدِّيۡنِؕ ﴿۴﴾ [6]

---

1 Al-Hashr, 59:23
2 Al-Faatihah, 1:4
3 Al-Hashr, 59:24
4 Al-Hashr, 59:25
5 Al-Baqarah, 2:21
6 Al-Faatihah, 1:2-4

أُجِيبُ دَعْوَةَ الدَّاعِ إِذَا دَعَانِ[1]

الْحَيُّ الْقَيُّومُ[2]

قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ ۞ اللَّهُ الصَّمَدُ ۞ لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ ۞ وَلَمْ يَكُن لَّهُ كُفُوًا أَحَدٌ ۞[3]

Yaani: Mungu ambaye ni Mmoja asiye na mshirika wake, hakuna apasaye kuabudiwa na kutiiwa isipokuwa Yeye. Hayo yamesemwa kwani kama angekuwa na mshirika, hapo pengine nguvu Yake ingeshindwa mbele ya nguvu ya adui Yake, na hapo ndipo Uungu utadumu katika hatari. Na usemi huu kwamba hakuna apasaye kuabudiwa, unamaanisha kwamba Mungu Huyo ni mkamilifu hivi kwamba sifa Zake na uzuri Wake vimekamilika na kutukuka kiasi hiki kwamba watu wakitaka kumchagua Mungu katika ulimwengu kwa kuangalia sifa njema zilizokamilika au kwa kuwaza moyoni sifa bora bora, hapo mtukufu kabisa ambaye zaidi yake haiwezekani kupata mwingine ndiye Mungu ambaye kumshirikisha na chochote ni dhuluma. Kisha Amesema, Yu mjuzi wa mambo ya ghaibu; yaani anajijua peke yake wala hakuna awezaye kumzingira. Twaweza kuangalia jua na mwezi na kila kilichoumbwa, lakini kumwangalia Mungu hatuwezi katu. Tena Amesema, Yu mjuzi wa dhahiri. Yaani

[1] Al-Baqarah, 2:187

[2] Al-Baqarah, 2:256

[3] Al-Ikhlaas, 112:2-5

chochote hakifichikani kwake. Haijuzu Ajiite Mungu kisha Asiwe na ujuzi wa vitu. Bali Yeye Huangalia kila chembe ya ulimwengu, lakini mtu hawezi. Anajua lini atauvunja mfumo huu na kuleta kiyama wala hamna minghairi ya Yeye ajuaye lini itakuwa hivyo. Basi ndiye Yeye Azijuaye nyakati hizo. Kisha kasema Yu Rahmani, yaani kabla hawajaumbwa viumbe na kutenda matendo, Yeye huwatengenezea vitu vya kuwastarehesha kwa hisani yake kama vile alivyoumba jua, ardhi na vitu vingine vyote kabla hatujaumbwa na kutenda matendo ili kustahili kupewa neema hizo. Upaji huu huitwa Urahmani katika Kitabu cha Mungu, na kwa hiyo Mungu huitwa Rahmani. Tena kasema Yu Rahim, yaani hulipa malipo bora sana ya matendo mema wala hapotezi bure juhudi za mtu. Basi kwa sababu hii akaitwa Rahim, na sifa hii yaitwa Urahimu. Tena Yu "Maliki Yaumiddin", yaani malipo ya kila mtu huyatoa Yeye Mwenyewe. Hakuweka naibu Wake aliyepewa ufalme wa mbingu na ardhi na mwenyewe kakaa kando asifanye lolote, bali huyo naibu ndiye atoaye malipo na adhabu hapa au baadaye. Kisha asema: Al-Malik Al-Quddus, yaani Yu Mfalme aliyetukuka asiyehusiana na aibu yoyote. Ni dhahiri kwamba ufalme wa binadamu hauepukani na kasoro. Kwa mfano ikiwa raia wote wanahamia nchi nyingine, hapo ufalme hauwezi kubaki. Au kwa mfano, kama raia wakisibiwa na njaa, serikali itapata kodi kutoka kwa nani? Na kama raia wakianza kuhojiana na

mfalme ati umetuzidi katika nini, hapo yeye atawahakikishia ubora wake upi? Basi, ufalme wa Mungu sio hivyo, bali Yeye aweza kuwaangamiza wote na kuwaumba viumbe wengine. Kama asingekuwa mwumbaji na mwenye uwezo hivyo, asingeweza kuendesha ufalme wake pasipo dhuluma, kwani baada ya kuwasamehe watu na kuwaokoa, angeletaje dunia nyingine? Na kama angewanyima msamaha na wokovu baada ya kuwapatia kwanza, hapo Uungu wake ungepata ila na Mungu angekuwa Mfalme mwenye doa baya jinsi wafalme wa dunia wanavyokuwa na madoa mabaya ambao huwaundia wengine sheria, hukasirika juu ya mambo madogo madogo na wanapoona hakuna njia nyingine ya kunufaika isipokuwa kudhulumu, basi hapo huhalalisha dhuluma. Kwa mfano, sheria ya kifalme inahalalisha kuwatupa abiria wa mashua moja katika maangamio kwa ajili ya kuoka meli; lakini Mungu hapaswi kushurutika hivyo. Basi, kama Mungu hangekuwa mweza mkamilifu na mwenye kuumba pasipo chochote, angefanya mabavu kama wafalme wanyonge au katika kuwa mwadilifu angejiondolea Uungu wake; bali jahazi la Mungu linapita kwa nguvu zote juu ya msingi wa adili.

Kisha Yu As-Salaam, yaani ameepukana na kila aibu na misiba na shida, bali Yeye hutoa usalama. Muradi wake pia ni dhahiri; kwani kama Yeye mwenyewe angesibiwa na misiba, na kuuawa na watu na

kushindwa katika shabaha Zake, hapo kwa kuona mfano Wake mbovu, nyoyo zingewezaje kutulia kwamba Atatuokoa sisi katika taabu! Ndiyo maana, Mwenyezi Mungu asema kuhusu miungu ya bandia:

إِنَّ الَّذِينَ تَدْعُونَ مِن دُونِ اللَّهِ لَن يَخْلُقُوا ذُبَابًا وَلَوِ اجْتَمَعُوا لَهُ ۖ وَإِن
يَسْلُبْهُمُ الذُّبَابُ شَيْئًا لَّا يَسْتَنقِذُوهُ مِنْهُ ۚ ضَعُفَ الطَّالِبُ وَالْمَطْلُوبُ ﴿٧٤﴾
مَا قَدَرُوا اللَّهَ حَقَّ قَدْرِهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَقَوِيٌّ عَزِيزٌ ﴿٧٥﴾ [1]

Yaani, wale mnaowafanya kuwa miungu, wangalitaka kuumba hata nzi mmoja wasingeweza hata kama wangesaidiana wao kwa wao; bali nzi akiwanyang'anya kitu hawawezi kumpokonya. Hao wanaowaabudu wana fahamu ndogo; je miungu huwa hivyo? Mungu Ndiye Yule aliye na nguvu mno kuliko wenye nguvu, naye Yu Mshindi juu ya wote, hakuna awezaye kumkamata au kumwua. Wanaoangukia katika makosa ya aina hiyo, hawatambui heshima ya Mungu wala hawajui Mungu Hupaswa kuwa namna gani. Kisha amesema kwamba Mungu hutoa amani na hutoa dalili juu ya ukamilifu wake na Umoja wake. Hii inadokeza kwamba mwenye kumwamini Mungu wa kweli hawezi kufedheheka mbele ya watu wala mbele ya Mungu, kwani anayo dalili madhubuti. Lakini aaminiye mungu wa bandia huwa katika shida kubwa; na badala ya kuleta hoja, husema kuhusu kila

[1] Al-Hajj, 22:74-75

jambo la kipuuzi eti ni siri, ili asichekwe, na hujaribu kuficha makosa yaliyokwisha hakikishwa tayari.

Kisha amesema: الْمُهَيْمِنُ الْعَزِيْزُ الْجَبَّارُ الْمُتَكَبِّرُ (Al-Muhaimin, Al-Aziz, Al-Jabbaar, Al-Mutakabbir). Yaani, Yu mlinzi wa wote, mshindi juu ya wote, na mwenye kurekebisha kilichoharibika, tena Yu Mkwasi. Kisha kasema: هُوَ اللّٰهُ الْخَالِقُ الْبَارِئُ الْمُصَوِّرُ لَهُ الْاَسْمَآءُ الْحُسْنٰى

Yaani, Yu Mwumbaji wa miili na pia mwumbaji wa roho, mfanyaji wa sura katika tumbo la uzazi; sifa zote njema zinazoweza kuwazwa ni zake. Anaongeza kusema: يُسَبِّحُ لَهٗ مَا فِى السَّمٰوٰتِ وَ الْاَرْضِ ۚ وَ هُوَ الْعَزِيْزُ الْحَكِيْمُ ﴿۲۵﴾

Watu wa mbinguni na pia watu wa ardhini hutukuza jina lake. Katika aya hii Amedokeza kwamba sayari zinakaliwa na watu ambao nao wanafuata maagizo kutoka kwa Mungu. Kisha amesema: عَلٰى كُلِّ شَىْءٍ قَدِيْرٌ ﴿۱۴۹﴾

Yaani Mungu ni Mweza sana. Hapo wenye kumwabudu wametulizwa, kwani kama Mungu angekuwa mnyonge asiye na uwezo, wasingekuwa na matamanio kwake. Kisha anasema tena:

رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ ﴿۲﴾ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ﴿۳﴾ مٰلِكِ يَوْمِ الدِّيْنِ ﴿۴﴾

اُجِيْبُ دَعْوَةَ الدَّاعِ اِذَا دَعَانِ

Yaani, Mungu ndiye Yule aliye Mlezi wa ulimwengu wote. Yu mwingi wa rehema, mwingi wa ukarimu; Mmiliki wa siku ya malipo, ambaye hakumpa yeyote madaraka hayo. Husikiliza na kuitikia mwito wa mwitaji, yaani hupokea maombi. Kasema tena

Al-Hayyu, Al-Qayyumu, yaani mzima wa milele, uhai wa kila uhai na tegemeo la kuwepo kwa wote. Hii imesemwa kwani kama Yeye si wa milele, hapo daima watu watahofia isije Yeye akajifia kabla yetu. Tena kasema, Yu Mungu aliye Mmoja, hakuzaa wala hakuzaliwa wala hakuna aliye sawa naye.

Kumbukeni kwamba kuamini Umoja wa Mwenyezi Mungu sawasawa bila kuongeza humo kitu wala kupunguza ndiyo adili anayotenda binadamu kwa Mmiliki wa kweli. Hayo ndiyo mafunzo ya kikhulka yaliyoandikwa kutoka katika mafunzo ya Kurani Tukufu. Kanuni iliyomo humo ni kwamba Mungu amehifadhi khulka zote katika mazidio na vipunguo. Kila tabia inayoelekeza kwenye hali ya wasitani ndiyo inazalisha khulka njema. Kutambua mahali na wakati wa kufaa kwa jambo fulani ndiyo wasitani wake. Kwa mfano, kama mkulima anapanda mbegu kabla ya wakati au baada ya kupita wakati, hapo yeye huachana na wasitani. Wema, haki na hekima viko katika wasitani, na wasitani uko katika kutambua wakati ufaao. Au tuseme kwamba haki ni kitu ambacho huwa katikati ya batili mbili zinazotazamana. Na hakuna shaka katika hili kwamba kufungamana na mahali pafaapo kwamweka mtu katika wasitani. Na hali ya wasitani kuhusu kumtambua Mungu ni kwamba wakati wa kueleza sifa za Mungu, mtu asielekee kukana moja kwa moja sifa za Mungu wala asimfananishe Mungu na vitu vya

kiwiliwili. Hii ndiyo njia iliyoshikwa na Kurani Tukufu kwa kueleza sifa za Mungu. Basi yasema vile vile kwamba Mungu huona, husikia, hujua, husema na hunena, na pia yasema kwa kumwepusha na kufananishwa na viumbe kwamba:

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ [1]

فَلَا تَضْرِبُوا لِلَّهِ الْأَمْثَالَ [2]

Yaani, hakuna anayeshirikiana na Mungu katika dhati au sifa, kwa hiyo msimtolee mifano katika viumbe. Ndiyo kusema kwamba kumweka Mungu katikati ya Tashbihi na Tanzihi ndio wasitani kuhusu dhati yake, yaani kueleza sifa zake zinazoonekana katika viumbe kidhahiri lakini kutomfananisha na chochote. Ilmuradi mafunzo yote ya Islam ndiyo ya wasitani. Suratul-Faatiha pia hufundisha wasitani, kwani Mungu anasema katika hiyo sura:

غَيْرِ الْمَغْضُوبِ عَلَيْهِمْ وَلَا الضَّالِّينَ [3]

Walioghadhibikiwa ndio wale ambao dhidi ya Mungu wanatumia uwezo wao wa kughadhibika sana na wakawa kama nduli; na wanaopotea ndio wale wanaokuwa kama wanyama. Basi njia ya wasitani ndiyo iliyoelezwa kwa kusema 'Walioneemeshwa'.

---

[1] Ash-Shu'araa, 26:12

[2] An-Nahl, 16:75

[3] Al-Faatihah, 1:7

Ilmuradi kwa ajili ya umati huu uliobarikiwa kuna njia ya wasitani. Ndani ya Torati Mungu alitia mkazo katika kisasi, na ndani ya Injili akakazania msamaha; lakini ummati huu ukafundishwa kuangalia mahali pafaapo na kutumia wasitani. Kwa hiyo Mungu anasema:

وَكَذٰلِكَ جَعَلْنٰكُمْ اُمَّةً وَّسَطًا [1]

Yaani Tumewafanyeni kushika hali ya wasitani na tumewapeni mafunzo ya wasitani. Basi wamebarikiwa wanaoshika njia ya kati: [2] خَيْرُ الْاُمُوْرِ اَوْسَطُهَا Jambo la wasitani ndilo bora.

## HALI ZA ROHO

Sehemu ya tatu: Ni nini hali za kiroho? Ikumbukwe, nimekwisha eleza mapema kwamba sawa na mwongozo wa Kurani Tukufu chanzo cha Hali za Roho ni Nafsi Mutmainnah, yaani Nafsi iliyotulia, ambayo humfikisha mtu kutoka katika hali ya Khulka Njema hadi kuungana na Mungu, kama asemavyo Mwenyezi Mungu:

يٰاَيَّتُهَا النَّفْسُ الْمُطْمَئِنَّةُ ۞ ارْجِعِيْۤ اِلٰى رَبِّكِ رَاضِيَةً مَّرْضِيَّةً ۞
فَادْخُلِيْ فِيْ عِبٰدِيْ ۞ وَادْخُلِيْ جَنَّتِيْ ۞ [3]

---

[1] Al-Baqarah, 2:144

[2] Shuubul Imani wa Beheki, Mlango wa 42, Babul Iktisadi fin-nafaka.

[3] Al-Fajr, 89:28-31

Yaani, Ewe Nafsi uliyetulia, rudi kwa Mola wako hali umemridhia, naye Amekuridhia. Basi ingia katika watumishi Wangu, na ingia katika Pepo Yangu (89:28-31).

Inafaa hapa nifafanue zaidi aya hii ili kueleza hali za roho. Zingatieni, basi, kwamba hali bora zaidi ya roho katika maisha haya ya kidunia ni kwamba mtu aone raha ndani ya Mungu, na utulivu wake na furaha yake viwe katika Mungu. Hii ndiyo hali inayoitwa kwa maneno mengine maisha ya kipeponi. Katika hali hii mtu hupata Pepo hapa hapa kama malipo ya ikhlasi yake na ukweli na uaminifu wake. Wengine hungojea Pepo iliyoahidiwa, lakini yeye huingia katika Pepo iliyopo tayari. Katika daraja hili mtu hutambua kwamba mzigo wa kufanya ibada aliotwishwa, kwa kweli ni chakula kinachostawisha roho yake ambacho maisha ya roho yanakitegemea sana na natija yake haiahirishwi mpaka maisha ya baadaye. Hapo lawama zote za Nafsi Lawwaamah inayomlaumu mtu juu ya maisha yake maovu na hata hivyo inashindwa kumzindua mtu kupenda mema na kuchukia maovu kikwelikweli wala haimwezeshi kudumu katika wema, zinageuka kwa harakati hiyo iliyo chanzo cha ustawi wa Nafsi Mutmainnah (Nafsi iliyotulia). Katika daraja hili wakati unawadia kwa mtu kupata ufaulu kamili na tamaa za nafsi huanza zenyewe kupoa, na upepo baridi wenye kumpa nguvu huanza kuvuma juu ya roho na kumfanya mtu ajute juu ya

udhaifu wake wa zamani. Hapo tabia ya kibinadamu hupata mapinduzi makubwa na silika yake hubadilika moja kwa moja, na mtu huenda mbali na hali yake ya hapo kabla; hukoshwa na kusafishwa; na Mungu huyaandika kwa mkono wake mapenzi ya wema katika moyo wake, na kutupilia mbali uchafu wa maovu nje ya moyo wake kwa mkono wake mwenyewe. Jeshi zima la ukweli laingia katika ngome ya mji wake na buruji zote za tabia zatekwa na ukweli. Hapo haki inapata ushindi na batili inakimbia na kuacha silaha zake. Mkono wa Mungu huwa juu ya moyo wa mtu huyo naye hukanyaga kila hatua katika kivuli cha Mungu. Mwenyezi Mungu amedokeza habari hii katika aya zifuatazo:

أُولَٰئِكَ كَتَبَ فِي قُلُوبِهِمُ الْإِيمَانَ وَأَيَّدَهُمْ بِرُوحٍ مِنْهُ ۖ [1]

وَزَيَّنَهُ فِي قُلُوبِكُمْ وَكَرَّهَ إِلَيْكُمُ الْكُفْرَ وَالْفُسُوقَ وَالْعِصْيَانَ ۚ

أُولَٰئِكَ هُمُ الرَّاشِدُونَ ﴿٨﴾ فَضْلًا مِنَ اللَّهِ وَنِعْمَةً ۚ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٩﴾ [2]

جَاءَ الْحَقُّ وَزَهَقَ الْبَاطِلُ ۚ إِنَّ الْبَاطِلَ كَانَ زَهُوقًا ﴿٨١﴾ [3]

Yaani: Mwenyezi Mungu Ameiandika imani katika mioyo ya waaminio na kuwasaidia kwa Roho itokayo kwake. Enyi waaminio, Yeye ameipendezesha kwenu imani, na ameipamba mioyoni mwenu, na

[1] Al-Mujaadalah, 58:23

[2] Al-Hujuraat, 49:8-9

[3] Banii Israaiil, 17:82

amewafanyeni mchukie ukafiri na ufasiki na uasi. Na hayo yote yalisababishwa na fadhili na rehema za Mungu. Na ukweli umefika na uwongo umetoweka; hakika uwongo ndio wenye kutoweka, hauwezi kuukabili ukweli.

Ilmuradi, hizo zaashiria kwenye ile hali ya roho anayoipata mtu katika daraja la tatu. Na mtu hawezi kupata busara ya kweli mpaka ajipatie hali hiyo. Na kauli hii ya Mwenyezi Mungu kwamba 'Nimeiandika imani katika mioyo yao na kuwasaidia kwa Roho Takatifu', inadokeza kwamba mtu hawezi kupata utakaso wa kweli mpaka ajaaliwe msaada wa kimbinguni. Katika daraja la Nafsi Lawwaamah, mtu anatubu mara kwa mara na huanguka kila mara bali pengine anakata tamaa kujirekebisha na hudhania kwamba maradhi yake hayana tiba, na anabaki katika hali hii kwa muda; lakini muda wake unapotimia, mara wakati wa usiku au mchana nuru moja humshukia iliyo na nguvu ya kiungu na pale pale mabadiliko ya ajabu hutokea ndani yake. Mkono usioonekana unahisika ukifanya kazi kwa nguvu na mtu anashuhudia ulimwengu wa ajabu. Hapo mtu anatambua kweli Mungu Yupo; na nuru moja inaingia machoni ambayo haikuwapo hapo kabla.

Lakini tuitafuteje hiyo njia? Tuipateje hiyo Nuru? Tambueni, basi, kwamba katika dunia hii kila kitu kina sababu na kila mwendo una mwendeshaji, na kwa kupata kila elimu kuna njia iitwayo njia

iliyonyooka. Hakuna kiwacho chochote duniani kiwezacho kupatikana pasipo kuzifuata sheria zile zilizowekwa kwa kupata kitu hicho. Sheria ya ulimwengu inatuambia kwamba kwa kupata kitu chochote kuna njia iliyo sawa na bila kuifuata njia hiyo kitu hicho hakipatikani. Kwa mfano, kama tumo katika chumba chenye giza totoro na twataka mwanga wa jua, hapo njia iliyonyooka kupata mwanga huo ni kulifungua dirisha lililo upande wa jua, ndipo mara mwanga wa jua ukiingia utatuangaza. Basi, ni dhahiri kwamba lazima lipo dirisha fulani la kupata neema hasa za Mungu ambazo kweli zipo; na ipo njia maalum ya kujipatia hali ya kiroho iliyotukuka, nayo ni kutafuta njia iliyonyooka kwa mambo ya kiroho jinsi tunavyoendelea kutafuta njia iliyonyooka ya kufaulu katika mambo mengineyo. Lakini, je, njia hiyo ndiyo kujaribu kumpata Mungu kwa nguvu ya akili yetu peke yake na kwa mambo tuliyozusha sisi wenyewe? Je, kwa mantiki na falsafa yetu tu tunafunguliwa milango yake ile ambayo kufunguliwa kwake kunautegemea Mkono wake wenye nguvu? Tambueni kwa yakini kwamba hiyo si sawa kabisa. Hatuwezi kumpata Huyo Mzima wa milele, ambaye uhai wa kila kitu humtegemea Yeye, kwa njia ya mipango yetu pekee, bali kuhusu habari hii njia iliyonyooka ndiyo kwamba sisi tujitolee maisha yetu pamwe na uwezo wetu wote na nguvu zetu zote kwa

ajili yake na kisha tudumu katika maombi ili tumpate Mungu kwa njia ya Mungu Mwenyewe.

## DUA MOJA YA KUPENDEZA

Na dua yenye kupendeza zaidi inayotufunza mahali hasa pa kuomba na ambazo inatufunulia jazba ya kiroho ya tabia ya asili ndiyo dua ile aliyofundisha Mwenyezi Mungu katika Kitabu chake Kurani Tukufu yaani katika Sura Faatiha; nayo ndiyo hii:

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ۞ اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ ۞ [1]

Yaani: Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu, Mwumbaji na Msimamizi wa kila ulimwengu. الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ۞[2] (Ar-Rahman, Ar-Rahim): Ndiye Mungu ambaye kabla hatujatenda lolote hutuletea rehema zake, na baada ya kutenda pia hutupatia malipo kwa huruma yake. مٰلِكِ يَوْمِ الدِّيْنِ ۞[3] (Maaliki Yaumiddin); Ndiye Mungu aliye Mmiliki wa pekee wa siku ya malipo wala hakuna yeyote awaye aliyepewa usimamizi wa siku hiyo. اِيَّاكَ نَعْبُدُ وَ اِيَّاكَ نَسْتَعِيْنُ ۞[4] (Iyyaka Na‘budu, Wa Iyyaka Nastaiin): Ewe Mwenye sifa hizo zote, sisi twakuabudu Wewe tu na katika kila jambo twakuomba uwezo Wewe Peke Yako. Neno `sisi'

---

[1] Al-Faatihah, 1:1-2
[2] Al-Faatihah, 1:3
[3] Al-Faatihah, 1:4
[4] Al-Faatihah, 1:5

katika ombi hili linamaanisha kwamba nguvu zetu zote zinakuabudu na zinaanguka kwenye kizingiti chako. Kwani mtu kwa kulingana na nguvu zake za ndani ni kama jumuiya na ummati, na nguvu zote kumsujudia Mungu ndiyo hali inayoitwa Islam.

اِهۡدِنَا الصِّرَاطَ الۡمُسۡتَقِيۡمَ ۙ ٦ صِرَاطَ الَّذِيۡنَ اَنۡعَمۡتَ عَلَيۡهِمۡ ۙ [1]

Tuonyeshe njia yako iliyonyooka na kutuimarisha katika hiyo njia. Tuongoze kwenye njia ya wale uliowaneemesha waliopata fadhili zako na ukarimu wako.

غَيۡرِ الۡمَغۡضُوۡبِ عَلَيۡهِمۡ وَلَا الضَّآلِّيۡنَ ٧ [2]

Na tuepushe na njia za walioghadhibikiwa na wale wasioweza kukufikia na wakapotea njia. Amin, ufanye hivyo Ee Mungu.

Aye hizo zafahamisha kwamba neema za Mwenyezi Mungu huwashukia wale tu ambao kwa kutoa dhabihu ya maisha yao kwa Mungu na kujitolea dhati yao katika njia yake na kujipoteza katika radhi yake, wanashughulika katika maombi ili wapate yote yale wanayoweza kupata miongoni mwa neema za roho na ukaribu kwa Mungu na kuungana na kuongea naye. Kisha pamoja na kuomba wanafanya ibada kwa nguvu zao zote na vipawa vyao vyote, na

---

[1] Al-Faatihah, 1:6-7
[2] Al-Faatihah, 1:7

wanaepukana na dhambi na wanajitupa kwenye kizingiti cha Mungu, na wanajiepusha na maovu sawa na uwezo wao na wanakaa mbali sana na njia ya ghadhabu ya Mungu. Basi kwa kuwa wanamtafuta Mungu kwa uwezo wa hali ya juu na ukweli wa nia, humpata na kutoshelezwa na vikombe vya maarifa matakatifu ya Mungu Mwenye Enzi.

Uimara uliotajwa katika aya hii unaashiria kwenye jambo hili kwamba neema ya kweli ni ile inayofikisha hadi kwenye mahali ambapo ulimwengu wa roho hufungamana na uimara kamili. Na uimara kamili unamaanisha ile hali ya ukweli na uaminifu usioweza kudhurika na jaribio lolote; yaani mwungano usioweza kukatwa na panga lolote au kuchomwa na moto wowote au kudhurika na afa lolote liwalo. Vifo vya jamaa wa karibu visiweze kumtenga naye; kuondokewa na wapenzi kusiweze kuleta tofauti ndani yake; hofu ya kufedheheka isiweze kumtisha; na kuuawa kwa taabu za kutisha kusiweze kuogofya hata kidogo. Basi, mlango huu ndio mwembamba mno, na njia hii ni ngumu sana kupita. Lo, ngumu mno iliyoje! Ah!!

Kwenye jambo hilo hilo Mwenyezi Mungu anaashiria katika aya hizi:

قُلْ إِنْ كَانَ آبَاؤُكُمْ وَأَبْنَاؤُكُمْ وَإِخْوَانُكُمْ وَأَزْوَاجُكُمْ وَعَشِيرَتُكُمْ
وَأَمْوَالٌ اقْتَرَفْتُمُوهَا وَتِجَارَةٌ تَخْشَوْنَ كَسَادَهَا وَمَسٰكِنُ تَرْضَوْنَهَا أَحَبَّ

اِلَيۡكُمۡ مِّنَ اللّٰهِ وَرَسُوۡلِهٖ وَجِهَادٍ فِىۡ سَبِيۡلِهٖ فَتَرَبَّصُوۡا حَتّٰى يَاۡتِىَ اللّٰهُ بِاَمۡرِهٖ‌ ؕ
وَاللّٰهُ لَا يَهۡدِى الۡقَوۡمَ الۡفٰسِقِيۡنَ ﴿۲۴﴾ [1]

Yaani: Waambie, kama baba zenu na wana wenu, na ndugu zenu, na wake zenu na jamaa zenu na mali mlizochuma, na biashara mnazoogopa kusimama, na majumba mnayoyapenda ni vipenzi zaidi kwenu kuliko Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kufanya juhudi katika njia yake, basi ngojeni mpaka Mwenyezi Mungu Alete amri yake, na Mwenyezi Mungu Hawaongozi watu waasi.

Aya hizo zinadhihirisha bayana kwamba wanaopenda jamaa zao na mali zao kwa kuacha radhi ya Mungu ndio waovu machoni pa Mungu, nao hawana budi kuangamia kwani wamewatanguliza wengine mbele ya Mungu. Hili ndilo daraja la tatu ambapo mtu anakuwa pamoja na Mungu, na anakubali maelfu ya mabalaa kwa ajili Yake, na anaelekea kwa Mungu kwa ukweli wa moyo na ikhlasi hata kwamba habakiwi na yeyote mwingine isipokuwa Mungu tu, kana kwamba wote wengine wamekufa. Basi, ukweli wenyewe ni kwamba Mungu haonekani isipokuwa tunapokufa. Siku ya Mungu kudhihirika ndiyo ile ambapo maisha yetu ya kiwiliwili hupatwa na mauti. Tu vipofu hadi tukose uwezo wa kuona wengine isipokuwa Mungu. Tu wafile mpaka tuwe kama maiti mkononi

[1] At-Taubah, 9:24

mwa Mungu. Tukitazamana na Mungu barabara ndipo tutapata imara ya kweli inayoshinda maono yote ya nafsi, si kabla yake. Na ndiyo imara inayosababisha kuleta kifo kwa maisha ya kitamaa ya nafsi.

Uimara wetu ndio kama Asemavyo Mungu:

بَلٰى ۚ مَنْ اَسْلَمَ وَجْهَهٗ لِلّٰهِ وَهُوَ مُحْسِنٌ [1]

Yaani, wekeni shingo mbele yangu kama mnyama wa dhabihu. Kadhalika tutajipatia daraja la imara ambapo viungo vya mwili wetu na nguvu zote na nafsi zetu vitashughulikia kazi hiyo na kifo chetu na uhai wetu viwe kwa ajili Yake tu, kama Asemavyo:

قُلْ اِنَّ صَلَاتِيْ وَنُسُكِيْ وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِيْ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ ۙ﴿۱۶۳﴾ [2]

Yaani, Sema, sala yangu na dhabihu yangu, na uhai wangu na mauti yangu ni kwa ajili ya Mungu. Na upendo wa mtu kwa Mungu ukifikia daraja hili kwamba kufa kwake na kuhuika kwake hakuwi kwa ajili yake mwenyewe bali kwa ajili ya Mungu, hapo Mungu Anayedumu kuwapenda wampendao Yeye, Huwashushia mapenzi Yake, na kwa mapenzi mawili kukutana, nuru moja huzalika ndani ya mtu ambayo dunia haiielewi wala haiwezi kuitambua. Damu za maelfu ya Masiddiki na watawa zilimwagwa kwa sababu dunia haikuwatambua; wakaitwa walaghai na

---

[1] Al-Baqarah, 2:113

[2] Al-An‘aam, 6:163

wenye kujipenda, kwani dunia haikuweza kuona nyuso zao zenye mwanga, kama Asemavyo:

يَنْظُرُوْنَ اِلَيْكَ وَهُمْ لَا يُبْصِرُوْنَ ﴿١٩٩﴾ [1]

Yaani: Wanakutazama lakini hawaoni.

Ilmuradi nuru hiyo inapozalika ndipo mtu wa kiardhi anakuwa mtu wa kimbinguni. Yule aliye Mmiliki wa kila kitu, Anazungumza ndani yake na Anaonyesha miako ya Uungu wake; Anaufanya moyo wake uliojaa mapenzi matakatifu kuwa Kiti chake cha Enzi. Na tangu hapo mtu huyo kwa kupata mabadiliko ya kinuru anakuwa mtu mpya, na Mungu pia Anakuwa Mpya kwake na kudhihirisha desturi na suna mpya. Siyo kwamba Mungu Huyu ni mwingine au suna hizi ni zingine, bali hizo zinakuwa tofauti na zile za kawaida ambazo falsafa ya kidunia haizitambui. Na kuhusu mtu huyu Mungu Anasema:

وَمِنَ النَّاسِ مَنْ يَّشْرِىْ نَفْسَهُ ابْتِغَآءَ مَرْضَاتِ اللّٰهِ ؕ وَاللّٰهُ رَءُوْفٌۢ بِالْعِبَادِ ﴿٢٠٨﴾ [2]

Yaani: Miongoni mwa wanaadamu, kuna watu wa daraja la juu zaidi wanaojipoteza katika radhi ya Mungu; wanauza uhai wao na kujinunulia radhi ya Mungu. Hao ndio watu ambao juu yao kuna rehema ya Mungu. Kadhalika mtu anayefikia daraja la hali ya roho hujitolea katika njia ya Mungu.

---

[1] Al-A'raaf, 7:199
[2] Al-Baqarah, 2:208

Mwenyezi Mungu Anasema katika aya hizo kwamba yule mtu anaokoka katika udhia wa kila aina ambaye anauuza uhai wake katika njia ya radhi Yangu, na kwa bidii anahakikisha yu wa Mungu, na anaona dhati yake kuwa kitu kilichoumbwa ili kumtii Mwumba na kuwahudumia vitumbe. Kisha mema ya kweli yanayolingana na kila kipawa chake huyatenda kwa shauku na jazba na moyo wote kana kwamba anamwona Mpendwa wake katika kioo cha utii wake. Shabaha yake hufanana na shabaha ya Mungu. Na ladha zake zote huwa katika kumtii Yeye. Na hutenda matendo mema si kwa kusumbuka bali kwa kuvutika na ladha na utamu. Hii ndiyo Pepo ambayo mtu aliyefikia daraja la roho huipata papa hapa. Na ile Pepo atakayopata huko akhera, kwa kweli, ni kivuli cha Pepo hii ya hapa duniani ambayo uwezo wa Mungu utaidhihirisha huko kwa sura ya kiwiliwili. Akiashiria kwenye jambo hili, Anasema Mwenyezi Mungu:

وَلِمَنْ خَافَ مَقَامَ رَبِّهِۦ جَنَّتَانِ ﴿٤٧﴾ [1]

وَسَقَىٰهُمْ رَبُّهُمْ شَرَابًا طَهُورًا ﴿٢٢﴾ [2]

إِنَّ ٱلْأَبْرَارَ يَشْرَبُونَ مِن كَأْسٍ كَانَ مِزَاجُهَا كَافُورًا ﴿٦﴾

---

[1] Ar-Rahmaan, 55:47

[2] Ad-Dahr, 76:22

عَيْنًا يَشْرَبُ بِهَا عِبَادُ اللَّهِ يُفَجِّرُونَهَا تَفْجِيرًا ۝٧ [1]

يُسْقَوْنَ فِيهَا كَأْسًا كَانَ مِزَاجُهَا زَنْجَبِيلًا ۝١٨

عَيْنًا فِيهَا تُسَمَّىٰ سَلْسَبِيلًا ۝١٩ [2]

إِنَّا أَعْتَدْنَا لِلْكَافِرِينَ سَلَاسِلَا وَأَغْلَالًا وَسَعِيرًا ۝٥ [3]

وَمَنْ كَانَ فِي هَٰذِهِ أَعْمَىٰ فَهُوَ فِي الْآخِرَةِ أَعْمَىٰ وَأَضَلُّ سَبِيلًا ۝٧٢ [4]

Yaani, mwenye kuogopa makamu ya Mola wake atapata Pepo mbili: moja katika dunia hii hii na nyingine huko akhera. Na watu ambao wamejipoteza ndani ya Mungu, Mungu amewanywesha kinywaji kilichowatakasa nyoyo zao na mawazo yao na nia zao. Watu wema wanajinywea sharabeti iliyochanganyika na kafuri. Wanakunywa katika chemchemi wanayochimba wenyewe.

## UHAKIKA WA SHARUBATI YA KAFURI NA YA TANGAWIZI

Nimekwisha eleza nyuma kwamba neno 'Kafuri' limetumika katika aya hii kwa sababu, katika lugha ya Kiarabu, Kafar linamaanisha kuzima na kufunika. Basi, muradi wake ni kwamba hao wamekunywa kikombe cha kuelekea kwa Mungu kwa ikhlasi na

[1] Ad-Dahr, 76:6-7
[2] Ad-Dahr, 76:18-19
[3] Ad-Dahr, 76:5
[4] Banii Israaiil, 17:73

kujitenga na vyote vingine hata kwamba mapenzi ya dunia yamepoa kabisa. Ni jambo linalojulikana kwamba maono yote huzalika katika moyo; na kama moyo ukiepukana na mawazo yasiyofaa hata kwamba hauhusikani nayo kabisa, hapo maono hayo yanaanza kupungua pole pole mpaka yanafutika kabisa. Basi hapa Mungu anayo shabaha hiyo hiyo na anafahamisha katika aya hii kwamba wale wanaoelekea kwake kikamilifu, hujitenga mbali kabisa na tamaa za nafsi; na humwelekea kabisa hata kwamba nyoyo zao zikapoa katika shughuli za dunia na maono yao yakakoma jinsi kafuri inavyokomesha sumu.

Kisha Amesema, hao watu baada ya kunywa vikombe vya kafuri wanavinywa vikombe vilivyochanganyika na Zanjabil (tangawizi). Tambueni kwamba neno Zanjabil ni mchanganyiko wa maneno mawili: Zana na Jabal. Zana katika Kiarabu humaanisha kupanda juu, na jabal ni mlima. Ukichanganya, neno litakuwa Zanal-Jabal, yaani kapanda mlima. Jueni kwamba baada ya kupona katika maradhi mabaya sana, mtu hupata hali mbili kabla hajapata afya njema kamili. Hali ya kwanza ndiyo ile ambapo nguvu ya sumu inapoa na hatari inaanza kuondoka na shambulio la hali za kisumu hupita na tufani ya kuangamiza iliyozuka inatulia, lakini bado viungo vya mwili vina udhaifu; mtu hawezi kufanya kazi ya nguvu; bado anatembea kwa kuanguka-anguka. Na hali ya pili ndiyo ile

ambapo afya ya kawaida inarejea na mwili unajaa nguvu; na baada ya kupata nguvu mtu anapata moyo wa kupanda mlimani bila kusita na anapenda kwa furaha ya moyo atembee kwenye vilele vya juu. Basi katika daraja la tatu katika msafara wa roho mtu anapata nguvu kama hiyo. Kuhusu hali hii Mwenyezi Mungu ameashiria katika aya hiyo hapo juu kwamba watawa wa hali ya juu kabisa wanavinywa vikombe vilivyochanganyika na tangawizi; yaani baada ya kupata nguvu kamili ya kiroho, hupanda vilele vya juu na mambo makubwa makubwa hutendeka kwa mikono yao, nao wanaonyesha jitihada za ajabu kabisa katika njia ya Mwenyezi Mungu.

## ATHARI YA TANGAWIZI

Ibainike hapa kwamba sawa na elimu ya Utibabu, tangawizi ni dawa inayoimarisha joto la asili la mwilini na kuzuia kuharisha. Hiyo imepewa jina Zanjabil kwa sababu hii tu kwamba inampa nguvu mnyonge na kumwongezea joto hata kwamba mtu huyo huweza kupanda milima. Kwa kulinganisha aya zinazotaja kafuri na tangawizi, Mwenyezi Mungu Anakusudia kuwafahamisha watumishi wake kwamba mtu anapoelekea kwenye wema kutoka kwenye maono ya nafsi, hapo mwanzoni anapata hali ambapo sumu-sumu zake huzuiwa, na tamaa za nafsi zaanza kupungua jinsi kafuri inavyozuia vitu vya sumu-sumu na kwa hiyo inasaidia katika kuzuia kipindupindu na

homa kali ya matumboni. Kisha nguvu ya sumu-sumu inapokwisha kabisa na mtu anapopona lakini yu dhaifu, hapo hatua ya pili ni kwamba huyo mgonjwa mnyonge anapata nguvu kwa sharubati ya tangawizi. Na sharubati ya tangawizi ndiyo dhihirisho la uzuri na jalali ya Mungu Mwenyezi iliyo chakula cha roho. Mtu anapopata nguvu kutokana na onyesho hili la jalali, hapo anapata uwezo wa kupanda milima mirefu, na anafanya kazi ngumu za ajabu katika njia ya Mungu ambazo asingeweza kufanya mtu yeyote pasipo joto la kiashiki moyoni mwake. Kwa kifupi, Mwenyezi Mungu Ametumia maneno mwaili kwa kufahamisha hali hizo mbili: moja Kafuri linalomaanisha kuzuia na la pili Zanjabil (tangawazi) lielezalo kupanda juu. Katika msafara huu pia msafiri wa kiroho anazo hali hizo mbili.

Aya inaishia hivi: اِنَّآ اَعْتَدْنَا لِلْكٰفِرِيْنَ سَلٰسِلَا۟ وَاَغْلٰلًا وَّسَعِيْرًا ۝

Yaani, Sisi tumewatayarishia wakanao wasiotaka kukubali ukweli, minyororo na kola za shingoni na moto uwakao. Aya hii inamaanisha kwamba wale wasiomfuata Mwenyezi Mungu kwa ukweli wa moyo wanapata pigo kutoka kwa Mungu; wananaswa katika mambo ya dunia kiasi hiki kana kwamba wametiwa minyororo miguuni; na wanayainamia mambo ya kiardhi kana kwamba ziko kola shingoni mwao zisizowawezesha kuinua vichwa juu mbinguni; na nyoyo zao huungua kwa tamaa za kupata mali, milki na madaraka na kumshinda adui na kutajirika kiasi

fulani. Basi, kwa kuwa Mwenyezi Mungu anawakuta kwamba hawafai nao wanashughulikia maovu, hapo Huwaadhibu kwa mabalaa hayo matatu. Hapa pia panaashiria kwamba mtu anapotenda tendo fulani, Mungu naye Anatenda tendo moja kuwa matokeo ya tendo la mtu yule. Mathalan, mtu anapofunga milango yote ya chumba chake, Mwenyezi Mungu analeta tendo lake la kutia giza chumbani humo. Kwani mambo yote yaliyo matokeo ya matendo yetu kwa kulingana na sheria ya ulimwengu iliyowekwa na Mungu, ndiyo matendo ya Mungu. Maana, Yeye ndiye Huleta matokeo yote. Kadhalika kama mtu akila sumu ya kuua, hapo baada ya tendo hili, Mungu ataleta tendo lake kwamba atamwua. Vile vile mtu akifanya kitendo kisichofaa kinachosababisha maradhi ya kuambukiza, basi, baada ya kitendo hiki, kitendo cha Mungu kitakuwa kwamba mtu huyo atashikwa na maradhi ya kuambukiza. Basi, kama inavyoonekana katika maisha yetu ya kidunia kwamba kila kitendo chetu kina matokeo yake ya lazima, na matokeo hayo ni kitendo cha Mungu, basi ndivyo ilivyo sheria kuhusu mambo ya dini pia, kama Asemavyo Mwenyezi Mungu katika mifano hii miwili:

اَلَّذِيْنَ جَاهَدُوْا فِيْنَا لَنَهْدِيَنَّهُمْ سُبُلَنَا [1]

[1] Al-‘Ankabuut, 29:70

فَلَمَّا زَاغُوٓا اَزَاغَ اللّٰهُ قُلُوۡبَهُمۡ ؕ [1]

Yaani, watakaofanya tendo la kumtafuta Mwenyezi Mungu ipasavyo, hapo tendo hili halina budi kuleta tendo Letu kwamba Tutawaongoza njia Zetu. Na wale waliojichagulia njia iliyopinda wala hawakutaka njia iliyonyooka, basi tendo kwa kulingana na tendo lao hili litakuwa kwamba Tutapinda nyoyo zao. Kisha, ili kufafanua zaidi hali hiyo, Anasema:

وَمَنۡ كَانَ فِىۡ هٰذِهٖۤ اَعۡمٰى فَهُوَ فِى الۡاٰخِرَةِ اَعۡمٰى وَاَضَلُّ سَبِيۡلًا ﴿۷۲﴾ [2]

Yaani, yule aliyebaki kipofu duniani humu, atakuwa kipofu vile vile katika akhera, bali mbaya zaidi kuliko vipofu. Hili linaashiria kwenye jambo hili kwamba watawa wanapata kumwona Mungu katika dunia hii hii; wanamshuhudia mpendwa wao katika ulimwengu huu huu, ambaye kwa ajili yake wanapoteza kila kitu. Kwa kifupi, aya hii inamaanisha kwamba msingi wa maisha ya kipeponi huwekwa katika dunia hii hii. Na mzizi wa upofu wa kijahanamu pia ndio maisha maovu na mapotofu katika dunia hii.

Kisha Anasema:

وَبَشِّرِ الَّذِيۡنَ اٰمَنُوۡا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ اَنَّ لَهُمۡ جَنّٰتٍ تَجۡرِىۡ مِنۡ تَحۡتِهَا الۡاَنۡهٰرُ ؕ [3]

---

[1] As-Saf, 61:6

[2] Banii Israaiil, 17:73

[3] Al-Baqarah, 2:26

Yaani, wanaoamini na kutenda mema hurithi bustani ambazo mito inapita chini yake. Katika aya hii Mwenyezi Mungu Ameifananisha imani na bustani ambazo mito inapita chini yake.

Basi, ibainike kwamba hapa imeelezwa kifalsafa kwamba jinsi mito inavyohusikana na bustani, ndivyo matendo yanavyohusikana na imani. Na jinsi bustani yoyote isivyodumu kustawi bila maji, ndivyo imani isivyoweza kuhesabiwa kuwa imani iliyo hai bila matendo mema. Kama ipo imani lakini hamna matendo, basi imani hiyo ni bure; na kama yapo matendo pasipo imani, basi hayo matendo ni ya kutaka kuonwa na watu tu. Uhakika wa Pepo ya Kiislamu ni kwamba hiyo ni kivuli cha imani na matendo ya mtu aliyotenda katika dunia hii, siyo kitu kipya kitakachoingia kutoka nje na kumpata mtu; bali Pepo ya mtu hupatikana kutoka ndani ya mtu mwenyewe. Na Pepo ya kila mmoja ni imani yake na matendo yake mema ambayo ladha yake huanza kusikika duniani humu; na bustani za imani na amali huonekana kisiri na mito nayo huonekana; lakini huko akhera bustani hizi zitahisika kidhahiri. Mafunzo matakatifu ya Mwenyezi Mungu yatuambia kwamba imani ya kweli iliyo tukufu na imara na kamili juu ya Mungu na sifa Zake na mipango Yake ndiyo Pepo ipendezayo na mti utoao matunda, na amali njema ndiyo mito ya Pepo hii, kama Asemavyo:

ضَرَبَ اللَّهُ مَثَلًا كَلِمَةً طَيِّبَةً كَشَجَرَةٍ طَيِّبَةٍ أَصْلُهَا ثَابِتٌ
وَفَرْعُهَا فِي السَّمَآءِ ﴿٢٥﴾ تُؤْتِي أُكُلَهَا كُلَّ حِينٍ [1]

Yaani, Neno lile la imani lililoepukana na kila aina ya mazidio na vipunguo, nuksi na pengo, uwongo na upuuzi, bali limekamilika kwa kila jiha, hilo hufanana na mti ulioepukana na kila aibu, ambao mzizi wake umeimarika ardhini na matawi yako mbinguni, nao hutoa matunda daima; haufikiwi na wakati wa matunda kukosekana katika matawi yake. Katika kauli hii, Mwenyezi Mungu akifananisha neno la kiimani na mti utoao matunda daima, Ameeleza alama zake tatu:

1. Kwanza ni kwamba mzizi wake, ambao unamaanisha muradi wa kweli, uimarike katika ardhi ya moyo wa mtu. Yaani, tabia ya asili na dhamiri ya mtu iwe imekwisha kubali ukweli wake na hakika yake.

2. Alama ya pili ni kwamba matawi ya neno hili yawepo mbinguni, yaani neno hili lilingane na akili na liafikiane na sheria ya asili ya kimbinguni iliyo kitendo cha Mungu. Ndiyo kusema kwamba dalili za ukweli wake na hakika yake zitokane na kanuni ya maumbile, tena dalili hizo ziwe nzuri za hali ya juu sana kana kwamba ziko mbinguni, yaani mkono wa upinzani usiweze kuzifikia.

---

[1] Ibraahiim, 14:25-26

3. Alama ya tatu ni kwamba matunda yanayofaa kuliwa yadumu kupatikana bila kukatika. Yaani baada ya juhudi za kuyapata, baraka na athari zake zionekane katika zama zote, wala zisikome baada ya kudhihirika hadi zama fulani maalum. Kisha Kasema:

مَثَلُ كَلِمَةٍ خَبِيثَةٍ كَشَجَرَةٍ خَبِيثَةٍ اجْتُثَّتْ
مِنْ فَوْقِ الْأَرْضِ مَا لَهَا مِنْ قَرَارٍ ﴿٢٧﴾ [1]

Yaani, neno baya hufanana na mti mbaya uliong'oka ardhini. Muradi wake ni kwamba tabia ya asili ya binadamu hailikubali, wala halina imara, yaani kwa kupimwa na dalili za kiakili wala kwa sheria za maumbile wala dhamiri ya mtu; bali huwa kama kisa tu kisicho na msingi. Na jinsi Kurani Tukufu inavyofananisha miti mitukufu ya imani katika akhera na zabibu, komamanga na matunda mengine mazuri na kueleza kwamba siku hiyo imani itadhihirika kwa sura ya matunda yatakayoonekana, ndivyo ilivyouita mti mbaya wa imani mbovu kwa jina Zakkum katika akhera. Anasema:

أَذَٰلِكَ خَيْرٌ نُّزُلًا أَمْ شَجَرَةُ الزَّقُّومِ ﴿٦٣﴾ إِنَّا جَعَلْنَاهَا فِتْنَةً لِّلظَّالِمِينَ ﴿٦٤﴾
إِنَّهَا شَجَرَةٌ تَخْرُجُ فِي أَصْلِ الْجَحِيمِ ﴿٦٥﴾
طَلْعُهَا كَأَنَّهُ رُءُوسُ الشَّيَاطِينِ ﴿٦٦﴾ [2]

---

[1] Ibraahiim, 14:27
[2] As-Saaffaat, 37:63-66

إِنَّ شَجَرَتَ الزَّقُّومِ ﴿٤٤﴾ طَعَامُ الْأَثِيمِ ﴿٤٥﴾ كَالْمُهْلِ
يَغْلِي فِي الْبُطُونِ ﴿٤٦﴾ كَغَلْيِ الْحَمِيمِ ﴿٤٧﴾ [1]

ذُقْ إِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْكَرِيمُ ﴿٥٠﴾ [2]

Yaani, niambieni, bustani za Peponi ni bora ama mti wa zakkum ulio jaribio kwa wadhalimu. Huo ni mti unaotokeza kutoka katika mzizi wa Jahanamu; yaani huota kwa sababu ya kiburi na majivuno ambayo ndio mzizi wa Jahanamu. Matunda yake ni kama vichwa vya mashetani. Maana ya shetani ni aangamiaye. Neno hili linatokana na Shait. Basi kwa kifupi ni kwamba kuyala matunda yake ndiyo kuangamia. Kisha kasema mti wa zakkum ni chakula cha waendao Jahanamu wanaotenda dhambi kusudi. Chakula hicho ni kama shaba iliyoyeyuka; huchemka matumboni kama mchemko wa maji ya moto. Kisha anamwambia aendaye Jahanamu: Uonje mti huu! U mwenye nguvu, mheshimiwa!! Hili ni neno la kuonyesha ghadhabu nyingi, na maana yake ni kwamba kama usingejivuna wala usingekataa ukweli kwa kuhifadhi heshima yako, usingepata kuona machungu leo. Aya hii inadokeza kwamba kwa hakika neno Zakkum ni mchanganyiko wa Dhuk na Am. Kwa sababu ya kutumiwa sana Dh imegeuka ikawa Z, na Dhuk (onja) likawa Zuk. Na Am

---

[1] Ad-Dukhaan, 44:44-47
[2] Ad-Dukhaan, 44:50

imetengenezwa kwa kuchukua herufi ya kwanza na ya mwisho katika sehemu ya aya iliyobakia, yaani:

إِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْكَرِيمُ ﴿٥٠﴾ [1]

Ndiyo kusema kwamba jinsi Mwenyezi Mungu alivyofananisha maneno ya kiimani ya dunia hii na Pepo, ndivyo alivyofananisha maneno yapingayo imani katika dunia hii hii na Zakkum na akayahesabu kuwa mti wa Jahanamu; na akafafanua kwamba Pepo na Jahanamu huanzia katika dunia hii hii kama asemavyo mahali pengine kuhusu Jahanamu:

نَارُ اللَّهِ الْمُوقَدَةُ ﴿٧﴾ الَّتِي تَطَّلِعُ عَلَى الْأَفْئِدَةِ ﴿٨﴾ [2]

Yaani, Jahanamu ndio moto ambao chanzo chake ni ghadhabu ya Mungu na huwaka kwa dhambi, na kwanza huenea moyoni. Ndani yake kuna ishara kwamba asili ya Moto huu ni huzuni na majuto na machungu yanayoushika moyo, kwani adhabu zote za roho huanzia moyoni kisha huenea mwili mzima. Tena Anasema mahali pengine:

وَقُودُهَا النَّاسُ وَالْحِجَارَةُ [3]

Yaani, kuni za moto wa Jahanamu zinazodumisha moto kuwaka ni mambo mawili: Kwanza, wale watu

---

[1] Ad-Dukhaan, 44:50
[2] Al-Humazah, 104:7-8
[3] Al-Baqarah, 2:25

wanaoviabudu vitu vingine kwa kumwacha Mungu wa kweli ama wale wanaoabudiwa hali huridhika kuabudiwa, kama asemavyo:

إِنَّكُمْ وَمَا تَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ حَصَبُ جَهَنَّمَ [1]

Yaani, ninyi na miungu wenu wa bandia waliojifanya miungu ilhali ni wanadamu, watatupwa motoni. (2) Kuni za pili za Jahanamu ni masanamu. Ndiyo kusema kwamba kama mambo hayo yasingekuwapo, basi na Jahanamu isingekuwapo.

Hivyo, ni dhahiri kutokana na aya hizo kwamba katika Neno Tukufu la Mwenyezi Mungu, Pepo na Jahanamu siyo kama dunia hii ya kiwiliwili, bali chanzo cha hizo mbili ni mambo ya roho. Naam, vitu hivyo vitadhihirika kwa sura ya kiwiliwili lakini havitatokana na ulimwengu huu wa kiwiliwili.

## NJIA YA KUUNGANA KIROHO NA MWENYEZI MUNGU KIKAMILIFU

Sasa nikirejea tena kwenye shabaha hasa nasema kwamba njia ya kuungana na Mungu kiroho kwa ukamilifu tuliyofundishwa na Kurani Tukufu ni Islam na Dua iliyomo katika Sura Faatiha. Yaani kwanza kujitolea maisha mazima katika njia ya Mungu na kisha kudumu kuomba dua iliyofundishwa katika Sura Faatiha. Kiini cha Islam ni vitu hivi viwili:

[1] Al-Anbiyaa, 21:99

Kujitupa kwa Mungu na Ombi la Sura Faatiha. Duniani humu kuna njia hii pekee iliyo ya hali ya juu sana kwa kumfikia Mungu na kujinywea maji ya wokovu wa kweli; bali hii ndiyo njia ya pekee kabisa iliyowekwa na sheria ya asili kwa ajili ya mtu kupata maendeleo na kumpata Mungu. Na wale tu wanampata Mungu ambao wanaingia katika moto wa kiroho wa muradi wa Islam na kudumu kuomba dua iliyomo katika Faatiha. Islam ni nini? Ni ule Moto uwakao ambao kwa kuyaunguza maisha yetu duni na kuwachoma moto waabudiwa wa uwongo, unamtolea Mungu Mtukufu wa kweli dhabihu ya uhai wetu na mali zetu na heshima zetu. Kwa kuingia katika chemchemi hii twayanywa maji ya maisha mapya na nguvu zetu zote zinaungana na Mungu jinsi jamaa wa karibu wanavyoungana pamoja. Moto mmoja unatoka kutoka ndani yetu kama umeme, na moto mwingine hutushukia kutoka juu, na kwa kukutana miako hiyo miwili tamaa zetu zote na mapenzi ya kila kitu minsghairi ya Mungu huteketea, nasi twajifia kutokana na maisha yetu ya kwanza. Hali hii sawa na Kurani Tukufu ndiyo Islam. Kwa njia ya kushikamana na Islam, tamaa zetu za nafsi zinajifia na kisha twahuika upya kwa njia ya dua. Kwa ajili ya maisha haya ya pili ufunuo ni jambo la lazima. Kufikia daraja hili ndiyo huitwa Liqaa (kumlaki Mungu), yaani kumwona Mungu na kumshuhudia. Katika daraja hili mtu anaungana kikamilifu na Mungu kana kwamba anamwona kwa macho; na

anajaliwa nguvu; na hisia zake zote na vipawa vyake vyote hung'aa; na mvutano wa maisha matakatifu huanza kwa nguvu. Hilo ndilo daraja ambamo Mungu huwa jicho la mtu analoonea, na ulimi anaozungumzia na mkono ambao kwao anashambulia, na sikio ambalo kwalo anasikia na mguu ambao kwao anatembea. Katika kauli hii Mwenyezi Mungu anadokeza kwenye hiyo habari:

يَدُاللهِ فَوْقَ اَيْدِيْهِمْ ۚ [1]

Yaani, huu mkono wake (Mtume) ndio mkono wa Mwenyezi Mungu ulio juu ya mikono yao. Tena Anasema:

وَمَا رَمَيْتَ اِذْ رَمَيْتَ وَلٰكِنَّ اللّٰهَ رَمٰى ۚ [2]

Yaani: Hukutupa ulipotupa, walakini Mwenyezi Mungu ndiye Aliyetupa. Ilmurudi, katika daraja hili mtu anaunganika na Mungu kikamilifu na radhi tukufu ya Mungu Mwenyezi hupenya katika roho, na nguvu za khulka zilizokuwa dhaifu, zaonekana imara kama milima katika daraja hili; akili na busara huwa nyepesi; na hii ndiyo maana ya Aliyosema Mwenyezi Mungu:

وَاَيَّدَهُمْ بِرُوْحٍ مِّنْهُ ؕ [3]

---

[1] Al-Fat'h, 48:11
[2] Al-Anfaal, 8:18
[3] Al-Mujaadalah, 58:23

(Yaani: Na Akawasaidia kwa Roho itokayo Kwake). Katika daraja hili mito ya Upendo na ashiki huumuka kwa namna ambapo kufa kwa ajili ya Mwenyeji Mungu na kupata maelfu ya udhia na kufedheheka huwa rahisi kama kuvunja kijiti chepesi. Mtu huvutika kwa Mwenyezi Mungu, asitambue nani anamvuta. Mkono mmoja usioonekana unambeba kila mahali, na kutimiza matakwa ya Mungu huwa kanuni ya maisha yake. Katika daraja hili Mungu Mwenye Enzi huonekana karibu zaidi sana kama Asemavyo:

نَحْنُ اَقْرَبُ اِلَيْهِ مِنْ حَبْلِ الْوَرِيْدِ۝۱۷ [1]

Yaani: Sisi Tu karibu naye zaidi kuliko halkumu yake. Katika hali hii, mtu mwenye daraja hili uhusiano wake wote ulio duni hufutika jinsi tunda lililoiva linavyodondoka lenyewe kutoka kwenye mti. Na uhusiano wake na Mungu Mwenye Enzi unakuwa mkubwa zaidi, na mtu huenda mbali na viumbe, na anapata heshima ya kufunuliwa na Mwenyezi Mungu na kuongea naye. Milango ya kulipatia daraja hili bado ipo wazi jinsi ilivyokuwa wazi zamani; na hata sasa fadhili ya Mwenyezi Mungu huwatolea neema hii watafutaji jinsi ilivyotoa zamani. Lakini njia hii haipatikani kwa maneno matupu ya kipuuzi na mambo yasiyo na msingi, na mlango huu haufunguliwi na majivuno. Walitakao ni wengi bali

---

[1] Qaaf, 50:17

walipatao ni wachache. Sababu yake ni nini? Ni kwamba daraja hili linataka bidii ya kweli na jitihada hasa. Mwaweza kupiga domo mpaka kiyama, hapatafanyika lolote liwalo. Kukanyaga moto huu kwa usadiki, wanaouogopa watu wengine na kuukimbia, ndilo sharti la kwanza la kupita njia hii. Kama hamna bidii kwa vitendo, maneno mengi hayana maana. Kuhusu hii habari Mwenyezi Mungu Anasema:

وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِي عَنِّي فَإِنِّي قَرِيبٌ ۖ أُجِيبُ دَعْوَةَ الدَّاعِ إِذَا دَعَانِ ۖ
فَلْيَسْتَجِيبُوا لِي وَلْيُؤْمِنُوا بِي لَعَلَّهُمْ يَرْشُدُونَ ﴿١٨٧﴾ [1]

Yaani, watumishi wangu wakikuuliza kunihusu Mimi kwamba niko wapi, waambie Nipo karibu nanyi, sana. Nasikia ombi la mwombaji; basi yawapasa wanitafute kwa maombi na waniamini ili wapate kuongoka.

[1] Al-Baqarah, 2:187

# SWALI LA PILI

## HALI YA MTU INAKUWAJE BAADA YA KUFA?

Jawabu la swali hili ni kwamba hali ya mtu baada ya kufa kwa kweli si hali ngeni; bali hali zile alizokuwa nazo hapa duniani zinabainika kwa uwazi zaidi baada ya kufa. Hali yoyote nzuri au mbaya, ya imani ya mtu na matendo yake, huwa inafichikana ndani ya mtu katika dunia hii, na tiba yake au sumu yake huiathiri dhati ya mtu. Lakini haitakuwa hivyo huko akhera, bali athari hizo zote zitaonekana wazi wazi. Mfano wake unaonekana katika njozi. Hali zinazoushinda mwili wa mtu zadhihirika kwa sura ya kiwiliwili katika njozi. Mtu anapokurubia kupata homa kali, mara nyingi anaota moto na miako ya moto katika njozi. Na katika hali ya kuelekea kupata homa ya kamata na mafua, hapo huota yumo majini. Kwa kifupi, mwili unapokuwa katika hali ya kushikwa na maradhi fulani, hali hiyo huonekana kwa sura ya methali. Hivyo, basi, kwa kutafakari kuhusu mfumo wa njozi, kila mmoja anaweza kufahamu kwamba huko akhera pia suna ya Mungu ndiyo hii hii. Kwani jinsi njozi inavyogeuza hali yetu ya roho na kuonyesha kuwa hali ya kiwiliwili, ndivyo itakavyokuwa kule akhera. Siku hiyo matendo yetu

na matokeo ya matendo hayo yataonekana kwa sura ya kiwiliwili; na yoyote tutakayoenda nayo huko kutoka kwenye dunia hii ambayo hayaonekani hapa, yote hayo yatabainika katika nyuso zetu. Na kama zile sura anazoona mtu katika njozi hazidhani kuwa ni mifano tu bali anaamini kuwa ni vitu hasa, kadhalika itakuwa huko akhera. Bali kwa njia ya methali hizo, Mwenyezi Mungu Atadhihirisha kudra Yake mpya. Na kwa kuwa hiyo ni kudra kamili, basi hata kama tusitaje mithali bali tuseme kwamba huko ndiko kuzaliwa upya kwa uwezo wa Mungu, itakuwa sahihi na kweli tupu. Mwenyezi Mungu Anasema:

فَلَا تَعْلَمُ نَفْسٌ مَّآ أُخْفِيَ لَهُم مِّن قُرَّةِ أَعْيُنٍ ۚ [1]

Yaani, nafsi yoyote itendayo mema haijui ni neema zipi zilizofichikana kwa ajili yake. Ndiyo kusema Mwenyezi Mungu amezihesabu neema hizo kwamba zimefichikana ambazo hazina mfano wake katika hii dunia. Ni dhahiri kwamba neema za dunia hii hazikufichikana kwetu; twaelewa maziwa, komamanga, zabibu na kadhalika, na sikuzote twavila vitu hivyo. Kwa hiyo, imehakikika kwamba vitu vya akhera ni vitu vingine kabisa ambavyo vimeshirikiana na vitu vya dunia katika majina tu. Hivyo, yule aliyevidhania vitu vya Peponi kuwa vitu vya dunia

---

[1] As-Sajdah, 32:18

hii, yeye mtu huyo hajaelewa hata herufi moja ya Kurani Tukufu.

Kuhusu maelezo ya aya hiyo niliyotaja juu, Bwana wetu Mtume[saw] amesema kwamba neema za Peponi ni vitu ambavyo hakuna jicho lililowahi kuviona, wala sikio lililovisikia wala havikupita katika nyoyo. Lakini neema za dunia hii twaziona kwa macho na kusikia habari zake kwa masikio na twaziwaza hizo pia moyoni mwetu. Basi, kama Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanasema kwamba vitu vya Peponi vitakuwa vigeni kabisa kwetu, hapo tutakwenda mbali na Kurani Tukufu ikiwa tutadhani kuwa maziwa ya huko Peponi ndiyo haya haya ya kidunia yanayokamuliwa kutoka kwa ng'ombe na nyati, kana kwamba huko kutakuwa na makundi ya wanyama wenye kutoa maziwa, na kwenye mti ya Peponi kutakuwa na mizinga mingi sana ambayo Malaika wakiitafuta watatoa asali kutoka katika hiyo na kuimimina ndani ya mito. Je, mawazo haya yanaafikiana hata kidogo na mafunzo ambayo yanafundisha kwamba dunia haijaona vitu hivyo, na vitu hivyo vinaangaza roho na kuongeza maarifa kumhusu Mungu na ni vyakula vya roho? Ijapokuwa vyakula hivyo vimeelezwa kwa sura ya kiwiliwili, lakini papo hapo imefahamishwa kwamba chanzo chake ni roho na ukweli.

Asidhani mtu yeyote kwamba sawa na aya hii hapa chini watu watakaopewa neema huko Peponi watazitambua kwa kusema kwamba hizi ndizo tulizopewa zamani pia:

وَبَشِّرِ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ أَنَّ لَهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ ۖ كُلَّمَا رُزِقُوا مِنْهَا مِنْ ثَمَرَةٍ رِزْقًا ۙ قَالُوا هَٰذَا الَّذِي رُزِقْنَا مِنْ قَبْلُ ۖ وَأُتُوا بِهِ مُتَشَابِهًا ۖ [1]

Yaani: Wapashe habari njema wale walioamini na kutenda mema wasio na ila yoyote kwamba watarithi Pepo ambazo mito inapita chini yake. Watakapopata huko akhera matunda kutokana na miti ya huko waliyokwisha yapata katika maisha ya dunia hii, watasema haya ndiyo matunda tuliyojaliwa mapema, kwani watayaona yanafanana na hayo ya zamani. Sasa kudhani kwamba matunda ya zamani yanamaanisha neema za kiwiliwili ni kosa moja kwa moja tena ni kinyume cha muradi wa kweli wa aya. Bali Mwenyezi Mungu Anasema kwamba waaminio waliotenda mema walitengeneza kwa mikono yao Pepo ambayo miti yake ni imani na mito yake ndiyo matendo mema. Matunda ya Pepo hii hii watayala katika akhera pia ambayo matunda hayo yatabainika zaidi na yatakuwa matamu zaidi. Na kwa kuwa watakuwa wameisha yala matunda hayo

[1] Al-Baqarah, 2:26

kiroho katika dunia, hivyo watayatambua huko akhera na watasema haya yanaonekana kana kwamba ni yale yale tuliyoisha kula hapo kabla, nao watayakuta yanafanana na vyakula vya zamani. Basi aya hii inabainisha kwa uwazi kwamba wale waliokuwa wakila katika dunia hii chakula cha huba na upendo wa Mungu, sasa watakipata hicho kwa sura ya kiwiliwili. Na kwa kuwa walikwisha tambua ladha ya mapenzi ya Mungu zamani na walielewa utamu huo, hivyo roho zao zitapata kukumbuka zile zama ambapo walikuwa wakimkumbuka kwa mapenzi Mpendwa wa kweli katika giza la usiku kwenye kona katika hali ya upweke na kupata ladha ya kumkumbuka Yeye.

Ilmuradi, hapa havikutajwa vyakula vya kiwiliwili. Na kama mtu akifikiria kwamba ikiwa waja wa Mungu walikwisha pewa chakula hiki kwa njia ya roho katika dunia, basi siyo sawa kusema kwamba hizi ni neema ambazo hakuna duniani aliyewahi kuziona au kuzisikia au kuziwaza moyoni maana kwa njia hii aya mbili zitapingana, basi jawabu lake ni kwamba upingamizi ungepatikana iwapo aya hiyo ingemaanisha neema za kidunia. Na kama siyo neema za dunia, basi chochote anachopata mja wa Mungu kwa sura ya kumtambua Mungu hicho ni neema ya akhera kwa hakika ambayo mfano wake anajaliwa ili kumhimza.

Kumbukeni, mja wa Mungu hahusikani na dunia hii, kwa hiyo dunia inamchukia; bali yeye hutokana na mbingu na kwa hiyo hujaliwa neema ya kimbinguni. Mtu wa dunia anapata neema za kidunia na mja wa mbinguni hupata neema za kimbinguni. Basi ni kweli tupu kwamba neema hizo zimefichwa zisihisike na masikio ya kidunia na nyoyo za kidunia na macho ya kidunia. Lakini yule ambaye maisha yake ya kidunia yalififikiwa na mauti na akanyweshwa kiroho kikombe ambacho atakinywa kidhahiri, yeye mtu huyo atakumbuka kunywa kiroho pindi atakapokunywa kidhahiri kwa kiwiliwili. Lakini pia ni kweli kwamba yeye atatambua ya kuwa neema hii ni ngeni kwa macho na masikio ya kidunia na kadhalika. Kwa kuwa yeye alikuwa duniani ingawaje hakutokana na dunia, hivyo naye atashuhudia kwamba neema hiyo haiko miongoni mwa neema za kidunia wala jicho lake halikuona wala sikio lake halikuwahi kuisikia na wala moyo wake haukuiwaza alipokuwa katika dunia; lakini ameiona mifano yake katika akhera ambayo haikutokana na dunia, ball hiyo lilikuwa ni habari ya akhera tu ambayo yeye alihusikana kwayo wala hakuhusikana na dunia hata kidogo.

## MAARIFA YA NAMNA TATU KUHUSU AKHERA

Kumbukeni vile vile kwamba hali za baada ya kifo sawa na Kurani Tukufu ni za namna tatu, nazo ni

maarifa ya namna tatu ya Kurani kuhusu akhera ambayo nayaandika hapa chini.

MAARIFA YA KWANZA

Maarifa ya kwanza ni kwamba Kurani Tukufu inakariri mara kwa mara kwamba maisha ya akhera si kitu kigeni, bali maonyesho yake yote ni vivuli na athari za maisha haya ya kidunia, kama isemavyo:

وَكُلَّ إِنسَانٍ أَلْزَمْنَاهُ طَائِرَهُ فِي عُنُقِهِ ۖ وَنُخْرِجُ لَهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ
كِتَابًا يَلْقَاهُ مَنشُورًا ﴿١٤﴾ [1]

Yaani, sisi tumefungia kila mmoja katika dunia hii hii athari ya amali zake shingoni mwake, nasi tutadhihirisha athari hizo zilizofichikana siku ya Kiyama na kuzionyesha kwa sura ya daftari ya vitendo vyake. Katika aya hii neno liliotumika kumaanisha vitendo ni Twaair ambalo tafsiri yake ni ndege. Kimethali hilo linamaanisha kitendo kwani kila kitendo chema au kibaya baada ya kutendeka huruka kama ndege na uchovu wake au utamu wake unapotea lakini athari yake njema au mbaya inabakia moyoni.

Kurani inafundisha kwamba kila amali huendelea kuimarisha athari yake ndani kwa ndani. Mtu anapotenda tendo lolote, Mwenyezi Mungu naye hutenda tendo sawa na tendo la mtu; na tendo hilo la Mungu linahifadhi dhambi hiyo ya mtu au wema

[1] Banii Israaiil, 17:14

wake visipotee, bali athari zake huchorwa katika moyo wake, uso wake, macho yake, mikono yake na miguu yake. Hiyo ndiyo daftari ya vitendo iliyofichikana ambayo itadhihirika wazi wazi huko akhera.

Kisha mahali pengine anasema kuwahusu waendao Peponi:

يَوْمَ تَرَى الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ يَسْعَىٰ نُورُهُم بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَبِأَيْمَانِهِم [1]

Yaani, siku hiyo nuru waliyo nayo isiyoonekana hapa, itadhihirika wazi wazi ikikimbia mbele yao na kulia kwao. Na mahali pengine asema kuhusu waovu:

أَلْهَاكُمُ التَّكَاثُرُ ﴿٢﴾ حَتَّىٰ زُرْتُمُ الْمَقَابِرَ ﴿٣﴾ كَلَّا سَوْفَ تَعْلَمُونَ ﴿٤﴾
ثُمَّ كَلَّا سَوْفَ تَعْلَمُونَ ﴿٥﴾ كَلَّا لَوْ تَعْلَمُونَ عِلْمَ الْيَقِينِ ﴿٦﴾ لَتَرَوُنَّ
الْجَحِيمَ ﴿٧﴾ ثُمَّ لَتَرَوُنَّهَا عَيْنَ الْيَقِينِ ﴿٨﴾ ثُمَّ لَتُسْأَلُنَّ يَوْمَئِذٍ عَنِ النَّعِيمِ ﴿٩﴾ [2]

Yaani, tamaa nyingi za kidunia zimewaghafilisheni kutafuta akhera hadi mmeingia makaburini. Msiwe na mapenzi ya dunia. Karibuni mtajua kwamba kuipenda dunia hakufai. Nawaambieni tena, karibuni mtajua kuipenda dunia hakufai. Kama mngekuwa na elimu ya yakini, lazima mngeiona Jahanamu katika hii hii dunia. Kisha mtaiona kwa jicho la yakini huko katika Barzakh (baada ya kufa lakini kabla ya kiyama). Tena siku ya kufufuliwa mtakamatwa kikamilifu na adhabu

[1] Al-Hadiid, 57:13
[2] At-Takaathur, 102:2-9

itawashikeni kwa ukamilifu, hapo siyo kimaneno tu bali kwa kitendo mtapata elimu ya Jahanamu.

NAMNA TATU ZA ELIMU

Katika aya hizo Mwenyezi Mungu amebainisha kwamba waovu huwa na maisha ya kijahanamu katika dunia hii hii yanayofichikana; na kama wakitafakari wataishuhudia hapa hapa duniani. Hapa Mwenyezi Mungu ameigawa elimu katika madaraja matatu: Ilmul-Yakin (elimu ya yakini), Ainul-Yakin (jicho la yakini), Hakkul-Yakin (ukweli wa yakini). Ili kufafanua elimu hizi za namna tatu, mifano hii itasaidia: Kwa mfano, mtu akiuona moshi mwingi kutoka mbali, mara fikira yake kutoka moshi itaelekea kwenye moto na atakuwa na yakini kuna moto huko kwa kufikiria kwamba kuna uhusiano usiotanguka baina ya moshi na moto, na kuna ufungamano kamili kati yao; penye moshi pana moto. Basi elimu hii huitwa Ilmul-Yakin, yaani yakini iliyopatikana kwa njia ya hoja na dalili, siyo kwa kukiona kitu hasa. Na kisha akiisha uona ulimi wa moto atapata Ainul-Yakin, yaani jicho la yakini au tuseme yakini iliyopatikana kwa kujionea kitu chenyewe. Kisha akiingia mwenyewe katika moto atapata Hakkul-Yakin, yaani ukweli wa yakini — yaani siyo ameona tu kwa macho bali ameisha athirika na hicho. Basi, Mwenyezi Mungu anasema katika aya hizo kwamba elimu ya yakini ya Jahanamu mwaweza kuipata katika dunia hii hii; kisha huko katika Barzakh

mtapata Ainul-Yakin, na siku ya kufufuliwa elimu yenu hiyo itafikia daraja la Hakkul-Yakin.

## ULIMWENGU WA AINA TATU

Ibainike hapa kwamba sawa na mafunzo ya Kurani Tukufu, ziko aina tatu za ulimwengu.

Kwanza, dunia iitwayo ulimwengu wa vitendo na uumbaji wa kwanza. Katika dunia hii mtu hutenda mema na maovu. Ijapokuwa huko akhera pia maendeleo yatapatikana, lakini hayo ni kwa fadhili ya Mungu tu wala siyo kwa juhudi za mtu.

Ulimwengu wa pili huitwa Barzakh. Kwa hakika katika lugha ya Kiarabu Barzakh ni kitu kilichopo baina ya vitu viwili. Na kwa kuwa zama za baada ya kufa ziko baina ya dunia hii na akhera, basi zikaitwa Barzakh. Neno hili tangu kale tokea kuumbwa kwa dunia hii linatumika kwa ulimwengu wa kati, kwa hiyo ndani ya neno hili ushuhuda umefichikana juu ya kuwepo kwa ulimwengu wa katikati. Nimekwisha eleza katika kitabu changu, Minanur-Rahman, kwamba maneno ya Kiarabu ndiyo yaliyonenwa na kinywa cha Mungu na katika dunia lugha hii peke yake ndiyo iliyo lugha ya Mungu, na ya kale, na chanzo cha elimu zote, na mama wa lugha zote, na ni Kiti cha Enzi cha kwanza na cha mwisho cha wahyi wa Mungu: Kiti cha kwanza cha Enzi cha wahyi, kwa sababu Kiarabu chote kilikuwa Neno la Mungu lililokuwa pamoja na Mungu tangu azali, kisha Neno

hilo likashuka duniani na kutokana na hilo dunia ikaziunda lugha mbalimbali. Kiti cha Enzi cha Mungu cha Mwisho kikawa lugha ya Kiarabu kwani Kitabu cha Mwisho cha Mwenywzi Mungu, yaani Kurani Tukufu, kilifunuliwa kwa Kiarabu. Basi, Barzakh ni neno la Kiarabu lililo mchanganyiko wa Zakh-kha na Barra, maana yake nafasi ya kutenda matendo imekwisha na ikaingia katika hali ya ufícho. Hali ya Barzakh ndiyo ile ambapo umbo hili la muda la binadamu linavunjika, na roho na mwili hutengana. Jinsi mwili unavyowekwa katika shimo (kaburi) ndivyo roho nayo inavyoingia katika shimo la aina fulani linalohakikishwa na neno Zakh-kha, kwani sasa haiwezi kutenda mema au mabaya yaliyowezekana kwa kuungana mwili na roho. Ni dhahiri kwamba afya njema ya roho yetu hutegemea mwili. Sehemu maalum ya ubongo ikipigwa, hupotea uwezo wa kukumbuka; sehemu yake nyingine ikipata afa, uwezo wa kufikiria huaga na mtu anapotewa na fahamu; na ubongo ukifurukuta au kuvimba au damu au kitu fulani kikitulia humo na kusababisha kizuizi kamili au nusu-nusu, hapo mtu hupata kuzimia ghafla au kifafa au kiharusi. Maarifa yetu hutuyakinishia kwamba roho yetu haifai pasipo mwili. Basi ni batili kuwaza kwamba roho yetu tupu isiyo na mwili yaweza kupata furaha yoyote. Tukikubali kwa nguvu habari hii, ni jambo jingine, lakini hiyo haiwezi kuhakikishwa na dalili. Kabisa hatuwezi kuelewa kwamba roho yetu hii inayokuwa hoi kwa uharibifu kidogo tu mwilini,

itawezaje kubaki katika hali kamili ambapo itanyimwa kabisa mwungano na mwili? Je, hatutambui kwamba kwa afya ya roho, afya ya mwili ni lazima? Mtu anapozeeka, na roho yake pia huzeeka; na mtu huyo anaibiwa hazina yake ya elimu na mwizi aitwaye uzee kama Asemavyo Mwenyezi Mungu:

لِكَيْلَا يَعْلَمَ مِنْۢ بَعْدِ عِلْمٍ شَيْـًٔا [1]

Yaani, mtu anapochakaa kwa uzee, hufikia hali ambapo anakuwa hajui baada ya kwisha kuelimika. Basi ushuhuda wetu ni dalili ya kutosha kwamba roho pasipo mwili si chochote wala si lolote. Tena jambo hili pia laelekeza kwenye ukweli huu hasa kwamba kama roho ingefaa bila kuwa na mwili, hapo kitendo hiki cha Mwenyezi Mungu cha kuiunganisha na mwili wenye kuangamia kingeonekana cha kipuuzi. Vile vile yafaa kuzingatia kwamba Mwenyezi Mungu Amemwumba mtu kwa ajili ya kupata maendeleo yasiyokoma. Basi kama mtu hawezi kupata maendeleo katika maisha haya mafupi bila ya kuwa na mwili, tutumainije kupata maendeleo yasiyo na mipaka vivi hivi bila kuwa na mwili?

Basi yathibitika kutokana na dalili hizi kwamba sawa na kanuni ya Kiislamu haina budi roho kuwa na mwili kwa kudumu ndipo iweze kutenda matendo kamili. Ingawaje baada ya kufa mwili huu wa kuangamia

[1] Al-Hajj, 22:6

hutengana na roho, lakini katika hali ya Barzakh kila roho huazimiwa mwili mmoja ili kuionjesha kidogo matokeo ya amali zake. Mwili huo haufanani na mwili huu; bali huo huumbika kutokana na nuru au giza sawa na vitendo vya mtu, kana kwamba katika ulimwengu huo wa Barzakh, vitendo vya mtu hufanya kazi ya mwili. Ndivyo ilivyoelezwa mara kwa mara katika Neno la Mungu; na baadhi ya miili imesemwa kuwa ni ya kinuru na mingine ya kigiza inayotengenezeka kutokana na mwanga au giza la matendo. Ingawaje siri hii ni nyepesi, lakini inaeleweka akilini. Binadamu mkamilifu huweza kupata katika maisha haya haya mwili mmoja wa nuru zaidi ya mwili wa kiwiliwili, na ipo mifano yake mingi inayoonekana katika hali ya kashfi. Ijapokuwa ni vigumu kumfahamisha habari hii mtu mwenye akili ya kawaida, lakini wale wanaowahi kupata kashfi kiasi fulani hawatastaajabu juu ya mwili huo unaoumbika kutokana na vitendo, bali watasikia ladha katika maelezo haya.

Ilmuradi, mwili huo unaopatikana katika Barzakh husababisha mwema na mwovu kupata malipo ya vitendo. Mimi binafsi ninayo maarifa hayo. Mara nyingi nimewahi kuonana na baadhi ya wafu katika hali ya kashfi nikiwa macho kabisa, nami nimejionea waovu na wapotevu kuwa na mwili mweusi sana kana kwamba umeumbika kutokana na moshi. Kwa kifupi ninao ujuzi wa dhati kuhusu habari hii, na

ninakazania kusema, kama Alivyosema Mwenyezi Mungu, kwamba kila mmoja lazima anapewa mwili baada ya kufa unaotokana na nuru au giza. Litakuwa ni kosa la binadamu ikiwa atapenda kuhakikisha maarifa haya mepesi kwa kutumia akili yake tu. Bali tambueni kwamba jinsi jicho lisivyoweza kueleza ladha ya kitu kitamu, na kama ulimi usivyoweza kuona kitu, ndivyo ambavyo zile elimu za akhera ambazo zaweza kupatikana kwa njia ya kashfi, haziwezi kutambulikana kwa kutumia akili peke yake. Mwenyezi Mungu Ameweka njia mbalimbali kwa kufahamu mambo yasiyojulikana; hivyo kitafuteni kila kitu kwa njia ile maalum iliyoweka kwa kutambua kitu hicho ndipo mtakipata.

Vile vile jambo jingine linalopaswa kukumbukwa ni kwamba Mwenyezi Mungu katika Neno lake Amewaita wale waovu waliopotea kuwa wafu, lakini wema Akawaita wazima. Ndani yake kuna siri hii kwamba walioghafilika na Mungu, baada ya kuondoka duniani wakaishiwa vifaa vya maisha yao ambavyo vilikuwa ni kula, kunywa na kufuata tamaa za nafsi, na kile chakula cha roho walikuwa hawanacho, kwa hiyo wakafa hasa; watahuishwa kwa kuonja adhabu peke yake. Kwenye siri hiyo Mwenyezi Mungu  Aliashiria Aliposema:

مَنْ يَّأْتِ رَبَّهٗ مُجْرِمًا فَاِنَّ لَهٗ جَهَنَّمَ ۗ لَا يَمُوْتُ فِيْهَا وَلَا يَحْيٰى ﴿٧٥﴾ [1]

Yaani: Amfikiaye Mungu akiwa mkosefu, makao yake ndiyo Jahanamu; hatakufa humo wala hataishi. Lakini walio wapenzi wa Mungu, hao hawafi kwani maji yao na chakula chao viko pamoja nao.

Kisha baada ya Barzakh kuna zama ziitwazo Ufufuo. Katika zama hizo kila roho, njema au mbaya, nzuri au asi, itajipatia mwili mmoja wa kuonekana hasa; siku hiyo imewekwa kwa Onyesho kamili la Mungu ambapo kila mtu atatambua dhati ya Mola wake barabara, na kila mmoja atafikia upeo wa mwisho katika malipo yake. Msistaajabu kwamba Mungu atawezaje kufanya hivyo, kwani Mungu anao uwezo wote na hufanya apendavyo jinsi Anavyosema Mwenyewe:

اَوَلَمْ يَرَ الْاِنْسَانُ اَنَّا خَلَقْنٰهُ مِنْ نُّطْفَةٍ فَاِذَا هُوَ خَصِيْمٌ مُّبِيْنٌ ﴿٧٨﴾ وَضَرَبَ
لَنَا مَثَلًا وَّنَسِيَ خَلْقَهٗ ۗ قَالَ مَنْ يُّحْيِ الْعِظَامَ وَهِيَ رَمِيْمٌ ﴿٧٩﴾ قُلْ يُحْيِيْهَا
الَّذِيْٓ اَنْشَاَهَآ اَوَّلَ مَرَّةٍ ۗ وَهُوَ بِكُلِّ خَلْقٍ عَلِيْمٌ ۙ﴿٨٠﴾ [2]

اَوَلَيْسَ الَّذِيْ خَلَقَ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضَ بِقٰدِرٍ عَلٰٓى اَنْ يَّخْلُقَ مِثْلَهُمْ ۗ
بَلٰى ۙ وَهُوَ الْخَلّٰقُ الْعَلِيْمُ ﴿٨٢﴾ اِنَّمَآ اَمْرُهٗٓ اِذَآ اَرَادَ شَيْـًٔا اَنْ يَّقُوْلَ لَهٗ
كُنْ فَيَكُوْنُ ﴿٨٣﴾ فَسُبْحٰنَ الَّذِيْ بِيَدِهٖ مَلَكُوْتُ كُلِّ شَيْءٍ وَّاِلَيْهِ تُرْجَعُوْنَ ﴿٨٤﴾ [3]

---

[1] Taa Haa, 20:75

[2] Yaa Siin, 36:78-80

[3] Yaa Siin, 36:82-84

Yaani, Je, mwanadamu hatambui ya kwamba Tumemwumba kwa tone la manii lililotiwa katika tumbo la uzazi? Lakini lo! amekuwa hasimu dhahiri. Akatupigia mfano na kusahau umbo lake, akaseme: Nani ataihuisha mifupa na hali imesagika? Waambie, Ataihuisha Aliyeiumba mara ya kwanza, naye ni Mjuzi wa kila namna ya kuumba (36:78-80). Shani ya amri yake ni kwamba anapokusudia kipatikane kitu fulani anasema tu kuwa, basi huwa. Basi ni Mtukufu ambaye anao ufalme juu ya kila kitu, nanyi nyote mtarejeshwa Kwake. Katika aya hizi, Mwenyezi Mungu Ameeleza kwamba hakuna kisichowezekana kwake. Yule aliyeumba binadamu kutokana na tone dhaifu, je atashindwa kuumba mara ya pili?

Hapa wasiojua waweza kuuliza kwamba kwa kuwa ulimwengu wa tatu, yaani Ufufuo, utawadia baada ya muda mrefu sana, kwa hiyo Barzakh itakuwa kama jela kwa kila mwema na mbaya — jambo ambalo halina maana. Jibu lake ni kwamba kufikiri hivyo ni kosa ambalo lazuka kwa sababu ya kutokuelewa. Bali sawa na Kitabu cha Mungu malipo ya mwema na mbaya yatatolewa katika mahali pawili. Kwanza katika Barzakh ambako kila mmoja atapata malipo yake kisirisiri. Waovu wataingia motoni mara baada ya kufa na wema watastarehe Peponi mara wafapo. Ziko aya nyingi ndani ya Kurani Tukufu zinazosema kwamba mtu mara akifa huanza kuona malipo ya

matendo yake. Kuhusu mja mmoja aendaye Peponi Mungu Anasema:

قِيلَ ادْخُلِ الْجَنَّةَ[1]

Yaani, akaambiwa: Ingia Peponi. Kadhalika kuhusu aendaye Motoni anasema:

فَرَآهُ فِي سَوَاءِ الْجَحِيمِ ۝٥٦[2]

Yaani: Mja mmoja alikuwa na rafiki mbaya; wote walipofariki, yule mja wa Mungu akasema yu wapi rafiki yangu? Mara akaonyeshwa yuko katikati ya Jahanamu. Kwa kifupi, thawabu na adhabu huanza mara baada ya kufa: waendao Motoni huingia Motoni na wenye Pepo huingia Peponi. Lakini baada yake, kuna siku nyingine ya Dhihirisho Kuu la Mungu aliyoweka Mwenyezi Mungu kwa hekima Yake kubwa. Kwani Yeye aliumba binadamu ili Atambulikane kuwa Mwumba. Kisha atawaangamiza wote ili Ajulikane kuwa Kahari. Kishapo Akiwapa wote uhai kamili Atawakusanya uwanjani ili Atambuliwe kwa njia ya uwezo wake. Hilo nililoeleza ni jambo la kwanza la maarifa kuhusu akhera.

## MAARIFA YA PILI

Jambo la pili lenye maarifa kuhusu akhera lililoelezwa na Kurani Tukufu ni kwamba mambo

[1] Yaa Siin, 36:27

[2] As-Saaffaat, 37:56

yote yaliyo ya kiroho katika hii dunia yatamithilika kwa sura ya kiwiliwili huko akhera, yaani katika Barzakh na pia siku ya Ufufuo. Kuhusu madhumuni hayo aya mojawapo kati ya kauli za Mwenyezi Mungu ni hii:

وَمَنْ كَانَ فِي هٰذِهِ أَعْمٰى فَهُوَ فِي الْاٰخِرَةِ أَعْمٰى وَأَضَلُّ سَبِيلًا ﴿٧٢﴾ [1]

Yaani, aliye kipofu duniani humu atakuwa kipofu huko akhera pia. Aya hii inamaanisha kwamba upofu wa kiroho katika dunia hii utaonekana na kuhisika kwa kiwiliwili katika akhera. Kadhalika katika aya nyingine Anasema:

خُذُوهُ فَغُلُّوهُ ﴿٣١﴾ ثُمَّ الْجَحِيمَ صَلُّوهُ ﴿٣٢﴾ ثُمَّ فِي سِلْسِلَةٍ ذَرْعُهَا سَبْعُونَ
ذِرَاعًا فَاسْلُكُوهُ ﴿٣٣﴾ [2]

Yaani: Mkamateni huyo mtu wa kijahanamu na tieni kola shingoni mwake kisha mwunguzeni katika Jahanamu, tena katika mnyororo wenye urefu wa dhiraa sabini mwingizeni. Itambulikane kwamba katika aya hizo, Amebainisha kwamba adhabu ya roho ya duniani humu itadhihirika kwa kiwiliwili huko akhera, na kwa hiyo kola za dunia zilizokuwa shingoni mwa mtu ambazo zilimwinamisha chini kichwa chake, zitaonekana kidhahiri. Kadhalika mnyororo wa mapenzi ya dunia utaonekana kidhahiri

---

[1] Banii Israaiil, 17:73

[2] Al-Haaqqah, 69:31-33

miguuni, na moto wa tamaa za kidunia utaonekana wazi wazi ukiwaka.

Mtu mwovu huwa na Jahanamu moja ya tamaa mbaya nafsini mwake, na anahisi kuungua katika Jahanamu hiyo wakati wa ushinde. Basi huko akhera atakapotengwa mbali na tamaa zake za kuangamia na kukata tamaa kwa kudumu, Mwenyezi Mungu atayadhihirisha majuto yake hayo kwa sura ya moto wa kiwiliwili, kama Asemavyo:

وَحِيلَ بَيْنَهُمْ وَبَيْنَ مَا يَشْتَهُونَ [1]

Yaani, kizuizi kitawekwa baina yao na yale wanayoyatamani; na hiyo ndiyo asili ya adhabu. Na kauli hii kwamba mwingizeni katika mnyororo wenye urefu wa dhiraa sabini, inamaanisha kwamba wakati mwingine mwovu anaweza kupata umri wa miaka 70, bali pengine kwa kuondoa muda wa utoto na uzee ukongwe, anapata miaka kama hiyo halisi kwa kutenda kazi za busara na bidii, lakini huyo mwenye bahati mbaya anapitisha miaka hiyo sabini ya maisha yake mazuri kwa kujinasa katika tamaa za kidunia wala hataki kujinasua katika mnyororo huo. Basi Mwenyezi Mungu anasema kwamba hiyo miaka sabini aliyoishi kwa kujinasa katika tamaa za kidunia itamithilika kidhahiri kwa sura ya mnyororo huko akhera utakaokuwa wenye urefu wa yadi sabini. Kila

---

[1] As-Sabaa, 34:55

yadi moja kwa mwaka mmoja. Tambueni hapa kwamba Mwenyezi Mungu Hampatii mtu taabu yoyote, bali Yeye Huweka tu mbele ya mtu maovu yake.

Tena Anasema Mwenyezi Mungu mahali pengine akieleza desturi yake hiyo:

اِنْطَلِقُوْٓا اِلٰى ظِلٍّ ذِىْ ثَلٰثِ شُعَبٍ ۝٣١ لَّا ظَلِيْلٍ وَّلَا يُغْنِىْ مِنَ اللَّهَبِ ۝٣٢ [1]

Yaani: Enyi waovu, wapotevu, nendeni kwenye kivuli chenye matawi matatu ambayo hayatoi kivuli wala hayafai kumkinga mtu na joto. Katika aya hii matawi matatu yanamaanisha nguvu za umbuai, unyama na kuwaza. Wale wasiorekebisha na kusawazisha nguvu hizo tatu na kuzifanya ziwe khulka njema, nguvu zao hizo zitadhihirika siku ya kiyama kwa sura ya matawi matatu yasiyo na majani yasiyoweza kumkinga mtu na joto, kwa hiyo wataungua na joto kali.

Tena, Mungu Anasema kwa kudhihirisha suna yake kuhusu wenyeji wa Peponi kwamba:

يَوْمَ تَرَى الْمُؤْمِنِيْنَ وَالْمُؤْمِنٰتِ يَسْعٰى نُوْرُهُمْ بَيْنَ اَيْدِيْهِمْ وَبِاَيْمَانِهِمْ [2]

Yaani, Siku hiyo utawaona waaminio wanaume na wanawake kwamba nuru yao iliyofichikana hapa duniani itakimbia mbele yao na kulia kwao wazi wazi.

Anasema tena katika aya nyingine:

---

[1] Al-Mursalaat, 77:31-32
[2] Al-Hadiid, 57:13

يَوْمَ تَبْيَضُّ وُجُوهٌ وَتَسْوَدُّ وُجُوهٌ ۚ [1]

Yaani, siku hiyo baadhi ya nyuso zitakuwa nyeusi na zingine nyeupe na zenye nuru. Na Anasema katika aya nyingine:

مَثَلُ الْجَنَّةِ الَّتِي وُعِدَ الْمُتَّقُونَ ۖ فِيهَا أَنْهَارٌ مِّن مَّاءٍ غَيْرِ آسِنٍ وَأَنْهَارٌ مِّن
لَّبَنٍ لَّمْ يَتَغَيَّرْ طَعْمُهُ وَأَنْهَارٌ مِّنْ خَمْرٍ لَّذَّةٍ لِّلشَّارِبِينَ وَأَنْهَارٌ مِّنْ عَسَلٍ مُّصَفًّى ۖ [2]

Yaani, Pepo watakayopewa watawa, mfano wake ni kama mfano bustani, ndani yake mna mito ya maji yasiyonuka, na mito ya maziwa yasiyoharibika ladha yake, na mito ya mvinyo ya kupendeza isiyolevya, na mito ya asali iliyo safi isiyo na uchafu. Hapa pameelezwa ya kuwa mfano wa Pepo ni huu kwamba ndani yake kuna mito ya vitu hivyo vyote isiyo na mipaka. Maji yake ya uzima anayoyanywa mja wa Mungu kwa kiroho hapa duniani yatakuwepo kidhahiri huko; na yale maziwa ya kiroho anayonyonya kwa kiroho kama mtoto mchanga yataonekana kidhahiri huko Peponi, na mvinyo ile ya mapenzi ya Mungu iliyomlevya daima kwa njia ya roho hapa duniani, itaonekana huko Peponi, na asali ya utamu wa kiimani iliyoingia kinywani mwa mja wa Mungu kwa njia ya roho, itadhihirika wazi wazi kwa sura ya mito katika Pepo. Kila mwenye kwenda

[1] Aali'Imraan, 3:107

[2] Muhammad, 47:16

Peponi atabainisha wazi wazi hali yake ya roho kwa njia ya mito yake na bustani zake, na Mungu pia siku hiyo Atajitokeza katika mapazia kwa ajili ya wenyeji wa Peponi. Ilmuradi, hali za roho hazitabaki katika uficho bali zitaonekana kwa sura ya kiwiliwili.

MAARIFA YA TATU

Jambo la tatu la maarifa ni kwamba huko akhera maendeleo hayatakomea popote na wakati wowote. Kuhusu habari hii Mwenyezi Mungu anasema:

وَالَّذِينَ آمَنُوا مَعَهُ ۖ نُورُهُمْ يَسْعَىٰ بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَبِأَيْمَانِهِمْ يَقُولُونَ رَبَّنَا
أَتْمِمْ لَنَا نُورَنَا وَاغْفِرْ لَنَا ۖ إِنَّكَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٩﴾ [1]

Yaani: Walio na nuru hapa duniani, hiyo nuru yao siku ya kiyama itakimbia mbele yao na kulia kwao. Watadumu kuomba, Ee Mungu wetu tukamilishie nuru yetu na tughofirie, hakika Wewe unao uwezo juu ya kila kitu (66:9).

Katika aya hii, kauli hii kwamba watadumu kusema tutimizie nuru yetu inaashiria kwenye kuendelea daima mbele bila kukoma wakati wowote. Ndiyo kusema kwamba watakuwa na daraja la ukamlifu wa nuru, lakini kisha wataliona daraja la juu zaidi la nuru kamili, hapo ukamilifu wa kwanza watauona kuwa mpungufu, ndipo wataomba kupatiwa hilo daraja la pili la ukamilifu wa nuru. Na pindi watakapolipata

[1] At-Tahriim, 66:9

hilo pia watadhihirikiwa na daraja la tatu la ukamilifu na hapo watauona ukamilifu wa hapo kabla kuwa si kitu na kwa hiyo watapenda kulipata hilo la tatu na kadhalika. Huo ndio upendo wa kudumu kupata maendeleo unaofahamika kutokana na neno 'Tutimizie nuru yetu.'

Ilmuradi, mtu daima atasonga mbele wala hatarudi nyuma katu. Wala wenyeji wa Peponi hawatatolewa nje ya Pepo, bali sikuzote watasonga mbele zaidi bila kurudi nyuma. Hapa swali linazuka kwamba ikiwa wamekwisha ingia tayari Peponi, kuna haja gani tena ya kuomba ghofira? Jibu lake ni kwamba tafsiri ya kweli ya neno ghofira ni kuzuia na kufunika hali pungufu isiyokamilika. Bali wenyeji wa Peponi watatamani kujipatia ukamilifu uliotimilika, wazame moja kwa moja katika nuru. Wakiona hali ya pili wataikuta hali yao ya kwanza kuwa pungufu, kwa hiyo watapenda hiyo hali ya kwanza ifunikwe chini. Kisha wakiona ukamilifu wa tatu, wataomba ghofira kuhusu hali ile ya pili, yaani watapenda hiyo hali ifunikwe chini isionekane tena. Ilmuradi, daima dawamu watatamani kupata ghofira. Hili ndilo neno la 'maghfirah' na 'istighfar' lililotumika kwa ajili ya Mtume[saw] ndani ya Kurani Tukufu ambalo wapinzani wanalipinga. Basi, sasa wasomaji bila shaka wamekwisha tambua kwamba upendo wa kuomba ghofira ndio fahari kwa mtu. Mtu aliyezaliwa kutoka tumboni mwa mwanamke kisha hazoei kuomba

ghofira ni mdudu si binadamu, ni kipofu si mwenye macho, ni mchafu si twaibu.

Kwa kifupi, basi, sawa na mafunzo ya Kurani Tukufu, Jahanamu na Pepo, zote hizo mbili, ni vivuli na athari za maisha haya ya binadamu; hakuna kitu chochote kipya cha kiwiliwili kijacho kutoka mahali pengine. Ni kweli kwamba zote mbili zitamithilika kwa sura ya kiwiliwili, lakini ni athari na vivuli vya hali za kiroho tu. Hatuamini Pepo yenye miti ya dunia hii wala Jahanamu iliyo na mawe matupu ya kiberiti. Bali sawa na imani ya Kiislamu Pepo na Jahanamu ni vivuli vya matendo anayotenda mtu duniani.

# SWALI LA TATU

## NINI SHABAHA YA MAISHA YA BINADAMU KATIKA DUNIA
## NA NI NJIA GANI YA KUIPATA?

Jawabu la swali hilo hapo juu ni kwamba ingawaje watu wenye tabia mbalimbali wanajiwekea shabaha tofauti ya maisha yao kwa sababu ya busara ndogo au moyo mdogo, na wanakomea kwenye makusudio na matamanio ya kidunia peke yake, lakini shabaha Anayoeleza Mwenyezi Mungu katika Neno lake ndiyo hii:

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنْسَ إِلَّا لِيَعْبُدُوْنِ ۝٥٧ [1]

Yaani: Sikuwaumba majinni na watu isipokuwa wanitambue na kuniabudu (51:57). Sawa na aya hii, shabaha ya kweli ya maisha ya binadamu ni kumwabudu Mwenyezi Mungu na kupata maarifa ya kumjua Yeye na kuungana naye. Ni dhahiri kwamba mtu hana madaraka ya kujiwekea shabaha hii au ile ya maisha yake, kwani binadamu haji duniani kwa kutaka wala haendi kwa kupenda: bali yu kiumbe, na Yule aliyemwumba na kumjalia vipawa vya hali ya juu kuliko wote wenye uhai, huyo Mwumba amekwisha mwekea shabaha ya maisha yake. Mtu atambue

[1] Adh-Dhaariyaat, 51:57

asitambue, lakini shabaha ya kuumbwa kwake ni kumwambudu Mwenyezi Mungu na kumjua Yeye na kujipoteza ndani yake, Asemavyo Mwenyezi Mungu ndani ya Kurani Tukufu:

إِنَّ الدِّينَ عِندَ اللَّهِ الْإِسْلَامُ ۗ [1]

فِطْرَتَ اللَّهِ الَّتِي فَطَرَ النَّاسَ عَلَيْهَا ۚ ... ذَٰلِكَ الدِّينُ الْقَيِّمُ ۙ [2]

Yaani: Dini inayofunza maarifa ya kweli ya Mungu na ibada kwa njia iliyo nzuri sana ni Islam. Na Islam imetiliwa katika tabia ya ajili ya mtu. Na Mwenyezi Mungu amemwumba mtu juu ya Islam na kwa ajili ya Islam. Ndiyo kusema, Yeye Anapenda kwamba binadamu kwa vipawa vyake vyote ashughulike katika kumwabudu na kumtii na kumpenda Yeye. Ndiyo maana, huyo Mweza Mkarimu amempatia binadamu nguvu kwa kuafikiana na Islam.

Maelezo ya aya hizo ni marefu, nami nimekwisha andika kiasi fulani katika sehemu ya tatu chini ya swali la kwanza. Lakini sasa ningependa kufafanua kwa kifupi kwamba shabaha hasa ya mtu kujaliwa viungo vya nje na vya ndani au kupewa vipawa kadha wa kadha ndiyo hii kwamba kwa njia ya kuvitumia hivyo mtu aweze kumtambua Mungu na kumwabudu na kumpenda Yeye. Ndiyo sababu licha ya mtu kujishughulisha katika maelfu ya shughuli za kidunia,

---

[1] Aali‘Imraan, 3:20

[2] Ar-Ruum, 30:31

hapati furaha ya kweli katika chochote kile minghairi ya Mungu Mwenye Enzi. Mtu hata akitajirika sana au kupata cheo cha hali ya juu au kuwa mfanya biashara mkubwa au kujipatia ufalme mkubwa au kujulikana kuwa mtaalamu sana wa falsafa, mwishowe anaondoka katika magereza hayo kwa majuto sana na daima moyo wake humlaumu juu ya kuzama kwake katika mambo ya kidunia; na dhamiri yake haimwungi mkono kamwe katika hila zake na ulaghai wake na kazi zake zisizo halali. Mtu mwenye busara anaweza kuelewa masaala haya kwa njia hii pia kwamba shabaha ya kitu fulani ni ile kazi nzuri zaidi ambayo zaidi yake kitu hicho hakiwezi kutekeleza. Mathalan, kazi nzuri zaidi ya fahali ni ukulima au kutilia maji shambani au uchukuzi; zaidi ya mambo hayo haihakikiki katika uwezo wake. Basi mambo hayo matatu ndiyo shabaha ya maisha yake, kwani hana vipawa zaidi ya hivyo. Lakini tuchunguzapo nguvu za binadamu ili kujua ni nguvu yake ipi iliyo nzuri zaidi kuliko zote zingine, twagundua kwamba mtu ana kiu ya kumtafuta Mungu Mtukufu Mwenye Enzi, na anapenda kujisahau katika Upendo wake hata kwamba asibaki na chochote kile bali kila alicho nacho kiwe cha Mungu. Binadamu anashirikiana na wanyama katika mahitaji ya lazima kama vile kula na kulala. Katika utendaji, baadhi ya wanyama wamemzidi binadamu; bali nyuki nao kwa kutoa uturi wa maua hutengeneza asali njema ambayo hadi sasa binadamu ameshindwa kuitengeneza. Bali im-

ethibitika kwamba ukamilifu wa hali ya juu wa binadamu ni kuungana na Mwenyezi Mungu; kwa hiyo, shabaha hasa ya maisha yake ni kwamba dirisha la moyo wake lipate kufunguliwa upande wa Mungu Mwenye Enzi.

## NJIA ZA KUPATA SHABAHA YA MAISHA YA MTU

Hapa swali laweza kuzuka kwamba shabaha hiyo ya mtu yawezaje kupatikana na kwa njia zipi mtu anaweza kujipatia shabaha hiyo? Basi ibainike kwamba njia kubwa zaidi ya kupata shabaha hiyo ni kumtambua Mwenyezi Mungu sawa sawa na kumwamini Mungu wa kweli. Kwani, kama hatua ya kwanza kabisa siyo sawa, na mtu amemfanya ndege au mnyama au vitu vya ardhi au mwana mtu kuwa Mungu, hapo haitumainiwi hatua za baadaye kukanyagwa katika njia iliyo sawa. Mungu wa kweli humsaidia yule anayemtafuta Yeye, lakini mfile awezaje kumsaidia mfu? Kuhusu habari hii Mwenyezi Mungu Ametoa mfano bora sana, nao ndio huu:

لَهُۥ دَعْوَةُ ٱلْحَقِّ ۖ وَٱلَّذِينَ يَدْعُونَ مِن دُونِهِۦ لَا يَسْتَجِيبُونَ لَهُم بِشَىْءٍ إِلَّا كَبَٰسِطِ
كَفَّيْهِ إِلَى ٱلْمَآءِ لِيَبْلُغَ فَاهُ وَمَا هُوَ بِبَٰلِغِهِۦ ۚ وَمَا دُعَآءُ ٱلْكَٰفِرِينَ إِلَّا فِى ضَلَٰلٍ ﴿١٥﴾ [1]

---

[1] Ar-Ra‘d, 13:15

Yaani: Apasaye kuombwa ndiye Yule Mungu wa kweli aliye na uwezo juu ya kila kitu. Na wale wanaowaomba wengine badala Yake hawawajibu chochote. Mfano wao ni kama yule anyoshaye mikono yake kwenye maji akisema, Maji we, njoo kinywani mwangu'; je, kweli maji yataingia kinywani mwake? La hasha! Basi wasiomwelewa Mungu wa kweli, maombi yao hupotea bure.

**Njia ya pili** ni kuelimika kuhusu uzuri wa Mungu uliokamilika, kwani uzuri ni kitu kinachouvutia moyo, na kuuona kunamtilia mtu mapenzi Yake moyoni. Uzuri wa Mungu Mwenye Enzi ni Umoja Wake, adhama na utukufu wake na sifa zake, kama isemavyo Kurani Tukufu:

قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ ۚ اللَّهُ الصَّمَدُ ۚ لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ ۙ وَلَمْ يَكُن لَّهُ كُفُوًا أَحَدٌ [1]

Yaani: Mungu ni Mmoja katika dhati Yake na sifa Zake na jalali Yake; hakuna mshirika Wake. Wote wanamhitaji Yeye; kila chembe hujaliwa uhai kutoka Kwake. Yu chanzo cha neema kwa vitu vyote, lakini Mwenyewe Haneemeshwi na chochote. Si mwana wala baba wa yeyote; na anawezaje kuwa hivyo ilhali hakuna yeyote wa aina Yake anayefanana Naye? Kurani Tukufu ikieleza ukamilifu Wake mara kwa mara na kuonyesha utukufu Wake imewaelekeza watu kwamba Mungu wa aina hii ndiye Azipendezaye

[1] Al-Ikhlaas, 112:2-5

nyoyo, si aliye mfu, mnyonge, mwenye huruma ndogo na uwezo kiasi.

**Njia ya tatu** iliyo ngazi ya daraja la pili kufikia shabaha ya kweli ndiyo kutambua hisani ya Mungu. Kwani yanayozalisha mapenzi ni mambo mawili tu: uzuri na hisani. Na sifa za hisani za Mungu zimeelezwa kwa kifupi katika Suuratul-Faatiha, kama Asemavyo:

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ ۝٢ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ۝٣ مٰلِكِ يَوْمِ الدِّيْنِ ۝٤ [1]

Ndiyo kusema kwamba hisani kamili ni kwamba Mwenyezi Mungu Awaumbe watu Wake pasipo kitu chochote na kisha Adumu kuwalea, Yeye Mwenyewe awe tegemeo la kila kitu. Na rehema Zake za aina zote ziwe zimedhihirika kwa ajili ya watu wake; na hisani yake iwe nyingi mno isiyohesabika. Basi Mwenyezi Mungu Ametaja mara kwa mara hisani Zake za aina hii, kama Asemavyo:

وَاِنْ تَعُدُّوْا نِعْمَتَ اللّٰهِ لَا تُحْصُوْهَا [2]

Yaani: Mkijaribu kuhesabu neema za Mwenyezi Mungu, hamtaweza kuzihesabu.

**Njia ya nne** ya kupata shabaha ya kweli iliyoelezwa na Mungu ni kuomba dua, kama Anavyosema:

---

[1] Al-Faatihah, 1:2-4

[2] Ibraahiim, 14:35

ادْعُونِي أَسْتَجِبْ لَكُمْ [1]

Yaani: Niombeni nitapokea. Mara kwa mara Amehimiza kuomba ili mtu ampate Mungu si kwa uwezo wake bali kwa uwezo wa Mungu.

**Njia ya tano** iliyoelezwa na Mungu kupata shabaha ya kweli ndiyo kujitahidi katika njia Yake; yaani amtafute Mungu kwa kutoa mali yake katika njia Yake na kutumia nguvu zake katika njia yake na kutoa uhai wake katika njia Yake na kutumia akili yake katika njia Yake, kama Asemavyo:

جَاهِدُوا بِأَمْوَالِكُمْ وَأَنفُسِكُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ [2]

وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنفِقُونَ ﴿٤﴾ [3]

وَالَّذِينَ جَاهَدُوا فِينَا لَنَهْدِيَنَّهُمْ سُبُلَنَا [4]

Yaani: Toeni mali zenu na uhai wenu na nafsi zenu pamwe na nguvu zake zote katika njia ya Mungu. Na chochote Tulichowapeni kama vile akili, fahamu, ufundi na kadhalika, toeni vyote hivyo katika njia Yake. Wanaojibidiisha kwa kila jiha katika njia Yetu, Tutawaongoza kwenye njia zetu.

---

[1] Al-Mu’min, 40:61

[2] At-Taubah, 9:41

[3] Al-Baqarah, 2:4

[4] Al-‘Ankabuut, 29:70

**Njia ya sita** Aliyoeleza ya kupata shabaha ya kweli ndiyo Uthabiti. Yaani mtu asidhoofike wala asichoke wala asiogope akijaribiwa, kama Asemavyo:

إِنَّ الَّذِينَ قَالُوا رَبُّنَا اللَّهُ ثُمَّ اسْتَقَامُوا تَتَنَزَّلُ عَلَيْهِمُ الْمَلَائِكَةُ أَلَّا تَخَافُوا وَلَا تَحْزَنُوا وَأَبْشِرُوا بِالْجَنَّةِ الَّتِي كُنتُمْ تُوعَدُونَ ﴿٣١﴾ نَحْنُ أَوْلِيَاؤُكُمْ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَفِي الْآخِرَةِ [1]

Yaani: Wale waliosema Mola wetu ndiye Allah na wakajitenga mbali na miungu ya bandia kisha wakaonyesha uthabiti, yaani wakaonyesha uimara wakati wa majaribio na taabu, hushukiwa na malaika wakisema, msiogope wala msihuzunike na furahini kwelikweli kwani mmerithi ile furaha mliyoahidiwa. Tu marafiki zenu katika maisha haya ya dunia na katika akhera. Hapa Amedokeza kwamba radhi ya Mungu hupatikana kwa kuonyesha uthabiti. Ni kweli kabisa kwamba kuonyesha uimara kunazidi kuonyesha mwujiza. Uimara kamili ni kwamba mtu akizungukwa na mabalaa pande zote nne, na kuona uhai wake na heshima yake hatarini katika njia ya Mungu, na pasikuwepo lolote la kutuliza bali hata Mungu kwa kutahini Aache kuleta kashfi, ruya na funuo za kutuliza moyo na kumwacha mtu katika hatari za kuogofya, wakati huo mtu asivunjike moyo wala asirudi nyuma kama waoga; wala asilete tofauti

[1] Haa Miim As-Sajdah, 41:31-32

katika uaminifu wake; uthabiti na uimara wake usidhoofike; afurahie dhila na kuridhika kufa; wala asimtegemee rafiki yeyote aje kumpa nguvu; wala asitamani kupata bishara za Mungu kwa sababu ya hali kuwa ngumu; na juu ya kuwa mnyonge, bila msaidizi, pasipo mwenye kutuliza, asimame wima; hata ikitokea nini, ajitolee kuwa dhabihu bila kunung'unika juu ya kadiri ya Mungu, wala asidhihirishe utukutu wala asipige kelele mpaka apate kujaribiwa ipasavyo. Huo ndio uimara unaomwezesha mtu kupata Mungu; hicho ndicho kitu kinachonukia hadi sasa katika mchanga wa makaburi ya mitume, manabii, masiddiki na mashahidi. Hiyo ndiyo hali inayoashiriwa na Mwenyezi Mungu katika dua hii:

اِهۡدِنَا الصِّرَاطَ الۡمُسۡتَقِيۡمَ ۙ‏ ۝٦ صِرَاطَ الَّذِيۡنَ اَنۡعَمۡتَ عَلَيۡهِمۡ ۙ [1]

Yaani: Ee Mungu wetu, Tuongoze njia ya imara — njia ya kuleta neema zako na radhi Yako. Amedokeza habari hiyo katika aya hii pia:

رَبَّنَآ اَفۡرِغۡ عَلَيۡنَا صَبۡرًا وَّتَوَفَّنَا مُسۡلِمِيۡنَ ۝١٢٧ [2]

Yaani: Ee Mola, katika wakati huu wa shida tuteremshie utulivu mioyoni mwetu utakaotusuburisha, na utufishe katika hali ya utii mbele Yako. Kumbukeni kwamba katika nyakati za shida na taabu, Mwenyezi

[1] Al-Faatihah, 1:6-7
[2] Al-A‘raaf, 7:127

Mungu huzishushia nyoyo za waja wake nuru moja inayowaimarisha ndipo wanakabiliana na shida zote kwa utulivu, na kwa sababu ya ladha ya imani wanaibusu minyororo wanayotiwa miguuni katika njia Yake. Mja wa Mungu anaposibiwa na mateso na alama za mauti zinapodhihirika, haanzi kugombana na Mungu ili aokolewe katika mabalaa hayo; kwani katika wakati kama huo kung'ang'ania kuomba kuokolewa ndiyo kugombana na Mungu, tena ni kinyume cha kuafikiana na Mungu kikamilifu. Bali mpenzi wa kweli husonga mbele zaidi balaa likishuka; na akiona uhai wake hauna thamani, na kwa kuagana na upendo wa uhai wake, huwa mtii mbele ya radhi ya Mola wake na hutaka kupata radhi Yake. Kuhusu hali hiyo Amesema Mwenyezi Mungu:

وَمِنَ النَّاسِ مَنْ يَشْرِي نَفْسَهُ ابْتِغَاءَ مَرْضَاتِ اللَّهِ ۗ وَاللَّهُ رَءُوفٌ بِالْعِبَادِ ﴿٢٠٨﴾ [1]

Yaani: Mpendwa wa Mungu hutoa uhai wake katika njia ya Mungu na badala yake hupata radhi Yake; hao ndio wanaopata rehema maalum ya Mungu Mwenye Enzi. Ilmuradi, uimara ule unaompatia mtu Mungu kiini chake kimeelezwa hapa. Mwenye kupenda kufahamu na afahamu

**Njia ya saba** ya kupata shabaha ya kweli ndiyo kukaa na watu wema kuiga mifano yao kamili. Itambulikane kwamba sababu mojawapo ya manabii kuletwa ni

[1] Al-Baqarah, 2:208

kwamba binadamu kitabia anahitaji mfano uliokamilika. Na mfano kamili huzidisha shauku na kutia hima. Yule asiyefuata mfano, hulegea na kupotea. Akiashiria kwenye habari hiyo Mwenyezi Mungu Anasema katika aya hii:

كُونُوا مَعَ الصَّادِقِينَ ﴿١١٩﴾ [1]

صِرَاطَ الَّذِينَ أَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ [2]

Yaani: Kaeni na wasemao kweli; jifunzeni njia ya wale walioneemeshwa kabla yenu.

**Njia ya nane** ndiyo kashfi tukufu, funuo takatifu na njozi njema. Kwa kuwa njia ya kusafiri kwa kumwendea Mungu Mwenye Enzi ni nyepesi na ngumu na ina shida na mateso ya aina mbalimbali hata kwamba yawezekana mtu apotee katika njia hii ngeni au akate tamaa na kuacha kuendelea mbele, kwa hiyo rehema ya Mungu ilipenda kumtuliza na kumhimiza na kumpa moyo na kuzidisha shauku katika safari hii. Hivyo, basi, ni suna ya Mungu kuwahusu wasafiri wa njia Yake kwamba mara kwa mara huwatuliza kwa Neno lake na ufunuo wake na kuwahakikishia Yu pamoja nao; ndipo hao kwa kupata nguvu hivyo huendelea na safari yao kwa nguvu. Kuhusu habari hiyo Mwenyezi Mungu Anasema:

---

[1] At-Taubah, 9:119

[2] Al-Faatihah, 1:7

لَهُمُ الْبُشْرٰى فِي الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا وَفِي الْاٰخِرَةِ ۚ [1]

Yaani: Watapata habari njema katika maisha ya dunia na katika akhera(10:65). Ziko njia zingine pia zilizoelezwa na Kurani Tukufu, lakini nasikitika siwezi kuzieleza kwa sababu ya nafsi ndogo niliyo nayo.

---

[1] Yuunus, 10:65

# SWALI LA NNE

## NINI ATHARI YA VITENDO KATIKA DUNIA NA AKHERA?

Nimeisha lijibu swali hilo hapo kabla kwamba athari ambayo sheria ya kweli ya Mungu iliyokamilika inaleta moyoni mwa mtu ni kumwondoa mtu katika hali ya unyama na kumfanya binadamu, kisha kumfanya mwenye khulka njema na mwishowe kumwunganisha na Mungu. Na matokeo mengine ya kutenda sawa na sheria katika maisha haya ni kwamba mtu anaanza kutambua hatua baada ya hatua hali za wanadamu wenzake na anatumia vipawa vya adili na hisani na huduma katika mahali pake; na chochote alichopewa na Mungu kama vile elimu, maarifa, mali na raha, anawashirikisha wengine katika neema hizo sawa na hali yao. Yeye huwaangaza watu wote kwa mwanga wake wote kama jua; na kama mwezi, akijipatia nuru huwafikishia wengine nuru hiyo. Aking'aa kama mchana, anawaangazia njia za mema; na kama usiku anamsitiri kila dhaifu na kuwastarehesha waliochoka. Kama mbingu, anawapa wenye haja nafasi ya kuingia katika kivuli chake, na kuwaletea mvua za neema zake katika nyakati zifaazo. Na kama ardhi, yeye kwa unyenyekevu kamili anakuwa kama sakafu kwa kumstarehesha kila mmoja, na kuwahurumia wote na

kuwapa matunda ya kiroho ya aina mbalimbali. Basi athari ya sheria kamili ndiyo hii kwamba anayeifuata sawa sawa anatimiza haki za Mungu na haki za wanadamu kikamilifu. Anapotea ndani ya Mungu na kuwa mtumishi wa kweli wa viumbe. Hiyo ndiyo athari ya kutenda sawa na sheria juu ya mtu katika maisha haya. Lakini athari yake baada ya maisha haya ndiyo hii kwamba siku hiyo mwungano wake na Mungu kiroho utadhihirika kwa sura ya kumwona Mungu wazi wazi, na huduma aliyofanya kwa viumbe kwa sababu ya mapenzi ya Mungu iliyosababishwa na imani na upendo wa matendo mema, itadhihirika kwa sura ya miti na mito ya Peponi. Kuhusu habari hii Mungu Anasema:

وَالشَّمْسِ وَضُحٰهَا ۝٢ وَالْقَمَرِ اِذَا تَلٰهَا ۝٣ وَالنَّهَارِ اِذَا جَلّٰهَا ۝٤ وَالَّيْلِ اِذَا يَغْشٰهَا ۝٥
وَالسَّمَآءِ وَمَا بَنٰهَا ۝٦ وَالْاَرْضِ وَمَا طَحٰهَا ۝٧ وَنَفْسٍ وَّمَا سَوّٰىهَا ۝٨ فَاَلْهَمَهَا
فُجُوْرَهَا وَتَقْوٰىهَا ۝٩ قَدْ اَفْلَحَ مَنْ زَكّٰىهَا ۝١٠ وَقَدْ خَابَ مَنْ دَسّٰىهَا ۝١١ كَذَّبَتْ
ثَمُوْدُ بِطَغْوٰىهَآ ۝١٢ اِذِ انْبَعَثَ اَشْقٰىهَا ۝١٣ فَقَالَ لَهُمْ رَسُوْلُ اللّٰهِ نَاقَةَ اللّٰهِ
وَسُقْيٰهَا ۝١٤ فَكَذَّبُوْهُ فَعَقَرُوْهَا فَدَمْدَمَ عَلَيْهِمْ رَبُّهُمْ بِذَنْۢبِهِمْ فَسَوّٰىهَا ۝١٥
وَلَا يَخَافُ عُقْبٰهَا ۝١٦ [1]

Yaani: Naapa kwa jua na mwanga wake, na ninaapa kwa mwezi unapoliandama, yaani unapochukua nuru ya jua na kuwafikishia wengine. Na ninaapa kwa

[1] Ash-Shams, 91:2-16

mchana unapolidhihirisha jua sawa sawa na kuangaza njia. Na ninaapa kwa usiku unapolifunika jua na kuwatandazia giza wote. Na ninaapa kwa mbingu na shabaha ya kuumbwa mbingu. Na ninaapa kwa ardhi na shabaha ya kuumbwa kwake hivyo. Na ninaapa kwa nafsi na ukamilifu wake ulioisawazisha na vitu hivyo vyote; yaani sifa zote zinazopatikana katika vitu hivyo mbalimbali, zote hizo zinakuwepo katika nafsi ya mtu mkamilifu; na huduma mbalimbali zinazoletwa na vitu hivyo kwa wanadamu, mtu mkamilifu peke yake anazitoa huduma hizo zote, kama nilivyoisha eleza hapo juu. Kisha Anasema, ameokoka mtu yule na kusalimika katika mauti, aliyejitakasa nafsi yake hivyo, yaani kwa kuzama ndani ya Mungu akawahudumia viumbe kama jua, mwezi, ardhi na kadhalika.

Kumbukeni kwamba uzima hasa maana yake ni ule uzima wa milele atakaojaliwa mtu mkamilifu baadaye. Hii inadokeza kwamba matokeo ya kutenda sawa na sheria ndiyo maisha ya milele katika akhera, ambayo yatadumu kwa chakula cha kumwona Mungu. Kisha Amesema, ameangamia yule mtu na kukata tamaa na maisha, aliyeifukia nafsi yake, na sifa kamili alizojaliwa uwezo wa kujipatia hakuzipata, bali akarejea katika hali ya kuishi maisha maovu. Kisha kimfano akasema kwamba hali ya mtu huyo ni kama hali ya Wathamudi ambao walimjeruhi ngamia jike yule aliyeitwa 'ngamia jike wa Mungu' na

kumzuia asinywe katika chemchemi yake. Habari hii inaashiria kwenye jambo hili kwamba nafsi ya mtu ndiye ngamia wa Mungu anayempanda; yaani moyo wa mtu ni mahali pa maonyesho ya Mungu. Na ngamia huyo maji yake ndiyo mapenzi ya Mungu na maarifa yake ambayo kwayo huhuika. Kisha kasema, Wathamudi walipomjeruhi ngamia huyo jike na kumnyima maji, wakashukiwa na adhabu. Na Mungu hakujali tena itakuwaje hali ya watoto wao na wajane wao baada ya kuangamia kwao. Kadhalika mtu anayemjeruhi ngamia jike wa Mungu, yaani nafsi yake na kuizuia isifikie ukamilifu wake na anainyima maji, mtu huyo ataangamia.

## HEKIMA YA MWENYEZI MUNGU KUAPA KWA VITU MBALIMBALI

Kumbukeni hapa kwamba kiapo cha Mungu kwa jua, mwezi na kadhalika kina hekima ya ndani sana ambayo kwa sababu ya kutokuijua wapinzani wetu wengi wanawahi kupinga wakisema Mungu ana haja gani ya kuapa viapo, na kwa nini ameapa kwa vitu alivyoumba. Kwa kuwa wanayo akili ya kiardhi siyo ya kimbinguni, wanashindwa kuzingatia maarifa ya kweli. Basi ibainike kwamba shabaha ya kuapa ni kwamba mwenye kuapa anataka kuleta ushuhuda kuhakikisha ukweli wa madai yake. Kwani kama mtu hapati shahidi yeyote, hapo yeye mtu huyo anaapa kwa Mungu kwa sababu Mungu akiwa mjuzi wa mambo yote ya ghaibu ndiye shahidi wa kwanza wa

kila kesi. Kana kwamba mtu huyo anamleta Mungu kuwa shahidi wake hivi kwamba ikiwa baada ya kiapo Mungu atakaa kimya bila kumwadhibu, basi itafahamika kwamba Mungu amekwisha piga muhuri kusadikisha kauli ya mtu huyo. Hii ndiyo sababu viumbe hawapaswi kuapa kwa kiumbe, kwani hakuna kiumbe aliye mjuzi wa mambo ya ghaibu wala hawezi kumwadhibu mtu kwa sababu ya kiapo chake cha uwongo. Lakini katika aya hizo, kiapo cha Mungu siyo kama anavyoapa mtu. Bali suna ya Mungu kuhusu habari hii ni kwamba kazi za Mungu ni za aina mbili: Moja, zile kazi za Mungu zilizo wazi kabisa, wote wanaweza kuzielewa, wala hakuna hitilafu yoyote katika hizo. Pili, zile kazi zisizo wazi sana ambazo kuhusu hizo watu wanafanya makosa na wanahitilafiana. Basi Mwenyezi Mungu Alitaka kuwahakikishia watu kazi zake zisizo wazi sana kwa njia ya kutaja kazi zake zilizo wazi mno.

Basi, ni dhahiri kwamba jua, mwezi, mchana, usiku, mbingu na ardhi vinazo zile sifa tulizotaja nyuma, lakini sifa kama hizo zilizomo ndani ya nafsi ya mtu, kila mtu hazitambui. Kwa hiyo Mungu ametoa ushahidi wa kazi zake zilizo dhahiri kwa kuhakikisha kazi zake zisizo dhahiri sana. Kana kwamba Anasema: Ikiwa mna shaka kuhusu kuwepo kwa sifa zilizomo katika nafsi ya mtu, basi fikirini kuhusu jua na mwezi na vinginevyo, mtazikuta sifa hizo zimo ndani ya vitu hivyo wazi wazi. Na mnajua kwamba

mtu ni ulimwengu mdogo ambaye katika nafsi yake ramani ya ulimwengu mzima imechorwa kwa ujumla. Na kama imethibitika kuwa vitu vikubwa hivyo vya ulimwengu mkubwa vinazo sifa hizo na vinawanufaisha viumbe hivyo, hapo binadamu anayehesabiwa mkuu kuliko hivyo vyote na ameumbwa akiwa na daraja la juu zaidi atawezaje kukosa hizo sifa ndani yake? Haiwezekani kabisa. Bali yeye naye anao mwanga wa kielimu na kiakili kama jua, na anaweza kuangaza dunia kwa njia ya huo mwangaza. Na kama mwezi, anapata kutoka kwa Mungu nuru ya kashfi, ufunuo na wahyi na anawafikishia wengine nuru hiyo wasiojipatia ukamilifu wa kibinadamu hadi sasa. Twawezaje, basi kukataa Unabii na kusema kwamba utume, sheria na vitabu vimesababishwa na ulaghai wa binadamu na uchoyo wake? Pia mwashuhudia kwamba mchana unapotokea, njia zote zinang’aa na miinamo na miinuko huonekana. Basi mtu mkamilifu ndiye mchana wenye mwanga na kiroho; kwa kutokea kwake kila njia hubainika; yeye huonyesha njia ya kweli iko wapi na upande gani, kwani yu mchana wa nuru ya kweli na usawa. Kadhalika mwashuhudia jinsi usiku unavyotuliza waliochoka. Wafanyakazi waliochoka na kazi ngumu ya mchana kutwa wanalala kwa furaha katika usiku na kupata raha; tena usiku pia unamsitiri kila mmoja. Ndivyo waja wa Mungu waliokamilika huja duniani kuwapa watu raha. Wenye kupata wahyi na ufunuo kutoka kwa

Mungu wanastarehesha wenye busara kwani hao wanatambua maarifa makubwa kwa urahisi sana kwa sababu ya hao waja wa Mungu. Kadhalika wahyi wa Mungu huisitiri akili ya binadamu kama usiku unavyositiri; unayaficha makosa yake mabaya yasidhihirike kwa dunia; kwani wenye busara wakipata mwanga wa wahyi wanarekebisha makosa yao na kwa baraka ya ufunuo mtukufu wa Mungu wanajiokoa katika fadheha. Ndiyo sababu mwana falsafa yeyote wa Kiislamu hakulitolea dhabihu ya jogoo sanamu lolote kama alivyofanya Pleto. Kwa kuwa Pleto hakujaliwa mwanga wa wahyi, akadanganyika; na juu ya kuwa mwana falsafa akawahi kutenda kitendo cha kuchukiza na cha kipumbavu. Lakini wana falsafa wa Kiislamu walilindwa wasitende makosa machafu ya kipumbavu kwa sababu ya kumfuata Mtume Mtakatifu[saw] Angalieni, sasa, namna ilivyothibitika kwamba ufunuo unawasitiri wenye akili kama usiku unavyositiri.

Isitoshe, mwajua kwamba waja wa Mungu waliokamilika wanampatia kivuli chao kama mbingu kila aliyechoka. Hususan Manabii wa Yule Mtukufu na wapokeao ufunuo wanawanyeshea mvua za neema kama mbingu. Kadhalika wanayo sifa ya ardhi pia. Kutoka katika dhati yao tukufu huota miti ya elimu za juu za aina mbalimbali na watu wananufaika kwa kivuli na maua na matunda ya miti hiyo. Basi, kanuni

hiyo iliyo wazi sana ya ulimwengu iliyo mbele ya macho yetu ndiyo shahidi juu ya sheria hiyo nyingine iliyofichikana na ushahidi huo umeelezwa na Mungu kwa njia ya viapo viwili katika aya hizo. Zingatieni, basi, maneno ya Kurani Tukufu yamejaa hekima namna gani yaliyotoka katika kinywa cha asiyejua kusoma na kuandika, mkazi wa jangwani. Kama hayo yasingekuwa maneno ya Mungu, akili za kawaida na wale wote wanaoitwa wataalamu wasingeyapinga kwa kushindwa kutambua maarifa yaliyomo humo. Ni kawaida kwamba mtu asipozingatia jambo fulani kwa sababu ya fahamu yake ndogo, hapo huanza kulipinga jambo hilo la hekima, na upinzani wake huhakikisha kwamba hekima hiyo inazishinda akili za kawaida, ndiyo maana wenye akili juu ya kuitwa wenye akili wakalipinga. Lakini sasa maadamu siri hii imekwisha fichuliwa, hakuna yeyote mwenye akili atakayeipinga bali atasikia ladha ndani yake.

Yapaswa kukumbuka kwamba mahali pengine pia Kurani Tukufu imeapa kiapo cha aina hiyo sawa na desturi ya kale ya wahyi na ufunuo, kwa kuleta ushahidi wa sheria ya asili ya ulimwengu, nacho ni hiki:

وَالسَّمَآءِ ذَاتِ الرَّجۡعِ ﴿١٢﴾ وَالۡاَرۡضِ ذَاتِ الصَّدۡعِ ﴿١٣﴾
اِنَّهٗ لَقَوۡلٌ فَصۡلٌ ﴿١٤﴾ وَّمَا هُوَ بِالۡهَزۡلِ ﴿١٥﴾ [1]

---

[1] At-Taariq, 86:12-15

Yaani: Naapa kwa mbingu irudishayo mvua, na naapa kwa ardhi inayopasuka kwa mvua na kutoa mimea ya aina mbalimbali, kwamba kwa hakika Kurani hii ndiyo Neno la Mungu na wahyi kutoka Kwake, ipambanuayo haki na batili wala siyo mzaha na upuuzi; yaani haikuja pasipo wakati wake bali imekuja sawa na mvua ya msimu.

Hapa Mwenyezi Mungu Ameeleza kanuni ya ulimwengu kwa sura ya kiapo kwa kuhakikisha ukweli wa Kurani Tukufu. Kwani sheria hii ya ulimwengu inajulikana daima dawamu kwamba wakati wa haja mvua hunyesha kutoka mbinguni, na ustawi wa ardhi hutegemea mvua ya mbinguni. Kama si mvua, visima vingekauka pole pole. Basi kuwepo kwa maji ya ardhini pia hutegemea mvua ya mbinguni. Ndiyo sababu mvua inaponyesha maji ya visimani pia hupanda juu. Kwa nini hupanda juu? Kwa sababu maji ya mbinguni huyavuta juu maji ya ardhini. Ndivyo wahyi wa Mungu unavyolingana na akili. Wahyi kutoka kwa Mungu, yaani ufunuo wa Mungu, ndiyo maji ya mbinguni, na akili ndiyo maji ya ardhini yanayoruzukiwa na maji ya mbinguni. Na kama maji ya mbinguni yakome, yaani wahyi usifunuliwe, hapo maji haya ya ardhini nayo yatakauka pole pole. Je, dalili hii haitoshi kuhakikisha kwamba kama kwa muda mrefu sana hazaliwi duniani mtu mwenye kupata wahyi, hapo akili za wenye akili zinachafuka na kuharibika jinsi maji ya

ardhini yanavyochafuka na kukauka? Kwa kuzingatia jambo hili, inatosha kuangalia zama za kabla ya ujaji wa Mtume[saw] Kwa kuwa miaka mia sita ilikwisha pita kutoka Masihi[as] na katika zama hizo hakuna mwenye kupata wahyi aliyezaliwa, hivyo hali ya dunia iliharibika. Historia za nchi zote zatangaza kwa uwazi kwamba katika zama za Mtume[saw], kabla ya kutumwa kwake, dunia nzima ilijaa mawazo machafu. Kwa nini ikawa hivyo na kwa sababu gani? Ni kwa sababu ufunuo haukushuka kwa muda mrefu sana. Ufalme wa mbinguni ulikuwa mkononi mwa akili peke yake. Hakuna asiyejua uharibifu uliosababishwa na akili pungufu hiyo. Angalieni, maji ya ufunuo yasiponyesha kwa muda mrefu, maji ya akili hukauka namna gani!

Hivyo, basi, katika viapo hivyo Mwenyezi Mungu Anaeleza sheria hiyo ya ulimwengu na Anasema kwamba fikirini kwa makini je, siyo sheria imara ya Mwenyezi Mungu kwamba ustawi wote wa ardhi huyategemea maji yatokayo mbinguni? Basi hiyo sheria iliyo wazi ndiyo shahidi juu ya ile sheria iliyofichikana kuhusu mfumo wa kufunuliwa wahyi. Basi jinufaisheni kwa shahidi huyo. Msiongozwe na akili peke yake, kwani hiyo siyo maji yawezayo kubaki pasipo maji ya mbinguni. Kama ilivyo sifa ya maji ya mbinguni kwamba hayo kwa vyovyote hupandisha maji ya visima vyote bila kujali mvua imepiga ndani ya kisima fulani au hapana, ndivyo

yalivyo maji ya wahyi. Mpokeaji wa wahyi anapotokea duniani, katika zama zake akili kwa jumla zinang'aa na kusafika zisivyokuwa hapo kabla, bila kujali wenye akili wanamfuta huyo mja wa Mungu au hapana. Watu huanza kujibidiisha kutafuta ukweli bila kujua, na kutoka ghaibu nguvu yao ya kufikiria hutaharukishwa. Basi, maendeleo hayo ya kiakili na jazba ya moyo hupatikana kwa sababu ya ujaji uliobarikiwa wa mwenye kufunuliwa, na huo ujaji wake hupandisha juu maji ya kiardhi. Kwa hiyo, mkiona kila mmoja ameinuka kuzichunguza dini, na maji ya kiardhi yamefurika, hapo mwinuke na kuzinduka na kutambua kwa yakini kwamba mvua kita imenyesha kutoka mbinguni na moyo wa mtu fulani umenyeshewa mvua ya Ufunuo.

# SWALI LA TANO

## NI ZIPI NJIA ZA KUPATA ELIMU YA ROHO?

Nikijibu swali hili ningependa kueleza kwamba jinsi Kurani Tukufu ilivyofafanua habari hii kwa kirefu, hapa sina nafasi ya kutaja kikamilifu, lakini nitatoa maelezo kiasi fulani kama mfano.

Ifahamike basi kwamba Kurani Tukufu imegawanya elimu katika sehemu tatu: Ilmul-yakin (Elimu ya yakini), Ainul-yakin (Jicho la Yakini) na Hakkul-yakin (Ukweli wa Yakini). Kama nilivyoeleza nyuma kwa kutoa maelezo ya Sura Takaathur, Ilmul-Yakin (Elimu ya Yakini) ni kugundua kitu fulani, si moja kwa moja bali kwa njia fulani. Kwa mfano twasema penye moshi pana moto. Ijapokuwa twauona moshi tu, sio moto, lakini tunaamini moto upo pale penye moshi. Na kama tumekwisha ona moto wenyewe, hilo ni daraja la pili la elimu iitwayo Ainul-yakin (Jicho la Yakini) sawa na Sura Takaathur ya Kurani Tukufu. Na tukiisha ingia katika moto huo, tutapata daraja la tatu la elimu, yaani Hakkul-Yakin (Ukweli wa Yakini). Haina haja ya kurudia tena Sura At-Takaathur; wasomaji waweza kusoma nyuma pale ilipoelezwa.

Sasa mwapaswa kujua kwamba namna ya kwanza ya elimu, yaani Ilmul-Yakin, hupatikana kwa njia ya

akili na kujulishwa na wengine. Mwenyezi Mungu Anaeleza kwamba waendao Motoni watasema:

وَقَالُوا لَوْ كُنَّا نَسْمَعُ أَوْ نَعْقِلُ مَا كُنَّا فِي أَصْحَابِ السَّعِيرِ ﴿١١﴾ [1]

Yaani, waendao Jahanamu watasema, kama tungetumia akili kwa kuchunguza ukweli wa dini na imani au kuzingatia maandishi au maneno ya wenye akili kamili na wachunguzi, tusingeingia leo Motoni (67:11). Aya hii inaafikiana na aya ifuatayo:

لَا يُكَلِّفُ اللَّهُ نَفْسًا إِلَّا وُسْعَهَا [2]

Yaani, Mwenyezi Mungu haikalifishi nafsi yoyote zaidi ya uwezo wake wa kielimu, na anamtaka mtu kukubali ile itikadi iliyo katika uwezo wake wa kufahamu ili amri yake isiingie katika mambo yasiyowezekana. Aya hizo pia zaashiria kwamba mtu kwa masikio pia aweza kujipatia Ilmul-Yakin, yaani elimu ya yakini. Kwa mfano, sisi hatukuona London, bali tumesikia tu habari zake kutoka kwa waliouona mji huo. Je, twaweza kuwashuku wote hao kuongopa? Au kwa mfano hatukuwa katika zama za mfalme Alamgir wala hatukuona sura yake; lakini je, twaweza kutia shaka kwamba zamani Alamgir aliyekuwa Mfalme wa Kimoghal hakupatikana? Hapana. Tumepataje yakini kwamba kweli alipita zamani

[1] Al-Mulk, 67:11
[2] Al-Baqarah, 2:287

Mfalme huyo? Jibu lake ni kwamba kwa kusikiliza habari zake mfululizo. Basi hapana shaka kwamba kusikia pia hufikisha kwenye daraja la Elimu ya Yakini. Vitabu vya Manabii pia vinatoa elimu ile ya kupatikana kwa kusikia sharti mnyororo wa kusimuliwa kwake usiwe na pengo lililoingia. Lakini kama kitabu fulani kinadaiwa kufunuliwa, lakini chenyewe kimesimuliwa kwa njia hamsini au sitini mbalimbali ambazo kila moja katika hizo inazipinga zingine, hapo ingawaje kundi fulani limeamini kwamba kati ya hizo, mbili, tatu au nne ziko sahihi na zingine zimezushwa tu, lakini mchunguzi ataona ni upuuzi tu hiyo yakini ambayo haikupatikana katika msingi wa uchunguzi kamili, na matokeo yake ni kwamba aina zote za kitabu hicho kwa sababu ya kupingana hizo kwa hizo zitahesabiwa bure wala hazitategemewa. Wala haitajuzu kuyahesabu masimulizi hayo yote kuwa njia ya kupata elimu yoyote. Maana kifafanuzi cha Elimu ni kutoa ujuzi wa yakini; lakini lundo la maneno yanayopinzana haliwezi kuwa na maarifa yoyote ya yakini.

Hapa yapasa kukumbuka kwamba Kurani Tukufu haiishii kwenye kusikia tu, kwani ndani yake mna dalili nzito nzito za kiakili. Itikadi, sheria na amri zote zilizotolewa na Kurani Tukufu, hata moja katika hizo haikukubalishwa kwa nguvu, kwani imeisha sema itikadi zote hizo zimetiliwa mapema katika tabia ya

asili ya binadamu. Kwa hiyo Kurani Tukufu huitwa Dhikr, yaani kumbukumbu kama Asemavyo:

هٰذَا ذِكۡرٌ مُّبٰرَكٌ [1]

Yaani, hii Kurani yenye baraka haikuleta chochote kigeni, bali hukumbusha tu yale yaliyojaa mapema katika tabia ya asili ya mtu na daftari ya sheria ya ulimwengu. Yasema tena mahali pengine:

لَآ اِكۡرَاهَ فِى الدِّيۡنِ [2]

Yaani, Dini hii haimshurutishi mtu kuamini, bali inaeleza kila jambo kwa dalili. Isitoshe, Kurani inayo sifa ya kiroho ya kuangaza nyoyo, kama isemavyo:

شِفَآءٌ لِّمَا فِى الصُّدُوۡرِ [3]

Yaani, Kurani inayo sifa ya kuponya maradhi yote. Kwa hiyo hatuwezi kusema kwamba Kurani inatoa elimu kwa njia ya kusikia tu, bali inatoa pale pale hoja za kiakili za hali ya juu na ndani yake mna nuru ing'aayo.

Kadhalika, hoja za kiakili zinazothibitika kutokana na maelezo sahihi zinafikisha mtu hadi kwenye Elimu ya Yakini. Jambo hili limedokezwa na Mwenyezi Mungu katika aya zifuatazo:

---

[1] Al-Anbiyaa, 21:51
[2] Al-Baqarah, 2:257
[3] Yuunus, 10:58

إِنَّ فِي خَلْقِ السَّمٰوٰتِ وَالْأَرْضِ وَاخْتِلَافِ الَّيْلِ وَالنَّهَارِ لَاٰيٰتٍ لِّأُولِي
الْأَلْبَابِ ﴿١٩٠﴾ الَّذِينَ يَذْكُرُونَ اللَّهَ قِيٰمًا وَّقُعُودًا وَّعَلٰى جُنُوبِهِمْ وَيَتَفَكَّرُونَ فِي خَلْقِ
السَّمٰوٰتِ وَالْأَرْضِ ۚ رَبَّنَا مَا خَلَقْتَ هٰذَا بَاطِلًا ۚ سُبْحٰنَكَ فَقِنَا عَذَابَ النَّارِ ﴿١٩١﴾ [1]

Yaani: wenye busara na akili wanapotafakari kwa makini muundo wa ardhi na sayari za mbinguni na sababu za kupungua usiku na mchana, wanapata dalili juu ya kuwepo kwa Mwenyezi Mungu kwa kuchunguza mfumo huu wote. Hapo hao wanataka kusaidiwa na Mungu kupata mwangaza zaidi, nao wanamkumbuka wakiwa wamesimama, wamekaa na kulala kibavubavu, na kwa njia hiyo akili zao husafika sana. Basi kwa kutumia akili hizo nzuri wanapotafakari katika muundo bora wa sayari za mbinguni na ardhi, mara wanakiri kwamba mfumo huu kamili na imara sio bure usio na faida yoyote, bali hudhihirisha usu wa Mwumba wa kweli. Hapo baada ya kukiri Uungu wa Mwumba wa ulimwengu, huomba wakisema: Ee Mola, Umeepukana na kukanwa na kusifiwa kwa sifa zisizofaa; basi Tuokoe katika Moto wa Jahanamu. Yaani kukukukana ndio moto wa Jahanamu, na kukutambua kuna raha na starehe zote. Yule aliyenyimwa kukutambua hasa, kwa hakika yuko motoni katika dunia hii hii.

[1] Aali'Imraan, 3:191-192

UHAKIKA WA UMBlLE LA MTU

Kadhalika njia nyingine ya kupata elimu ndiyo Dhamiri ya binadamu ambayo huitwa Umbile ndani ya Kurani Tukufu, kama Asemavyo Mwenyezi Mungu:

فِطۡرَتَ اللّٰهِ الَّتِیۡ فَطَرَ النَّاسَ عَلَیۡهَا ؕ [1]

Yaani: Ndilo umbile Mwenyezi Mungu Alilowaumbia watu (30:31). Nakshi hiyo ya Umbile ni nini? Ni kukiri kwamba Mungu ni Mmoja, hana mshirika, ni Mwumba wa kila kitu, ameepukana na kufa na kuzaliwa. Tunaihesabu Dhamiri kuwa njia ya kutoa elimu ya yakini, kwani ijapokuwa katika dhamiri siyo kwamba elimu moja inaongoza kidhahiri kwenye elimu nyingine kama vile elimu ya kuwepo moshi huongoza kwenye elimu ya kuwepo Moto, lakini hata hivyo katika habari ya Dhamiri ndani kwa ndani sifa hii ipo. Ni hivi kwamba Mwenyezi Mungu amekipa kila kitu sifa fulani maalum ambayo haielezeki kwa maneno, lakini kwa kukiangalia au kukiwaza hicho kitu, mara fahamu inaongozwa kwenye hiyo sifa. Yaani sifa hiyo inaambatana na kitu hicho jinsi moshi unavyoambatana na moto. Kwa mfano, tunapotafakari kuhusu dhati ya Mungu kwamba Mungu Anapaswa kuwa namna gani, je Azaliwe kama sisi na kuudhika kama sisi na Afe

[1] Ar-Ruum, 30:31

kama sisi, tunaona tunaudhika kwa kuwaza hivyo na dhamiri yetu inatetemeka na inahamaki sana kana kwamba inafukuzilia mbali wazo hili na inasema kwamba Yule Mungu ambaye matamanio yote yanazitegemea nguvu Zake anapaswa kuepukana na kila kasoro, na awe mtakatifu, mkamilifu na mwenye nguvu. Na pindi tuwazapo Mungu, mara tunahisi ufugamano makamilifu baina ya Mungu na Umoja Wake jinsi moshi na moto vinavyofungamana, bali zaidi sana kuliko uhusiano ulio baina ya moshi na moto. Hivyo, elimu tunayopata kwa njia ya dhamiri yetu ndiyo elimu ya daraja la Elimu ya Yakini. Lakini lipo daraja la juu yake pia liitwalo Ainul-Yanin, yaani Jicho la Yakini. Daraja hili linamaanisha kwamba baina ya yakini yetu na kitu tulichotambua kwa yakini kusipatikane kitu kingine chochote, Mathalan, tunapogundua harufu njema au mbaya kwa nguvu yetu ya kunusa, au utamu au chumvi kwa nguvu ya kuonja, au kitu cha moto au baridi kwa hisia yetu, hizo elimu zetu zote huingia katika Ainul-Yakin (Jicho la Yakini).

Lakini kuhusu akhera elimu yetu inafikia daraja la Ainul-Yakin pale ambapo tunapata ufunuo moja kwa moja na tunasikia sauti ya Mungu kwa masikio yetu na kushuhudia kashfi safi na sahihi za Mungu kwa macho yetu. Hapana shaka kwamba tunahitaji kupata ufunuo moja kwa moja kwa kupata maarifa kamili. Na twasikia moyoni mwetu kiu na njaa ya maarifa

hayo. Kama Mwenyezi Mungu hakutuwekea njia za kupata maarifa hayo, kwa nini ametia kiu na njaa yake moyoni mwetu? Je, twaweza kuridhika kwamba katika maisha yetu haya, ambayo ndiyo kipimo cha pekee kwa akhera, tumwamini Mungu wa kweli, Mkamilifu, Muweza na Hai wa milele kwa kusikia visa na hekaya peke yake, au tutosheke na maarifa ya kiakili tu ambayo hadi sasa ni mapungufu na yenye kasoro? Je, wapenzi wa kweli wa Mungu hawapendi kusikia ladha ya kuongea na Mpendwa huyo? Je, wale ambao kwa ajili ya Mungu waliachana na dunia nzima, wakatoa mioyo yao na uhai wao, wanaweza kuridhika kuendelea kufa kwa kushinda katika mwanga wa utusitusi bila kuona Jua lenyewe la Ukweli? Je, si kweli kwamba tamko moja tu la Mungu Aliye Hai la kusema "Nipo" linampa mtu daraja lile la maarifa ambalo mbele yake vitabu vyote walivyotunga wataalamu wote wa falsafa wa dunia nzima si chochote wala si lolote? Waliobaki vipofu juu ya kuitwa wataalamu wa falsafa watatufundishaje? Ilmuradi, kama Mwenyezi Mungu amekusudia kuwapa maarifa watafuta ukweli, lazima ameacha wazi njia ya wahyi na ufunuo. Kuhusu habari hii Mwenyezi Mungu Anasema ndani ya Kurani Tukufu:

اِهۡدِنَا الصِّرَاطَ الۡمُسۡتَقِيۡمَ ۙ﴿۶﴾ صِرَاطَ الَّذِيۡنَ اَنۡعَمۡتَ عَلَيۡهِمۡ ۙ [1]

---

[1] Al-Faatihah, 1:6-7

Yaani: Ee Mungu, tuonyeshe njia ya usimeme iliyo njia ya walioneemeshwa nawe. Hapa neema inamaanisha ufunuo, kashfi na elimu za roho anazopata mtu moja kwa moja. Kadhalika Anasema mahali pengine:

إِنَّ الَّذِينَ قَالُوا رَبُّنَا اللَّهُ ثُمَّ اسْتَقَامُوا تَتَنَزَّلُ عَلَيْهِمُ الْمَلَٰٓئِكَةُ
أَلَّا تَخَافُوا وَلَا تَحْزَنُوا وَأَبْشِرُوا بِالْجَنَّةِ الَّتِي كُنتُمْ تُوعَدُونَ ﴿٣١﴾ [1]

Yaani: Wale wanaoimarika sawa sawa baada ya kuamini Mungu, hushukiwa na malaika wa Mungu Mwenye Enzi na kuwafunulia: Msiogope wala msihuzunike. Mmewekewa Pepo mliyoahidiwa. Katika aya hii pia imeelezwa kwamba waja wa Mungu watapata ufunuo wakati wa hofu na huzuni, na Malaika watawatuliza kwa kuwashukia. Kisha Asema tena katika aya nyingine:

لَهُمُ الْبُشْرَىٰ فِي الْحَيَوٰةِ الدُّنْيَا وَفِي الْآخِرَةِ ۚ [2]

Yaani: Marafiki wa Mungu hupata habari njema kwa njia ya wahyi na Ufunuo katika dunia hii na pia huko Akhera.

## MURADI WA UFUNUO

Tambueni hapa kwamba ufunuo haumaanishi wazo lolote linalozuka moyoni mwa mtu jinsi ambavyo

---

[1] Haa Miim As-Sajdah, 41:31

[2] Yuunus, 10:65

mshairi anapojaribu kutunga shairi na anapokwisha tunga msitari mmoja anatafakari ndipo msitari wa pili unatiliwa moyoni mwake. Kutiliwa huku moyoni sio Ufunuo, bali ni matokeo ya fikara ya mtu sawa na kanuni ya kawaida. Mtu anapotafakari katika mambo mema au mabaya, hutiliwa moyoni mwake jambo sawa na fikira zake. Kwa mfano kuna mtu mwema na mkweli anayetunga beti kadha kuusaidia ukweli, na kuna mwingine aliye mbaya na mchafu anayesaidia uwongo kwa kutunga mashairi ya kuwatukana wakweli. Bila shaka wote hao wawili wataweza kutunga beti kadha; bali yawezekana huyo mwovu, kwa sababu ya mazoea ya sikuzote, aweze kutunga kwa ufasaha zaidi. Basi kama ufunuo ni kutiliwa tu moyoni neno fulani, hapo mshairi huyo mwovu aliye adui wa ukweli na wakweli na daima anaandika kupinga haki na kuzusha uzushi, atahesabiwa kuwa Mpokea Ufunuo. Mnajua kwamba watu wanatunga vitabu vya hadithi za kubuniwa, lakini wanaandika kwa fasaha sana visa mfululizo wanavyotiliwa moyoni kwa sababu ya kutafakari. Je, visa hivyo vyaweza kuitwa ufunuo? Kama ufunuo ni kutiliwa tu moyoni wazo fulani, basi hapo hata mwizi anaweza kuitwa Mpokeaji Ufunuo, kwani mara nyingi kwa kutafakari yeye hugundua njia za ajabu za kutoboa ukuta wa nyumba za watu na kuwaibia, na anawaza njia mbalimbali za ujambazi na mauji pasipo haki. Je, yatupasa kuziita njia hizo zote chafu kuwa Ufunuo? La, hasha! Bali hilo ni wazo la wale ambao hadi sasa

hawajapata habari ya Mungu wa kweli Anayetuliza nyoyo kwa ufunuo Wake na kuwapatia wasioelimika maarifa kutokana na elimu za roho.

Ufunuo ni nini, basi? Ni maongezi ya Mungu Mtukufu Mwenye uwezo na mja Wake mteule au na yule anayekusudiwa kufanywa mteule, kwa maneno yaliyo hai na yenye nguvu. Basi, maongezi hayo ya kutosha na ya kutuliza yakianza kufululiza yasiyo na giza la mawazo machafu wala siyo maneno machache yasiyo na maana bali ni maneno matamu yaliyojaa hekima na shani, ndiyo maneno ya Mungu Anayomfunulia mja Wake kwa kumtuliza na kujidhihirisha kwake. Naam, wakati mwingine ufunuo huwa kwa kumjaribu mtu, hapo hauna baraka ndani yake wala ukamilifu. Shabaha yake ni kumtahini mtu katika hali yake ya mwanzo kwamba yeye mtu huyo baada ya kuonja ufunuo kidogo anasawazisha hali yake na matamshi yake sawa na hali ya wapokeaji wa kweli wa ufunuo ama anateleza. Basi asiposhika ukweli kama walio wakweli hasa, ananyiwa neema hii kukamilika na anabaki na majivuno peke yake. Mamilioni ya watu wema waliendelea kupata ufunuo, lakini cheo chao si cha daraja moja mbele ya Mungu, bali hata manabii watukufu wa Mungu wanaopata ufunuo wazi wazi katika daraja la kwanza kabisa nao hawana cheo kimoja. Mungu Mwenye Enzi Anasema:

تِلْكَ الرُّسُلُ فَضَّلْنَا بَعْضَهُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ [1]

Yaani: Hao mitume Tumewafadhili baadhi yao kuliko wengine. Hii inahakikisha kwamba ufunuo ni fadhili tupu ya Mungu na siyo dalili ya ubora wa mtu. Bali ubora unalingana na kiasi cha ukweli, ikhlasi na uaminifu Anachojua Mungu Mwenyewe. Naam, ufunuo pia ukiwa pamoja na masharti yake yenye baraka, ndiyo tunda la hizo. Hakuna shaka kwamba ikiwa ufunuo unafunuliwa hivi kwamba mja wa Mungu anamwuliza Mungu jambo fulani na Mungu anamjibu mja Wake, na maongezi yapatikane kwa mpango, na ndani ya ufunuo huo adhama na nuru ziwepo, tena ufunuo huo uwe na elimu ya ghaibu ndani yake au maarifa ya kweli, hapo ufunuo huo unakuwa Maneno ya Mungu. Ni lazima kwa ufunuo wa Mungu kwamba jinsi rafiki mmoja anavyozungumza na rafiki yake pindi wanapokutana, ndivyo maongezi yapatikane baina ya Mola na mja Wake. Mtu akiuliza Jambo, asikie jawabu lake kutoka kwa Mungu kwa maneno matamu yenye ufasaha yasiyoingiliwa na mawazo na fikira za nafsi yake, na maongezi hayo yawe kipaji kwake, basi huo ndio ufunuo kutoka kwa Mungu. Na mtu wa aina hii ndiye mpenzi wa Mungu. Lakini daraja la kupata ufunuo kama kipaji na mtu daima kupata ufunuo hai na safi na mtukufu kutoka kwa Mungu, halipatikani kwa

[1] Al-Baqarah, 2:254

yeyote isipokuwa wale wanaopata maendeleo katika imani, ikhlasi, matendo mema na kile tusichoweza kueleza. Ufunuo wa kweli na mtukufu huonyesha maajabu ya Uungu. Mara nyingi huzalika nuru ing'aayo sana na pale pale ufunuo wenye shani ung'aao huteremka. Kuna neema gani kubwa kuliko hii kwamba mpokeaji ufunuo anaongea na Mwumba wa mbingu na ardhi. Kumwona Mungu katika dunia hii ndiyo kuzungumza naye. Lakini hiyo haimaanishi ile hali ya mtu ambaye midomoni mwake limetamkika ghafula neno au fungu la maneno au ubeti pasipo kuongea na Mungu; mtu huyo anajaribiwa na Mungu. Kwani Mungu wakati mwingine Anawatahini wazembe na wavivu kwa kumtilia mtu moyoni au kinywani mwake fungu au mafungu ya maneno, na huyo mtu anakuwa kama kipofu asitambue hayo yametoka wapi; kutoka kwa Mungu au Shetani! Basi mtu akifunuliwa hivyo, anapaswa kuomba ghofira. Lakini kama mtu mwema akianza kufunuliwa na Mungu moja kwa moja na akasikia kwa njia ya maongezi maneno safi, matamu, yenye maana, yaliyojaa hekima kwa shani yote; na mara nyingi amewahi kujibizana na Mungu katika hali ya kuwa macho kwa akali mara kumi, yaani kauliza na akajibiwa, na kisha wakati huo huo katika hali ya kuwa macho akamwuliza jambo lingine naye Akamjibu, kisha akaomba na akajibiwa na Mungu, na kwa njia hiyo akaongea na Mungu mara kumi katika kipindi kile kile kimoja; na mara nyingi Mungu

akapokea maombi yake na kumjulisha maarifa mema, na kumpasha habari za mambo yatakayotokea baadaye, na kumbariki na maongezi yake wazi wazi bila pazia, mtu huyo anapaswa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu na kujitolea sana kuliko wengine wote katika njia ya Mungu, kwani Mungu Amemchagua kati ya watu wake wote na kumfanya awarithi Masiddiki waliopita kabla yake. Neema hii hupatikana kwa nadra na ni bahati njema tu mtu kuipata; kwake vitu vyote vingine havina thamani tena.

## SIFA MAALUM YA ISLAM

Katika Islam, watu wa aina hii wamedumu kupatikana. Ni Islam peke yake ambayo ndani yake Mungu Anamsogelea mtu na kuongea naye, na Anatengeneza Kiti chake cha Enzi katika moyo wake na kumvuta juu upande wa mbinguni kutoka ndani yake, na kumpatia neema zote zile walizopewa watu wa zamani. Nasikitika kwamba dunia iliyopofuka haitambui kwamba mtu akisogea karibu na Mungu pole pole hufikia mpaka wapi. Wenyewe hawakanyagi hatua mbele, na yule anayekanyaga mbele anakufurishwa au anaanza kuabudiwa na kufanywa Mungu. Yote hayo mawili ni dhuluma: moja inasababishwa na kupita kiasi na nyingine kwa sababu ya kupunguza. Lakini mwenye busara anapaswa asipungukiwe hima wala asikane cheo hicho na daraja hilo wala asikose adabu mbele ya mwenye daraja hilo wala asianze kumwabudu.

Katika daraja hili Mwenyezi Mungu Anadhihirisha uhusiano Wake na mja Wake hivi kwamba Anamfunika na shuka la Uungu Wake na mtu anakuwa kioo kwa kumwona Mungu. Ndiyo siri aliyoeleza Mtume wetu[saw] aliposema: 'Aliyeniona, amemwona Mungu'. Ilmuradi hiyo ni ilani ya mwisho kwa watu. Na madaraja yote yanaishia hapo na mtu hutulia kikamilifu.

## MSEMAJI AMEJAALIWA KUPATA UFUNUO

Nitawadhulumu wanadamu wenzangu nisipotoboa kwamba cheo hicho nilichofafanua sasa hivi na daraja hilo la kupata kufunuliwa na Mungu nililoeleza, nimejaliwa hilo na Mungu Mpaji, ili niwafumbue macho vipofu na kuwajulisha watafutao kile kilichopotea, na kuwapasha wapokeao ukweli habari njema ya ile chemchemi tukufu wanayoitaja wengi lakini huipata wachache. Ninawahakikishia wasikilizaji kwamba Yule Mungu wa kumwokoa mtu na kumjalia furaha ya daima hapatikani bila kuifuata Kurani Tukufu. Laiti watu wangeliona nilichoona mimi na kusikia nilichosikia, na kuviacha visa bali kuukimbilia uhakika. Elimu kamili ionyeshayo Mungu, maji yasafishayo uchafu yanayoondolea mbali shaka zote, kioo ambamo Anaonekana Mungu Mwenye Enzi Mtukufu, ni ufunuo huo nilioisha eleza sasa hivi. Mwenye roho yenye kiu ya kutafuta ukweli ainuke na kutafuta. Nawaambieni kweli kweli kwamba kama roho zingekuwa na kiherehere na

mioyo ingekuwa na kiu ya kweli, watu wangejishughulisha kuitafuta njia hiyo. Lakini njia hiyo itajulikanaje? Na pazia litaondolewa na dawa gani? Nawahakikishia watafuta ukweli wote kwamba ni Islam peke yake inayotoa habari njema ya njia hiyo; mataifa mengine yameisha upiga muhuri Ufunuo tangu muda mrefu. Tambueni kabisa kwamba huo sio muhuri uliopigwa na Mungu, bali mtu hutafuta hila kwa sababu ya kunyimwa au tuseme kupungukiwa busara. Pia tambueni kabisa kwamba jinsi ambavyo haiwezekani kuona bila macho na kusikia bila masikio na kutamka bila ulimi, ndivyo hivyo isivyowezekana kuona uso wa Mpendwa Huyo bila kuifuata Kurani. Nilikuwa kijana, sasa ni mzee, lakini sijamkuta yeyote aliyekinywa kikombe cha maarifa wazi wazi ya Mungu bila kuchota katika chemchemi hii tukufu.

## NJIA YA KUPATA ELIMU KAMILI NI UFUNUO WA MUNGU

Enyi wapenzi, hakuna mtu awezaye kugombana na Mungu kuhusu mipango Yake. Fahamuni kabisa kwamba njia ya elimu kamili ni ufunuo wa Mungu waliopata Manabii watukufu wa Mungu. Kisha Mungu ambaye ni Mto wa neema hakupenda katu kuupiga muhuri Ufunuo na kuiangamiza dunia kwa njia hii; bali milango ya ufununo wake na maongezi Yake ipo wazi daima dawamu. Naam, itafuteni hiyo kwa njia zake maalum, ndipo mtaipata kwa urahisi.

Maji hayo ya uzima yameteremka kutoka mbinguni na yametulia katika mahali pafaapo. Sasa mwapaswa kufanya nini hata muweze kuyanywa maji hayo? Ni kwamba mnatakiwa mwifikie chemchemi hiyo kwa vyovyote na kuweka kinywa mbele ya chemchemi hiyo ili mtosheke na mail ya uzima. Wema wa mtu ndio kupakimbilia penye mwanga na kifuata njia iliyo na alama za Rafiki yake Aliyepotea. Mwashuhudia kwamba daima nuru hushuka kutoka mbinguni juu ya ardhi, kadhalika nuru ya kweli ya mwongozo pia hushuka kutoka mbinguni. Maneno ya mtu na werevu wake haviwezi kumpatia maarifa ya Mungu. Je, mwaweza kumpata Mungu pasipo Yeye kujidhihirisha? Je, mwaweza kuona gizani bila mwanga wa mbinguni? Kama mnaweza kuona bila mwanga, pengine mwaweza kumwona pia. Lakini hata kama macho yetu ni sawa, yanahitaji mwanga wa mbinguni; na hata kama masikio yetu yaweza kusikia, yanahitaji upepo unaovuma kutoka kwa Mungu. Si Mungu wa kweli akaaye kimya na kuzitegemea akili zetu zimgundue. Bali Mungu kamili aliye Hai ndiye Yule aliyejijulisha Mwenyewe dhati Yake zamani na sasa pia amependa Mwenyewe Ajijulishe kwa watu. Madirisha ya Mbingu yanakaribia kufunguliwa; na asubuhi ipo karibu kupambazuka. Wamebarikiwa wale wanaozinduka na kumtafuta sasa Mungu wa kweli — naam, Yule Mungu asiyepatwa na taabu na shida, ambaye mwanga wa Jalali Yake haufifii. Mwenyezi Mungu Anasema ndani ya Kurani Tukufu:

اَللّٰهُ نُوْرُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ؕ [1]

Yaani: Ni Mungu aliye nuru ya mbingu na nuru ya ardhi wakati wote. Yeye ndiye Anapaangaza pahali pote; ndiye Jua la jua; ndiye uhai wa viumbe vyote. Ndiye Mungu wa kweli. Amebarikiwa anayemkubali Yeye.

NJIA YA TATU ya kupata elimu ni mambo yale yaliyo katika daraja la Hakkul-Yakin (Haki ya Yakini). Nayo ni shida, misiba na mateso yanayowasibu Manabii wa Mungu na wakweli kwa mikono ya wapinzani au kwa kadiri ya mbinguni. Na kwa njia ya mateso hayo na taabu hizo, maagizo yote ya sheria yaliyokuwa moyoni mwa mtu kwa sura ya kielimu tu yapata sura ya vitendo, na kisha yakistawi katika ardhi ya vitendo hufikia ukamilifu mtimilifu. Na dhati ya watendao huwa kitabu kamili cha miongozo ya Mungu; na khulka zote za kusamehe na kulipiza kisasi, subira na huruma na kadhalika zilizokuwa zimejaa ubongoni na moyoni tu sasa sehemu zote za mwili zinapata hisa zake kwa sababu ya baraka za kufululiza kutenda, na kwa kuushukia mwili mzima hutia nakshi zake mle ndani yake, kama Asemavyo Mwenyezi Mungu:

وَلَنَبْلُوَنَّكُمْ بِشَيْءٍ مِّنَ الْخَوْفِ وَالْجُوْعِ وَنَقْصٍ مِّنَ الْاَمْوَالِ وَالْاَنْفُسِ
وَالثَّمَرٰتِ ؕ وَبَشِّرِ الصّٰبِرِيْنَ ﴿۱۵۶﴾ الَّذِيْنَ اِذَآ اَصَابَتْهُمْ مُّصِيْبَةٌ ۙ قَالُوْٓا اِنَّا لِلّٰهِ وَاِنَّآ

[1] An-Nuur, 24:36

إِلَيْهِ رَاجِعُونَ ﴿١٥٧﴾ أُولَٰئِكَ عَلَيْهِمْ صَلَوَاتٌ مِنْ رَبِّهِمْ وَرَحْمَةٌ ۖ وَأُولَٰئِكَ هُمُ الْمُهْتَدُونَ ﴿١٥٨﴾ [1]

لَتُبْلَوُنَّ فِي أَمْوَالِكُمْ وَأَنْفُسِكُمْ وَلَتَسْمَعُنَّ مِنَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ مِنْ
قَبْلِكُمْ وَمِنَ الَّذِينَ أَشْرَكُوا أَذًى كَثِيرًا ۚ وَإِنْ تَصْبِرُوا وَتَتَّقُوا فَإِنَّ ذَٰلِكَ مِنْ
عَزْمِ الْأُمُورِ ﴿١٨٧﴾ [2]

Yaani: Tutawajaribuni kwa jambo la hofu na kwa njaa na kwa upungufu wa mali na uhai na kwa kupotewa na juhudi na kufiwa na kizazi. Yaani shida hizo zote zitawasibuni kwa kadiri ya Mungu au kwa mikono ya maadui. Basi wapashe habari njema wale ambao katika wakati wa msiba husema tu: Sisi ni wa Mwenyezi Mungu na Kwake tutarejea. Hao wanapata baraka za Mungu na rehema Zake. Na hao ndio waliofikia upeo wa ukamilifu wa mwongozo. Ndiyo kusema kwamba hakuna utukufu katika ile elimu iliyojaa katika ubongo na moyo tu; bali elimu hasa ni ile inayotoka katika ubongo na sehemu zote za mwili zikaadibika na kupata athari yake, na kumbukumbu la ubongo likaonekana katika matendo. Basi njia kubwa ya kuimarisha elimu na kuikuza ni kudumisha athari zake katika sehemu zote za mwili. Elimu, hata kama ndogo namna gain, haiwezi kukamilika mpaka itumike katika matendo. Kwa mfano, tangu muda mrefu twajua kwamba kupika chapati ni kazi rahisi sana, wala haina ugumu wowote: ni kukanda tu unga

---

1 Al-Baqarah, 2:156-158

2 Aali'Imraan, 3:187

na kutengeneza madonge ya kiasi cha chapati moja moja, kisha kuchukua kila donge na kutengeneza sura ya mviringo kwa mikono mwili na kuweka juu ya chuma na kwa kuzungusha-zungusha na kupindua-pindua juu ya chuma cha moto na kisha kuoka kidogo, chapati itakuwa tayari imepikwa. Lakini hayo ni majivuno ya kielimu tu. Kwa kitendo tukianza kupika bila kuwa na ufundi, kwanza kabisa tutapata shida kuukanda unga sawa sawa, kwani pengine kwa sababu ya maji kidogo unga utakuwa mgumu kama jiwe, au kwa kutiwa maji zaidi ya kiasi utakuwa laini sana usiofaa kutengenezea chapati. Na kama kwa shida na taabu nyingi tutawahi kukanda unga vizuri kidogo, basi hali ya chapati itakuwa kwamba sehemu moja itaungua na sehemu nyingine itabaki mbichi, katikati itakuwa kama tembe na itakuwa na pembe nyingi wala haitakuwa ya mviringo, ilhali tuliona chapati ikipikwa kwa miaka hamsini. Kwa kifupi tutaharibu kilo nyingi za unga kwa sababu ya elimu tupu isiyokuwa na mazoezi kwa vitendo. Basi kama katika mambo madogo madogo hali yetu ya elimu ndiyo hii, twawezaje kuitegemea elimu tupu bila matendo katika mambo makubwa? Basi, Mwenyezi Mungu Anasema katika aya hizo kwamba shida ninazowapeni ndiyo elimu ya mazoezi, yaani kwa njia hii elimu yenu itakamilika.

Kisha Anasema mtajaribiwa kuhusu mali zenu na uhai wenu. Watu watanyang’anya mali zenu na

kuwaueni. Mtasumbuliwa na Wayahudi, Wakristo na Washirikina. Watasema maneno mengi ya kuwaudhi, lakini mkisubiri na kuepukana na matamshi yasiyofaa, hiyo itakuwa ni kazi yenu ya hima na ushujaa. Aya hizi zote zinamaanisha kwamba elimu yenye baraka ni ile inayong'aa katika vitendo. Na elimu mbovu ni ile inayobaki kuwa ujuzi tu lakini bado haijatendwa.

Tambueni kwamba jinsi mali inavyozidi na kustawi kwa njia ya biashara, ndivyo elimu inavyokamilika kiroho kwa njia ya kutenda sawa nayo. Na fahamuni kwamba elimu kufikia daraja la Hakkul-Yakin (Haki ya Yakini), ndiyo hii kwamba kila kona ya elimu hiyo ijaribiwe kimatendo. Ndivyo ilivyofanyika katika Islam. Mafunzo yote Mwenyezi Mungu Aliyowafunza watu kwa njia ya Kurani Tukufu, Akawapa nafasi wayang'arishe kimatendo na wajae nuru hiyo.

## ZAMA MBILI ZA MAISHA YA MTUME[saw]

Ndiyo sababu Mwenyezi Mungu aligawanya maisha ya Mtume wetu[saw] katika sehemu mbili: Sehemu moja iliyokuwa na taabu, misiba na mateso, na sehemu ya pili ya ushindi — ili zile khulka zipate kudhihirika zinazodhirika katika hali ya shida, na zithibitike pia zile khulka ambazo haziwezi kudhirika bila mtu kupata madaraka. Basi namna zote mbili za khulka za Mtume[saw] zilithibitika wazi kwa sababu ya yeye

kufikiwa na zama zote mbili na hali zote mbili. Kwa miaka kumi na mitatu mfululizo Mtume[saw] alipata mateso mjini Makka. Kwa kutaali historia yake ya zama hizo, inabainika kwamba Mtume[saw] alionyesha khulka zile wanazopaswa kudhihirisha wakweli waliokamilika katika hali ya taabu, kama vile kumtegemea Mwenyezi Mungu, kuepukana na kuondokewa na subira, kutokulegea katika juhudi na kutokumwogopa yeyote kwa heba yake. Akaonyesha khulka hizo kwa namna ambavyo makafiri wakamwamini kwa kuona uimara wake na wakashuhudia kwamba yule tu anayemtegemea Mungu aweza kudhihirisha uthabiti huo na kuvumilia mateso.

Na zilipowadia zama za pili, yaani zama za ushindi, madaraka na utajiri, Mtume[saw] akaonyesha khulka njema sana za msamaha, ukarimu na ushujaa kwa ukamilifu kiasi hiki kwamba kundi kubwa la makafiri likasilimu kwa kuziona khulka hizo. Akawasamehe waliomtesa, akawapa amani waliomfukuza mjini, akawapa mali nyingi waliokuwa na hali ndogo kati yao, na juu ya kuwa na madaraka akawasamehe maadui zake wabaya sana. Matokeo yake ni kwamba watu wengi walipoona khulka zake njema wakatoa ushahidi kwamba mtu hawezi kuonyesha khulka za aina hii mpaka awe ametumwa na Mungu na awe mkweli hasa. Ndiyo maana maadui zake waliondokewa na chuki nyoyoni mwao. Khulka

yake kubwa zaidi ilikuwa ni ile iliyotajwa ndani ya Kurani Tukufu, nayo ndiyo hii:

قُلْ إِنَّ صَلَاتِي وَنُسُكِي وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٦٣﴾ [1]

Yaani: Waambie, ibada yangu na dhabihu zangu na kufa kwangu na kuishi kwangu ni kwa ajili ya Mungu, yaani kwa kudhihirisha Jalali Yake na kwa kuwapa raha watu Wake ili wapate uzima kwa kufa kwangu. Kufa katika njia ya Mungu kwa kuwahurumia watu hakumaanishi kwamba, Mungu apishe mbali, Mtume[saw] alinuia kujiua hasa kama wajinga na wenye wazimu, kwa kudhani kwamba nikijiua kwa kitu kama upanga nitawanufaisha wengine. Bali yeye alikuwa anapinga vikali kitendo cha aina hii. Sawa na mafunzo ya Kurani, mwenye Kujiua ni mkosefu sana na anastahili kuadhibiwa vikali kama isemavyo:

وَلَا تُلْقُوا بِأَيْدِيكُمْ إِلَى التَّهْلُكَةِ [2]

Yaani: Msijiue, wala msiwe sababu ya kujiangamiza (2:196). Ni dhahiri kwamba kama Khalidi amepatwa na maumivu tumboni, itakuwa kazi bure ikiwa Zaidi anajipasua kichwa chake kwa kumhurumia Khalidi; bali anaponda kichwa chake bila haki kwa sababu ya ujinga wake. Ingekuwa kazi njema kumshughulikia

[1] Al-An'aam, 6:163
[2] Al-Baqarah, 2:196

Khalidi na kumtafutia dawa nzuri na kumtibu sawa na sheria za utibabu. Lakini kujipasua kichwa hakukumfaa Khalidi, bali ameiudhi sehemu ya muhimu ya mwili wake bila haki. Ilmuradi, aya hii inamaanisha kwamba Mtume[saw] alijitolea uhai wake kwa kuwahurumia watu na kujibidiisha kwa ajili yao ili kuwaokoa; na kwa kuwaombea na kuwahubiri na kuvumilia mateso kutoka kwao na kwa kila njia ya hekima akajinyima kila raha, kama Asemavyo Mwenyezi Mungu:

لَعَلَّكَ بَاخِعٌ نَّفْسَكَ اَلَّا يَكُوْنُوْا مُؤْمِنِيْنَ ۝٤ [1]

فَلَا تَذْهَبْ نَفْسُكَ عَلَيْهِمْ حَسَرٰتٍ ۭ [2]

Je, utajiangamiza katika huzuni na jitihada kubwa unayofanya kwa ajili ya watu? Je, utatoa uhai wako kwa kuwasikitikia wale wasiokubali ukweli? Basi, njia ya hekima kwa kuwahurumia watu ni kuvumilia shida katika njia ya kuwanufaisha, na kujitolea uhai katika kutekeleza mambo yafaayo kwa faida yao. Siyo kwamba tukiona watu katika taabu au upotevu na katika hatari, tujipige jiwe kichwani au kwa kumeza sumu ya mtongotongo tuage dunia na kudhani kwamba tumewaokoa watu kwa kitendo hiki cha kipuuzi. Hiyo siyo kazi ya wanaume, bali ni tabia ya wanawake. Na njia ya wenye moyo mdogo ndiyo

---

[1] Ash-Shu'araa, 26:4

[2] Faatir, 35:9

sikuzote kukimbilia haraka Kujiua kwa kuona shida fulani haivumiliki. Kujiua hivyo, hata ukitolewa udhuru gani baadaye, ni aibu kwa akili na wenye akili.

Pia yule mtu asiyepata nafasi ya kujilipiza kisasi, subira yake na kutokushindana kwake na adui haviwezi kuaminika, kwani hatujui angefanya nini kama angepata uwezo wa kujilipiza kisasi. Kama hapati zama za kupata mateso na kisha akajaliwa madaraka na utawala na utajiri, khulka zake za kweli haziwezi kudhihirika katu. Ni dhairi kwamba kama mtu akifa kwa kupigwa na watu katika hali ya unyonge, umaskini na kutokuwa na uwezo, bila kujaliwa zama za kupata madaraka, utawala na utajiri, khulka zake zozote hazitathibitika. Kama hakufika katika uwanja wa vita, haitajulikana kwamba alikuwa shujaa au mwoga. Hatuwezi kusema kitu kuhusu khulka zake, kwani hatuelewi angewatendeaje kama angepata uwezo juu ya maadui zake; na kama angetajirika, angejikusanyia mali ama angewapa watu; na kama angeingia katika medani angeikimbia vita ama angeonyesha ushujaa. Kwa fadhili za Mwenyezi Mungu na msaada Wake, Mtume[saw] alijaliwa nafasi ya kuonyesha khulka zote hizo. Ukarimu, ushujaa, upole, msamaha na adili vilidhihirika kwake katika mahali pake kwa ukamilifu sana hata kwamba mfano wake hauonekani juu ya uso wa dunia. Katika zama zote mbili za unyonge na nguvu, umaskini na utajiri, akaionyesha

dunia nzima kwamba yeye huyo mtukufu alijikusanyia khulka zote njema hata kwamba khulka yoyote haikubaki bali Mungu Alimpatia nafasi ya kuidhihirisha. Ushujaa, ukarimu, uimara, msamaha, upole na kadhalika khulka zote njema zilihakikika namna ambavyo kupata mfano wake duniani haiwezekani. Naam, ni kweli kwamba waliofikisha ukatili wao hadi upeo wa mwisho na kutaka kuiangamiza Islam, hawakuachwa na Mungu bila kuadhibiwa; kwani kuwaacha hivyo ingekuwa kuwaangamiza wakweli kwa kukanyagwa chini na miguu yao.

## SHABAHA YA VITA VYA MTUME[saw]

Shabaha ya vita vya Mtume[saw] haikuwa kuwaua watu bure na kumwaga damu. Yeye Mtume[saw] alifukuzwa katika nchi yake, na Waislamu wengine wanaume kwa wanawake wasio na hatia wakauawa; na wapinzani hata hivyo hawakutosheka na ukatili wao bali waliendelea kudhulumu na wakazuia mafunzo ya Kiislamu yasikubaliwe. Hapo sheria iliyowekwa na Mungu ya kujihifadhi ilitaka kuwaokoa waliodhulumiwa wasiangamie kabisa. Basi vita vilipiganwa na hao walioinua upanga kwanza. Ilmuradi, kwa kuondoa fitina ya wauaji, vita hivyo vilipiganwa kwa kujilinda na shari wakati wakatili walipotaka kuwaangamiza kabisa wenye ukweli. Katika hali kama hiyo kama Islam isingeshika njia

ya kujilinda, maelfu ya watoto na wanawake wasio na hatia wangeuawa na hatimaye Islam ingeangamia.

Kumbukeni kwamba wapinzani wetu wanakosea wanapofikiri kwamba mwongozo wa Mungu unapaswa kufundisha kutokupigana na maadui wakati wote hata ikitokea nini, na kudhihirisha mapenzi na huruma sikuzote kwa njia ya upole. Watu hao katika mawazo yao wanamtukuza Mungu Mwenye Enzi kwani wanadhani sifa zote za Mungu zinaishia katika upole na ulainifu. Lakini wenye kutafakari kwa makini habari hii, watatambua kwamba hilo ni kosa wazi wazi la hao watu. Sheria ya Mungu inayofanya kazi ulimwenguni ikichunguzwa, itajulikana kwamba sheria hiyo bila shaka ni rehema tupu kwa dunia. Lakini rehema hii haionekani sikuzote kwa sura ya upole na ulainifu; bali kwa sababu ya huruma tupu pengine inatunywesha sharubati tamu na pengine dawa chungu kama afanyavyo tabibu mahiri. Rehema yake kwa wanadamu ni kama kila mmoja wetu anavyojirehemu dhati yake. Hapana shaka kwamba kila mmoja wetu anapenda mwili wake mzima. Kama mtu akitaka kung'oa unywele wetu mmoja, twamkasirikia; lakini hata hivyo upendo wetu kwa mwili wetu umegawanyika katika sehemu mbalimbali za mwili. Twazipenda sehemu zote za mwili wetu wala hatutaki hasara ipatikane katika sehemu yoyote mojawapo ya hizo. Lakini ni kweli tupu pia kwamba upendo

wetu kwa sehemu mbalimbali za mwili wetu sio wa daraja moja, bali tunao upendo mwingi zaidi kwa sehemu zile za mwili zilizo za muhimu zaidi ambazo zinategemewa na shabaha zetu. Kadhalika upendo wetu kwa mwili mzima ni mwingi zaidi kuliko upendo wa sehemu moja ya mwili. Basi wakati wowote tunapoona kwamba hakuna budi kuijeruhi sehemu fulani au kuikata au kuivunja ili kuokoa sehemu nyingine iliyo muhimu zaidi, hapo kwa kuokoa maisha tunakuwa tayari bila kusita kuijeruhi sehemu hiyo au kuikata. Na ingawaje twahuzunika kwa kuijeruhi au kuikata hiyo sehemu tunayoipenda, lakini twalazimika kuikata ili isije maradhi ya hiyo sehemu yakaiangamiza sehemu ile iliyo ya muhimu zaidi. Basi twapaswa kutambua kwa mfano huu kwamba Mungu Anapoona kwamba wakweli wanaangamia kwa mikono ya waongo na amani inachafuka, hapo kwa kuokoa maisha ya wakweli na kuondolea mbali uchafuzi, Analeta mpango ufaao kutoka mbinguni au ardhini, kwani kama Alivyo mwingi wa rehema, kadhalika Yu mwingi wa hekima pia. Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu.